ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe.Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais

20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe.Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake

43. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo

44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo

45. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake

46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni

47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje

48. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe

49. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini

50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo

51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani

52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando

53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu

54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini

59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole

61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani

62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani

65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy - Jimbo la Chaani

66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni

67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde

68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni

70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chake Chake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini na Nane - Tarehe 15 Juni, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Spika: Ahsante Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa ajili ya kuweka Hati Mezani.

Mhe. Mohammed Said Mohammed Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti): Mhe. Spika kwa heshima kubwa sana na kwa idhini yako naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Serikali ya Zanzibar na Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2017/2018. Mhe. Spika, kwa heshima kubwa sana naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2017/2018

(Majadiliano yanaendeelea)

Mhe. Spika: Ahsante sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ili sasa nae aje awasilishe sasa. Mwenyekiti Kamati ya Bajeti kwa niaba yake namuona Mhe. Abdalla Ali Kombo. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Ali Kombo (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti): Naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Serikali, Mwelekeo wa Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Utangulizi:

Mhe. Spika, Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena katika chombo hichi muhimu tukiwa wazima wa afya, ili kutekeleza majukumu yetu ya kikatiba ya kuwatumikia wananchi katika Mkutano huu wa Bajeti kwa kujadili, kushauri na hatimae kupitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati yangu ya Bajeti, napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya awali kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali, Mwelekeo wa Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha

2017/2018. Kwa namna ya pekee naomba pia kutumia fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bajeti pamoja na Makatibu wa Kamati kwa kutumia muda wao mwingi kuipitia na kuifanyia uchambuzi bajeti na kutoa michango yao mizuri sana katika ngazi ya Kamati wakati tulipokaa na Watendaji wa Serikali.

Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba niwatambue kwa majina Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Mohammed S. Mohammed (DIMWA)	Mwenyekiti
2.	Mhe. Bahati Khamis Kombo	M/Mwenyekiti
3.	Mhe. Shehe Hamad Mattar	Mjumbe
4.	Mhe. Simai Mohammed Said	Mjumbe
5.	Mhe. Asha Abdalla Mussa	Mjumbe
6.	Mhe. Zulfa Mmaka Omar	Mjumbe
7.	Mhe. Abdalla Ali Kombo	Mjumbe
8.	Ndg. Abdalla Ali Shauri	Katibu
9.	Ndg. Kassim Tafana Kassim	Katibu

Mhe. Spika, Kamati yangu inapenda kumpongeza kwa dhati Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa jitihada zake anazoendelea kuzichukua katika kuhakikisha nchi yetu inapata mafanikio ili kuwaondolea wananchi shida zinazowakabili. Aidha, Kamati yangu inaunga mkono jitihada za Mhe. Rais katika kuhakikisha nidhamu, uwazi na uwajibikaji kwa watumishi wa umma katika kusimamia mali za Serikali. Kwa dhati kabisa tunamuomba Mwenyezi Mungu amlinde, kutokana na husda na wale wote wanaomtakia mabaya na wasiopenda kuona juhudi hizo zinaendelea. Kimsingi jitihada hizo zitasaidia kuimarisha utendaji wa Serikali ambao ni msingi muhimu katika kufikia malengo ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watakumbuka kuwa katika hatua za mwanzo kuchukuliwa na Uongozi wa Baraza letu ni kutupatia wataalamu ambao walituongezea uelewa wetu katika shughuli za Baraza ikiwemo bajeti. Tulielezwa kuwa Bajeti ni mpango ama mkataba wa namna Serikali itakavyokusanya na kutumia pesa za wananchi. Mchakato wa bajeti unasimamiwa na sheria kadhaa, ikiwemo Katiba yetu ambayo ndiyo sheria mama iliyo juu yetu sote. Hivyo ni wajibu wetu kusimamia ipasavyo mwenendo mzima wa bajeti ili wananchi ambao ndio waajiri wetu waridhike na kazi muhimu tunayoifanya. Kulitekeleza hili ipasavyo, Kamati yangu haitokuwa na muhali katika kusema kweli na kutenda haki kwani kuendekeza muhali ni kuwaacha wachache wanufaike huku wananchi wetu walio wengi wakiathirika; hiyo si haki na hatuko tayari kuonekana tukiwa ni sehemu ya wachache hao.

Mhe. Spika, Kamati yangu inashauri Serikali kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria, watendaji wa Serikali ambao kwa makusudi au kwa uzembe wanakiuka maadili ya kazi katika dhamana zao walizokabidhiwa na ambao kupitia taarifa mbali mbali za Kamati za Kudumu za Baraza lako tukufu, wamebainika kutumia vibaya dhamana zao walizo kabidhiwa.

Mhe. Spika, kuwachukulia hatua watendaji hao sio tu italeta nidhamu ya uwajibikaji katika utumishi wa umma, lakini pia itasaidia kukijengea heshima chombo chetu hichi ambacho hutumia muda na fedha nyingi za wananchi katika kutimiza wajibu wake wa kikatiba wa kuisimamia Serikali. Aidha, hatua hiyo pia itaonesha taswira nzuri ya mgawanyo wa madaraka kisheria baina ya mihimili mikuu mitatu ya dola (Serikali, Baraza la Wawakilishi na Mahkama), katika kutekeleza dhana nzima ya "*Check and Balance*".

Mhe. Spika, wakati wa kupitia Mapendekezo ya bajeti, Mwelekeo wa Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2017/2018, Kamati yangu ilipata kukaa na Waziri wa Fedha na Watendajii wa Wizara hiyo pamoja na Wizara nyengine, kwa lengo la kuipatia Kamati ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizoibuka.

Mhe. Spika, Serikali sikivu kama ilivyo hii yetu huandaa mazingira shirikishi katika mambo yake mbalimbali ikiwemo ya Bajeti. Kamati yangu ilipata fursa ya kukaa na wadau "*Stakeholders"* mbalimbali kwa lengo la kupata maoni yao kuhusu Mwelekeo wa Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Katika mchakato huo, tumeamini kuwa pindi zikishirikishwa ipasavyo Jumuiya za kiraiya na zile za Sekta Binafsi zina michango mikubwa na muhimu katika kupata bajeti zilizo bora kitaifa na kisekta. Mfano, mbali ya kuchangia asilimia kubwa ya mapato ya kodi ya ndani, sekta binafsi hupaswa hushiriki kikamilifu katika mashauriano ya muundo wa kodi. Hoja zao mara nyingi huzingatiwa wakati wa kutunga na kupitia upya kodi.

Mhe. Spika, mashirikiano ya wadau hao yamekuwa na msaada muhimu sana katika kuiwezesha Kamati yetu kukamilisha jukumu hili kikanuni, na Kamati yangu inathamini sana michango ya wadau hao. Hivyo, kwa dhati kabisa tunapenda kuwashukuru wadau wote walioshiriki katika vikao vya pamoja na Kamati yetu, kwa kukubali mualiko wa Kamati yetu na kutowa maoni yao ambayo pia yamezingatiwa katika kuandaa taarifa ya Kamati.

Hata hivyo, wadau hao wametupa salamu zao ambazo naomba kuziwasilisha kama tulivyoahidi; mara kadhaa walitujulisha kuwa ushirikishwaji wao katika uandaaji wa bajeti za mawizara haukufikia kiwango kinachoridhisha. Baadhi ya Wizara ni mashuhuda kuwa zilijifungia na kutayarisha bajeti zao bila hata kuthamini michango ya taasisi za kiraiya na Sekta Binafsi zilizo katika sekta zao, hii ni kasoro. Hawa ni wahusika muhimu, si washindani. Kamati yangu ilifaidika sana na michango yao ambayo tunaamini wangeshirikishwa ipasavyo na Wizara mbalimbali za Kisekta basi hata bajeti za Wizara hizo zingekuwa katika hali ya ubora zaidi.

Mhe. Spika, Kamati yangu pia inapenda kumshukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndg. Raya Issa Msselem pamoja na wasaidizi wake, kwa kuiwezesha Kamati yetu hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuipatia mafunzo ya awali ya kuijengea uwezo, pamoja na ziara ya kujifunza katika Bunge la Jamhuri la Tanzania huko Dodoma. Aidha, Kamati yangu inamshukuru sana Spika wa Bunge la Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kupitia kamati yake kwa mashirikiano mazuri waliyotupa wakati huo katika ziara ya kujifunza Bungeni Dodoma.

Mhe. Spika, shukurani maalum naomba ziende kwa wananchi wangu wa Jimbo langu la Mwanakwerekwe kwa kuendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu ya kuwatumikia. Naomba waendelee kuniombea ili niweze kuwatumikia na kupeleka mbele maendeleo ya jimbo letu, wote kwa ujumla nawapongeza ahsanteni sana Mwenyenzi Mungu awape baraka katika maisha yenu Amin. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kimsingi kabla ya kuanzishwa kwa Kamati ya Bajeti, majukumu ya Kamati hii yalikuwa yanatekelezwa na Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. Hata hivyo, Kamati ya Wenyeviti haikuwa na fursa pana ya kusimamia Bajeti ya Serikali pamoja na kuishauri Serikali katika mchakato mzima wa Bajeti kutokana na uchache wa muda ambao ilitengewa kwa ajili ya kazi hiyo. Aidha, kwakuwa Wajumbe wa Kamati ya Wenyeviti walikuwa ni Wajumbe wa Kamati nyengine za kisekta, wasingeweza kutekeleza majukumu ya Kamati mbili za kisekta kikamilifu. Hivyo, ni matarajio yetu kwamba, kuanzishwa kwa Kamati ya Bajeti kutatoa fursa pana kwa Baraza la Wawakilishi kushirikishwa kikamilifu katika mchakato wa bajeti katika hatua tofauti, ikiwa ni pamoja na kuishauri Serikali ipasavyo kuhusu Bajeti ya Serikali, Mipango ya Maendeleo pamoja na sera za kodi.

Mhe. Spika, matarajio hayo hayatofikiwa ikiwa Baraza la Wawakilishi pamoja na Serikali kwa pamoja watashindwa kufuata maelekezo ya Kanuni za Baraza, ambazo zimetoa msingi mzuri wa utaratibu wa uwasilishaji na ushirikishwaji wa Baraza katika mchakato wa Bajeti, sambamba na kuzingatia umuhimu wa kuanzisha Sheria ya Bajeti ambayo itaweka utaratibu mzuri na ufafanuzi wa mipaka na majukumu ya kila muhusika katika mchakato wa uandaaji wa Bajeti "*Budget Process".*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa nichukue fursa hii kwa mujibu wa maelekezo ya Kanuni ya 94(9) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2016, niwasilishe maoni ya Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Serikali, Mwelekeo wa Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI NA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

UKUAJI WA UCHUMI

Mhe. Spika, Uchumi wa Zanzibar umendelea kuimarika ukilinganisha na nchi za Afrika Mashariki na Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, ambapo ukuaji wa uchumi katika nchi za Afrika Mashariki ulifikia wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2016, Uchumi wa Zanzibar kwa wastani wa asilimia 6.8. Aidha, kwa mwaka 2017/2018 uchumi wa Zanzibar unatarajiwa kuendelea kuimarika na kufikia wastani wa asilimia 7.1. Kamati yangu inapongeza jitihada zinazochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha uchumi wa Zanzibar unaendelea kukua. Hata hivyo, Kamati yangu inashauri ukuaji huo wa uchumi

uakisi maendeleo ya jamii kwa kuzingatia matumizi na mgawanyo sahihi wa rasilimali za taifa ambao utapunguza umasikini wa kipato kwa mwananchi wa kawaida. Vilevile, mafanikio hayo ya ukuaji wa Uchumi yatafsiriwe sambamba na shabaha za Mipango ya kitaifa na kimataifa inayotuongoza, ikiwemo MKUZA, Dira ya Maendeleo ya 2020 pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Mhe. Spika, Kamati yangu pia inashauri Serikali kufanya juhudi za makusudi katika kuwaelimisha wananchi kupitia vipindi vya Televisheni na Redio, kuhusu dhana nzima ya ukuaji wa uchumi na viashiria vya ukuaji wa uchumi, kwa kuwa mara nyingi wananchi wengi wanapata tabu kuelewa wanapoelezwa kwamba uchumi umekuwa, ambapo kwa mwananchi wa kawaida hulinganisha dhana ya ukuaji wa uchumi na gharama za maisha pekee, hususan katika suala la kupanda kwa bei za bidhaa ambazo huathiri moja kwa moja uwezo wa kutumia yaani "*purchasing power".*

PATO LA TAIFA NA PATO LA MTU MMOJA MMOJA

Mhe. Spika, Pato la Taifa(GDP), limeongezeka kutoka TZS 1,188 bilioni mwaka 2015, hadi kufikia 1,628 TZS bilioni mwaka 2016. Aidha, pato la mtu binafsi (*GDP per Capital*) limeongezeka kutoka Dola za Kimarekani 818 mwaka 2015, hadi kufikia Dola 830 mwaka 2016.

Kimsingi, takwimu hizi pia zinaonesha kuimarika kwa hali ya Uchumi wa taifa lakini pia maisha ya mtu mmoja mmoja.

Mhe. Spika, Kamati yangu inapongeza ufanisi huo uliopatikana wa kuongezeka pato la Taifa pamoja na pato la mtu mmoja mmoja. Hata hivyo, Kamati yangu inashauri ni vyema tukajiridhisha kama kuongezeka kwa pato la taifa kumemsaidia kupunguza tatizo la umasikini hasa kwa wananchi wa vijijini, kwakuwa tafiti zinaonesha kuwa umasikini wa mijini umepungua lakini umasikini wa vijijini hali imebakia kuwa sawa. Aidha, kwa kuwa ukuaji huu wa Pato la mtu mmoja mmoja *(GDP per capita)* umelenga kufikia malengo ya Dira ya 2020 ambayo ni kufikia Dola 3,000 itakapofika mwaka 2020. Kamati yangu inashauri kiwango cha Dola 3,000 kilichowekwa katika Dira hiyo kifanyiwe mapitio *"review*" sambamba na viwango vyengine vilivyowekewa malengo kwa fedha za kigeni. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Kamati yangu imebaini hakuna mapitio yaliyofanywa katika viwango na shabaha hizo licha ya ukweli kwamba viwango hivyo vimewekwa kwa fedha za kigeni ambapo ndani ya kipindi cha utekelezaji wa Dira hiyo, tumeshuhudia mabadiliko makubwa ya kupanda thamani ya Dola ya Marekani dhidi ya fedha ya Shilingi ya Tanzania.

Mhe. Spika, kwa mantiki hiyo inawezekana kabisa kiwango hicho cha Dola za Kimarekani cha Dola 3,000 tayari tumeshakifikia, hasa tukizingatia kwamba Pato la Taifa tunalipima kwa thamani ya Shilingi ambayo inashuka thamani mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, mwaka 2000 Dola moja ya Marekani iliuzwa kwa thamani ya TZS 820, mwaka 2005 Dola moja ya Marekani iliuzwa kwa thamani ya TZS 1,050, mwaka 2010 Dola moja ya Marekani iliuzwa kwa thamani ya TZS 1,260.

THAMANI YA SHILINGI NA MFUMKO WA BEI

Mhe. Spika, Thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani, imeendelea kupungua ambapo kwa mwaka 2016, imepungua kwa wastani wa asilimia tisa (9). Kwa kuwa Jukumu la Msingi la Udhibiti wa thamani ya Shilingi (TZS) liko kwa Benki Kuu ya Tanzania –BOT kupitia sera za kifedha "*Monitory Policy*"ambazo huzichukua katika kuweka hali ya uchumi kuwa imara. Aidha, kwa kuwa athari za kushuka ama kupanda kwa thamani ya shilingi, zinaathiri pia uchumi wa Zanzibar kutokana na kuwa na sarafu moja, ni vyema kwa Benki Kuu (BOT) wakati wa kufanya
mapitio ya hali ya uchumi pamoja na mipango ya sera za kifedha wakashirikiana kwa karibu sana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) katika Mipango na maamuzi hayo.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine, kwa kuwa Zanzibar ni sehemu ya Tanzania ambayo chumi zake mbili zinaingiliana, inapaswa kuchukua hatua za kuongeza uzalishaji wa ndani ili kupunguza kiwango cha uagizaji wa bidhaa kutoka nje "*importation"* ambao ni miongoni mwa sababu zinazopelekea kushuka kwa thamani ya fedha ya nchi kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya kununua bidhaa. Hivyo, ushirikishwaji wa Sekta Binafsi ya Zanzibar katika maamuzi muhimu yanayowagusa wananchi ni wajibu wetu ambao hauepukiki. Tumekuwa tukishuhudia kwa upande wa Tanzania Bara vipi wanaishirikisha Sekta Binafsi katika maamuzi kama hayo, na hata katika safari za viongozi wakuu wa nchi za nje huwa pamoja.

MFUMKO WA BEI

Mhe. Spika, Nchi za Afrika Mashariki zimefanikiwa kwa kiasi kikubwa kudhibiti mfumko wa bei na kubakia katika tarakimu moja, ikiwa na wastani wa asilimia 5.1. Aidha, Mfumko wa bei wa Zanzibar umepanda hadi kufikia asilimi 6.7 mwaka 2016, kutoka asilimia 5.7 mwaka 2015.

Mhe. Spika, Miongoni mwa sababu ya msingi iliyosababisha kupanda kwa mfumko wa bei wa Zanzibar ni ongezeko la bei za bidhaa za chakula, ambao unasababishwa na uzalishaji mdogo wa ndani wa bidhaa hizo. Hali hii inapelekea nchi kutegemea zaidi kuagiza "*import*" bidhaa za vyakula nje ya nchi pamoja na Tanzania Bara. Mfumko wa bei unaathiri sana uwezo wa wananchi katika kutimiza mahitaji yao ya kila siku, hususani ya bidhaa za chakula ambayo ni mahitaji ya lazima "*necessary demand*". Kamati yangu inaishauri Serikali kuweka mikakati madhubuti kuhakikisha uzalishaji wa ndani wa chakula unaongezeka ili kupunguza tatizo la kupanda kiholela kwa bei za bidhaa hizo.

MAENDELEO YA KILIMO

Mhe. Spika, kwa kuwa Kilimo ni miongoni mwa sekta mama kwa uchumi wa nchi yetu, na kwa kuwa eneo la Ardhi ya Kilimo Zanzibar ni ndogo, Kamati yangu inaishauri serikali iweke mipango mizuri ya matumizi ya rasilimalli ya ardhi. Aidha, serikali iangalie uwezekano wa kutumia kisiwa cha Pemba na maeneo ya Kisiwa cha Unguja yenye rutba katika kuhamasisha uanzishaji wa kilimo cha kisasa "*Green House*" baada ya kufanya utafiti wa udongo ili kujuwa aina ya mazao yatakayoweza kulimwa. Hili

litasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza uzalishaji wa chakula pamoja na kuwapatia ajira wananchi na hatimaye kupunguza mfumko wa bei ambao huwa unakula sehemu kubwa ya kipato halisi cha wananchi wetu. Sambamba na hilo, serikali iangalie uwezekano wa kuishauri Benki ya Maendeleo ya Kilimo iliyopo Tanzania Bara kufungua Tawi Zanzibar , ili wananchi wa Zanzibar nao wapate fursa ya kupata mikopo nafuu ya kilimo ili kujiimarisha katika kuwekeza katika kilimo na hatimae kuwawezesha wananchi kujiajiri wenyewe. Serikali pia iwawezeshe wakulima wadogo wadogo kwa kuongeza fungu la uwezeshaji kwa vijana "*Guarantee Fund"* kupitia Wizara ya Uwezeshaji wa Vijana ili vijana wengi zaidi wanufaike na fedha hizo.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine Kamati yangu inashauri serikali iweke mipango madhubuti ya kusimamia matumizi bora ya ardhi pamoja na kuwawezesha wakulima kwa kuwapatia taaluma pamoja na nyezo za kisasa, ambazo zitawawezesha kuzalisha kwa faida na kwa kiwango kikubwa. Aidha, hatua hizo ziende sambamba na kuwatafutia wakulima masoko ya uhakika ya bidhaa zitakazozalishwa.

MPANGO WA KUKUZA UCHUMI NA KUPUNGUZA UMASIKINI MKUZA III

Mhe. Spika, serikali imeanza kutekeleza mpango mpya wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini- MKUZA III, ambao utakuwa ndio muongozo wa kuweza kufikia Mpango Mkuu wa Dira ya Maendeleo ya 2020. Kamati yangu imepata hofu juu ya uelewa wa wananchi kuhusu Mpango huu, lakini pia kwa baadhi ya Wajumbe wa Baraza lako hili.

Mhe. Spika, ili tuweze kufanikiwa katika mipango yetu tunayojiwekea ni lazima sote tunzungumze lugha moja wakati wa utekelezaji wa mipango yetu. Kamati yangu imepata hofu hiyo kutokana na kupata taarifa kwamba, wakati watendaji wa Tume ya Mipango walipokuwa wakifanya utafiti katika Mkoa wa Kaskazini Unguja katika kijiji cha Nungwi kujua uelewa wa wananchi kuhusu MKUZA, mmoja wa wanakijiji aliulizwa anaufahamu vipi MKUZA , mwanakijiji huyo naye aliuliza "Huo Mkuza ni Chama gani cha Siasa?".

Mhe. Spika, hii inaonesha wazi ni kwa kiasi gani wananchi hawaelewi Mipango ya kitaifa ambayo inatekelezwa na Serikali. Na hapa ndipo tunaona vipi jumuiya za kiraiya zingeweza kufikisha elimu kwa jamii pindi zikiwezeshwa kutekeleza jukumu hilo.

Mhe. Spika, Kamati yangu inashauri serikali ichukuwe jitihada za makusudi katika kuwaelimisha na kuwashirikisha wananchi wakati wa kuandaa na kutekeleza Mipango ya Kitaifa, ambayo kimsingi wao ni sehemu ya Utekelezaji wa Mipango hiyo.

MAMLAKA YA UWEKEZAJI VITEGA UCHUMI - (ZIPA)

Mhe. Spika, Mamlaka ya Uwekekezaji Vitega Uchumi Zanzibar- ZIPA inajukumu kubwa la kuhamasisha Wawekezaji kuja kuekeza nchini na hatimae kuchochea ukuaji wa Uchumi kutokana na kodi mbali mbali ambazo wawekezaji hao wanalipia. Aidha, kupitia

miradi hiyo wananchi wanaweza kufaidika na ajira za moja kwa moja pamoja na ajira nyengine zinazoambatana na uendeshaji wa miradi hiyo.

Mhe. Spika, taarifa ya Serikali ya Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 inaonesha kwamba, uwekezaji wa Miradi iliyoidhinishwa na Mamlaka hiyo umeshuka kutoka miradi 36 yenye thamanai ya Dola 346.8 milioni mwaka 2015, hadi miradi 16 tu yenye thamani ya Dola 150.5 mwaka 2016. Aidha, kutokana na kushuka kwa utekelezaji huo pia kumepelekea kushuka kwa idadi ya ajira kutoka ajira 1,597 mwaka 2015 hadi ajira 1,071 mwaka 2016.

Mhe. Spika, takwimu hizi hazileti taswira nzuri kwa Mamlaka ya ZIPA na nchi yetu kwa ujumla, hasa tukizingiatia kwamba, sababu za msingi zilizopelekea kushuka kwa uekezaji huo hazijabainsihwa. Mhe. Spika, ili kuweza kuhamasisha na kuvutia wawekezaji hususani wa miradi mikubwa, hatuna budi kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji kwa kuondosha vikwazo visivyo vya lazima. Sambamba na kuweka miundombinu imara itakayovutia wawekezaji ikiwemo huduma ya maji safi, barabara pamoja na umeme wa uhakika lakini pia kuzingatia suala zima la usalama wa wageni.

Mhe. Spika, ingawa zaidi ya miongo mitatu imepita tokea Sheria ya Vitega Uchumi kupitishwa na Baraza lako tukufu, ZIPA bado haijaweka mazingira mazuri kwa wawekekezaji si wa nje tu *(Foreign Direct Investment)* bali hata. Uwekezaji wa ndani *(Domestic Direct Investment)* umekuwa haufaidiki na vivutio vilivyo katika Sheria yetu ya Kuendeleza Vitega Uchumi. Umefika wakati kuifanyia mapitio yakinifu Sheria yetu hii ambayo imepitiwa mara kadhaa lakini bado mwananchi mzalendo hanufaiki na utaratibu uliopo hadi sasa.

Mhe. Spika, mazingira ya kufanya biashara Zanzibar bado ni magumu na hayamshawishi muwekezaji kuja kuekeza hapa visiwani. Ukiacha mahoteli, idadi ya viwanda vinavyofunga shughuli zake inaongezeka na kuikosesha nchi mapato, ajira na uhaulishaji teknolojia. Hali hii inaenda kinyume na matarajio ya Dira *"Vision"* ya Mamlaka hiyo ya kuifanya Zanzibar kuwa kituo cha kuvutia na cha ushindani kiuwekezaji kikanda na Kimataifa yaani *"To make Zanzibar an Attractive and Competetitive Investment Destination Regionaly and Globaly"*

Mhe. Spika a aidha, ZIPA wameshindwa kutekeleza dhana ya "*One Stop Centre"* kama ambavyo ilitarajiwa, ambapo kwa sasa hivi ni taasisi mbili tu za Idara ya Kazi na Idara ya Uhamiaji "*Labour and Immigration"* ndio zimeweka afisi zao ZIPA kutekeleza dhana ya "*One stop Center*", huku taasisi nyengine muhimu zinazohusiana na Mapato, Ardhi na Leseni bado hazijaweka wawakilishi wao. Sambamba na hilo, pia Kamati yangu ilipokaa na wadau iliarifiwa kwamba, imekuwa ni kawaida kwa Mamlaka ya Uwekezaji ZIPA kuwaita wawekezaji na kuwaahidi misamaha, lakini wawekezaji hao wanapokuja hawapatiwi au wanacheleweshewa kupatiwa misamaha ya kodi pamoja na vibali, mapungufu hayo kwa ujumla wake yanavunja moyo wawekezaji.

Mhe. Spika, Kamati yangu imearifiwa kwamba, serikali imeunda Kamati ya wataalamu kuifanyia mapitio dhana ya "*One Stop Center*" ili iweze kufanya kazi. Kwa kuwa serikali

imebaini udhaifu uliokuwepo katika Mamlaka ya ZIPA, kimsingi Kamati yangu inapongeza na inathamini juhudi hizo za Serikali. Ni imani yetu kuwa Hadidu Rejea za Kamati hiyo zinajumuisha pia uwezo wa kiutendaji wa raslimali watu katika Mamlaka ya ZIPA. Kamati yangu inashauri serikali kukamilisha haraka mchakato wa kuipitia ripoti iliyotolewa na Kamati hiyo, ili kuandaa mikakati ambayo itahakikisha uwekezaji unaongezeka kwa kuongeza ufanisi wa Utendaji katika Mamlaka ya ZIPA.

Mhe. Spika, hilo wakati linafanyika Kamati yangu inaishauri serikali kutuwasilishia katika Baraza katika kipindi kufupi kijacho mikakati iliyoipanga kuendeleza uwekezaji wa ndani *(Domestic Direct Investments)* ili wananchi wanaounga mkono jitihada za kuwafikishia huduma wananchi wenzao kama vile kuekeza katika kutoa huduma za afya, elimu na kadhalika, waone kuwa Serikali yao inathamini michango yao. Tukumbuke kuwa, wawekezaji hawa wa ndani wamekuwa wakitumia mitaji yao kufanikisha huduma hizo nchini kwao bila kuwepo taasisi zozote za kifedha ambazo zingewapa mitaji kwa gharama nafuu.

Mhe. Spika, naomba tutambue na tupongeze taasisi za elimu, maduka ya madawa baridi, vituo vya afya na hospitali zote binafsi ambazo hazipewi ruzuku ya aina yoyote pamoja na kusaidia kwao kuokoa mabilioni ya fedha ambayo yangetumwa nje ya nchi laiti wasingetoa huduma hizo hapa hapa nchini. Tukitoa pongezi hizo, serikali iziangalie kwa jicho la huruma na kuzisaidia ili huduma wanazotoa ziwe bora zaidi na ziendelee kutoa fursa za ajira wa wananchi wetu.

Mhe. Spika**,** serikali imetenga eneo la Mangapwani lenye ukubwa wa kilomita sita (6) kwa ajili ya shughuli za Mafuta na Gesi Asilia. Hata hivyo, Kamati yangu inashauri serikali iangalie upya matumizi sahihi ya eneo hilo, kwa kuwa eneo hilo ni kubwa na upo uwezekano wa kutumika kwa shughuli nyengine za ziada za uwekezaji sambamba na malengo yaliyopangwa awali. Hapa tuanaiomba serikali ifanye utafiti zaidi juu ya ukubwa wa eneo lilotengwa na mahitaji halisi kwa ajili ya shughuli hiyo, kwa kuangalia uzowefu wa nchi mbali mbali na uhalisia wa mahitaji yetu.

Mhe. Spika, eneo la Mangapwani lina bandari ya asili, aidha mazingira ya kuanzisha bandari Mangapwani ni mazuri na pia ni rahisi (mara tatu zaidi ya gharama za kujenga bandari eneo la Mpiga Duri), kutokana na uwepo wa kina kikubwa cha maji. Hivyo, Kamati yangu inaishauri serikali iangalie uwezekano wa kutumia eneo la kilomita nne (4) kwa ajili ya kuanzisha bandari ambapo gharama za kujenga bandari ni ndogo sana, pia eneo hilo linawezekana kutumika kwa ajili shughuli za viwanda. Kamati yangu inatambua kwamba serikali imeshafanya maamuzi kuhusu ujenzi wa Bandari ya Mpiga Duri, ikiwa ni pamoja na kusaini mkataba wa ubia na Mkataba wa ujenzi kwa ajili ya Ujenzi wa Banadari hiyo. Hata hivyo, serikali inaweza ikaanza kupanga mikakati ya baadae kuhusu namna bora ya kulitumia eneo la Mangapwani kama ambavyo Kamati yangu imeshauri.

UWEKEZAJI WA CCTV MKOA WA MJINI MAGHARIB

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetumia TZS 18 bilioni kwa ajili ya uwekaji wa CCTV Kamera na vifaa vya ulinzi kwa ajili ya kuimarisha shughuli

za ulinzi na usalama. Aidha katika mwaka wa fedha 2017/2018 mradi huo pia umepangiwa jumla ya TZS 20,000,000 Kamati yangu inafahamu umuhimu wa kuimarisha hali ya usalama wa nchi yetu ambapo, kimsingi tunathamini juhudi za Serikali. Hata hivyo, hofu ya Kamati yangu ni juu ya uhalali wa maamuzi hayo, kwa kuwa nchi yetu inamahitaji mengi ya msingi ya huduma za jamii. Aidha, Kamati yangu inapata hofu namna ambavyo Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba kutakuwa na utunzaji yaani "*mantanance"* mzuri wa vifaa hivyo ili thamani ya vifaa hivyo ionekane. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, mara nyingi tumekuwa hodari wa kuanzisha mambo mazuri lakini kwenye suala la utunzaji inakuwa ni changamoto kubwa. Hili ni kutokana na ukweli kwamba kumekuwa na malamiko ya kutokuwepo bajeti ya matengenezo kwa baadhi ya hospitali, vifaa na mitambo inayonuliwa, ambapo mara nyingi bajeti inayowekwa ni ya manunuzi tu.

Mhe. Spika, unapokuwa na rasilimali chache yaani "*limited resources*" na mahitaji mengi unatakiwa ufanye maamuzi sahihi, ambapo utalazimika kuchagua jambo moja kwa gharama ya jengine yaani "*Opportuniy Cost*". Ikiwa Serikali imechagua kuweka Kamera za Ulinzi, Kamati yangu inasisitiza Serikali ihakikishe tija na malengo ya vifaa hivyo yapatikane kwa kuwa fedha zilizotumika ni nyingi sana. Kwa kuzingatia hali halisi ya uchumi wetu kuwa ni mdogo fedha zilizotumika katika mradi huo zingeweza kutumika katika kuimarisha huduma za kijamii ambazo wananchi wanazihitaji ikiwemo huduma za maji safi, afya na elimu. Hivyo, ili kuyafanya matumizi hayo kuwa na tija ni vyema Serikali ikahakikisha inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya utunzaji wa vifaa hivyo.

SEKTA YA AFYA

Mhe. Spika, Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa jitihada inazozichukuwa katika kuimarisha huduma za Afya ambapo mafanikio mbali mbali yameelezwa kwenye waraka wa Mapitio ya Hali ya Uchumi wa mwaka 2016/2017, ikiwemo ununuzi wa "*Tele medicine*" ambayo itatoa huduma za matibabu kwa mtu alie masafa ya mbali. Aidha, kukamilika kwa Hospitali ya Abdalla Mzee kumeweza kupunguza tatizo la kufuata vipimo vingi Dar es Slaaam na Unguja ikiwemo vipimo vya *MRI, CT Scan, Utra Sound* na *X Ray*, kimsingi hii ni hatua ya kusifiwa. Hata hivyo, Kamati imepata taarifa kuwa, kuna uchache wa wataalamu wa kuvitumia vifaa hivyo.

Mhe. Spika, vile vile Kamati yangu inaishauri Serikali ihakikishe vifaa vilivyonunuliwa vinapata matunzo mazuri kwa kuwekewa fungu la kutosha la kufanyia matengenezo pamoja na huduma nyengine zinazopaswa kufanyiwa vifaa hivyo ili viweze kudumu kwa muda mrefu. Ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa wataalamu wa Afya Kamati yangu inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kuajiri Watalamu kutoka Tanzania Bara. Aidha, hatua hiyo iende sambamba na mikakati ya kuwatunza wataalamu wetu, ikiwemo suala zima la kuwaongezea maslahi yao na kuwafundisha wataalamu wetu.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo Kamati yangu imeona ni vyema kulipa uzito maalum kutokana na kugusa moja kwa moja wananchi, ni suala la kununuliwa kifaa cha *DNA*, ambacho kimekua ni kilio cha muda mrefu kwa wananchi na imeonekana kuwa kutokuwepo kwa kifaa hicho, ni kikwazo kikubwa kwa kesi za udhalilishaji. Kwa kuwa katika mazingatio ya Maagizo ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali

imeongeza bajeti ya Ununuzi wa Dawa, Chanjo, na vifaa tiba hadi kufikia Tsh. Bilioni 8,000,000,000. Kamati yangu inashauri kupitia fedha hizo suala la kununuliwa kifaa cha *DNA* liwe kipaumbele, ili kumaliza tataizo la kusuwasuwa kwa kesi za udhalilishaji kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba kukariri tena umuhimu wa Serikali kuunga mkono jitihada zinazochukuliwa na wananchi wenzetu katika kuanzisha utoaji huduma za afya zilizo bora. Kwa kuwa huduma hizi huwagusa wananchi moja kwa moja, tofauti na miongoni mwetu wenye uwezo wa kutibiwa nje ya nchi, basi ni vyema kuweke utaratibu wa kuwapa unafuu wa kodi wanapoingiza vifaa vitavyotumika katika maabara za uchunguzi na tiba. Hilo likifanyika, Zanzibar inaweza hata kuvutia kwa wageni kuja Zanzibar kufuata huduma hizo na hivyo kukuza utalii wa tiba *(medical tourism)*. Unafuu wa gharama, hali ya hewa nzuri, usalama wa nchi yetu, vifaa vya kisasa na watoa huduma wenye uweledi ni nyenzo muhimu katika kufanikisha hilo.

SEKTA YA UTALII ...

Mhe. Spika: Mhe. Abdulla Ali Kombo samahani kidogo waheshimiwa wajumbe kwa mujibu wa kanuni ya 96 walioekewa muda ni mawaziri wanapowasilisha muda usiozidi saa 1:30 na wakati wa kufanya majumuisho muda usiozidi saa 1:00, lakini hatukuweka utaratibu kwa Wenyeviti wa Kamati na imezoeleka mara nyingi sana Hotuba za Wenyeviti wa Kamati haziwi *back* sana hotuba hii mpaka sasa hivi tumeshatumia karibu dakika 45 na ndiyo kwanza uko ukurasa wa 15 na kuna kurasa 36 kwa maana kwamba muda mwingi sana utachukuliwa na Mwenyekiti wa Kamati.

Mimi ningeshauri mheshimiwa sehemu ya hotuba iliyobaki iingiye kwenye *Hansard* ili tuweza kuwapa sasa Waheshimiwa Wajumbe uwezo wa kuchangia kwa hiyo naomba umalizie halafu uombe iende kwenye *Hansard* halafu baada ya hapo tutaenda kwenye michango kuwapa Waheshimiwa. Ahsante sana.

Mhe. Abdalla Ali Kombo (Kny. Mwenyekiti Kamati ya Bajeti -Baraza la Wawakilishi): Waheshimiwa wajumbe namshukuru sana Mhe. Spika kwa maelezo yake na kwa niaba ya Mwenyekiti niko tayari kuyakata baada ya kumalizi sehemu hii ndogo ya Utalii.

Mhe. Spika, naomba kukiri tena umuhimu wa Serikali kuunga mkono jitihada zinazochukuliwa na wananchi wenzetu katika kuanzisha utowaji wa Huduma za Afya zilizobora kwa kuwa hudma hizi huwagusa wananchi moja kwa moja tofauti na miongoni mwetu wenye uwezo wakutibiwa nje ya nchi, basi ni vyema kuweka utaratibu wa kuwapa unafuu kwa kodi wanaopoingiza vifaa vinavyotumika katika maabara ya uchunguzi na tiba.

Hilo likifanyika Zanzibar inaweza hata kuwa kivutio kwa wageni wanaokuja Zanzibar kufuata huduma hizo na hivyo kukuza utalii wa tiba yaani *(medical tourism)*. Unafuu wa gharama, hali ya hewa nzuri, usalama wa nchi yetu, vifaa vya kisasa na watoa huduma wenye uweledi ni nyenzo muhimu katika kufanikisha hilo.

Mhe. Spika, napenda kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bajeti ninayosoma.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Abdalla Ali Kombo waheshimiwa wajumbe sehemu ya hotuba iliyobaki naomba sasa iende kwenye *Hansard* ili ni sehemu rasmi ya kile ambacho Mheshimiwa amekiwasilisha.

Ahsante sana Mhe. Abdalla Ali Kombo

Mhe. Abdalla Ali Kombo (Kny. Mwenyekiti Kamati ya Bajeti -Baraza la Wawakilishi): Napenda kuwasilisha. *(Makofi)*

(Sehemu hii imeombwa iingie katika Hansard)

SEKTA YA UTALII

Mhe.Spika, sekta ya Utalii ina mchango mkubwa sana katika Uchumi wa Zanzibar, ambapo utalii tunautegemea sana katika kuingiza nchi yetu fedha za kigeni kupitia makusanyo ya tozo mbali mbali zinazotokana na sekta hiyo. Aidha, Sekta ya Utalii imekuwa na mchango mkubwa katika kuwapatia ajira vija wetu ikiwemo ajira za moja kwa moja "*direct employment*" katika mahoteli ya kitalii, pamoja na ajira nyengine zinazoambatana na huduma zinazohusiana na sekta ya hiyo, zikiwemo huduma za kuwasafirisha wageni, huduma za kuwatembeza wageni katika vivutio vya utalii, huduma za masoko ya bidhaa, huduma za mikahawa pamoja na michezo ya baharini.

Mhe.Spika, pamoja na umuhimu wa Sekta hii katika Uchumi wa nchi, bado fursa ya Utalii haijatumika vizuri, ambapo mapato yanayotokana na sekta hii bado ni madogo sana. Hivyo, Kamati yangu inaishauri Serikali kuongeza ufanisi katika sekta hii hususani katika suala zima la ukusanyaji wa mapato, kwa kuziba mianya yote ya uvujaji wa mapato.

Mhe.Spika, suala la kuimarisha mfumo wa kukusanya mapato yanayotokana na sekta ya Utalii limekuwa likizungumzwa mara kwa mara katika Baraza hili, hivyo imefika wakati sasa kwa Serikali kuja na mpango madhubuti wa kubadilisha mfumo wa kukusanya mapato katika sekta hii muhimu sana kwa uchumi wa nchi kwa kubuni mifumo ya kisasa ya kukusanya kodi, ambayo itapunguza mianya ya uvujaji wa mapato na ambayo pia haitoleta usumbufu kwa watalii pamoja na wawekezaji katika sekta hiyo.

Mhe.Spika, viele vile Kamati yangu inaishauri Serikali kuweka utaratibu wa kudhibiti uingiaji wa wageni kwa kufanya kazi kwa karibu na mashirika ya ndege na boti za kusafirishia abiria kwa kutumia "*manifesto*". Aidha, mashirikiano hayo yaihusishe pamoja na Idara ya Uhamiaji ambapo nakala ya orodha ya wageni wanaoingia nchini ipelekwe Mamalaka ya Mapato- ZRB ili kujua idadi halisi ya wageni wanaoingia ili kuepuka udanganyifu unaofanywa na baadhi ya wamiliki wa Hoteli za Kitalii. Sambamba na hilo, ili kupunguza usumbufu kwa walipa kodi na kuhamasisha ulipaji Kodi kwa hiari "*Tax Compliance*" ni vyema Serikali ikapunguza utitiri wa kodi kwa kuzikusanya kodi pamoja ili zilipwe sehemu moja *"Single Point"* kwa kutumia mifumo ya kisasa.

Mhe.Spika, taarifa ya Serikali ya Mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2016/2017 inaonyesha kuongezeka kwa Idadi ya watalii. Aidha, taarifa hiyo inaonyesha kuongezeka kwa masoko mapya ya watalii wanaokuja Zanzibar kutoka nchi za Urusi, Ukrain, China, India na Israil. Hii ni baada ya kuanzishwa safari za ndege za moja kwa moja kutokea nchi za Ukraine, Israil na Uturuki. Kimsingi Kamati inapongeza hatua hiyo ya kuongezeka kwa idadi ya watalii ambayo pia inatarajiwa itaongeza kiwango cha mapato yanayotokana na sekta Hiyo. Hata hivyo, kwakuwa biashara ya Utaliii ni biashara ambayo haitabiriki "*Very Volatile*" ni vyema Serikali ikangalia kwa umakini aina ya makampuni yanayoleta watalii Zanzibar kwa kuangali mazingira halisi ya dunia, hii ni kutokana na ukweli kwamba baadhi ya mataifa yamekuwa ni walengwa sana wa matukio ya kigaidi. Kamati inashauri hivyo ili kuepusha kutokea kwa athari ambayo inaweza kuathiri vibaya sekta hiyo ambayo tunaitegemea sana kwa uchumi wetu. Hivyo, Kamati yangu inashauri vyombo vya usalama na diplomasia viangalie athari zinazoweza kutokea "*negative side"* kutokana na kupokea watalii wa mataifa hayo.

Mhe.Spika, kwa kuwa Tanzania ilisaini makubalino ya "*East African Tourism Protocal*" na kwakuwa Nchi za Kenya, Uganda na Rwanda waliingia makubaliano ya "*Coallition of the Wiilling"* ambayo yana lengo la kuzifanya nchi hizo kuwa kituo kimoja cha Utalii "*Single Tourist Destination*" kwa kuweka VIZA ya pamoja kwa watalii wanaotembelea katika nchi hizo. Ni vyema kwa Wizara husika ikafikiria uwezekanao wa kuondosha VIZA kwa miezi ambayo wageni wanakuwa wamepunguwa (Aprili, Mei, Septemba, Octoba na Novemba) kwa wageni ambao ni "*Diplomatic*" na ambao wana "*Residence*" katika miji ya Nairobi, Kigali, na Kampala.

Hii, itasaida kuongeza Idadi ya Watalii watakao kuja Tanzania na kuweza kutoa ushindani na nchi za jirani za Afrika Mashariki. Aidha, Waziri wa Utalii afanye matangazo katika mji wa Nairobi, Kigali pamoja na miji mingine, kwa mashaurinao na Jumuiya husika za pande mbili za Muungano. Hili litasaidia kuongeza idadi ya watalii watakao tembelea Tanzania na hatimae kuongeza mapato ya Utalii.

UVUVI WA BAHARI KUU

Mhe.Spika, Licha ya ukweli kwamba Zanzibar na Tanzania kwa ujumla ina rasilimali kubwa ya bahari, Sekta ya Uvuvi wa Bahari Kuu bado haijatumika ipasavyo, ambapo Mapato ya Bahari Kuu yanaendelea kusuasua. Aidha, sehemu kubwa ya mapato hayo yanategemea zaidi meli za nje kupitia mauzo ya leseni. Sambamba na hilo kuna tatizo la kutokuwa na usimamizi mzuri pamoja na miundombinu hafifu katika kuzihudumia meli za Uvuvi. Pia imebainika kwamba, kuna baadhi ya meli za kigeni zinakuja kuvua kwa magendo kutokana na kutokuwepo ulinzi madhubuti "*Patrol*".

Mhe.Spika, Ili Zanzibar na Tanzania kwa ujumla, iweze kunufaika na uvuvi wa Bahari Kuu, lazima ibadilishe mwelekeo wa mfumo wa usimamizi wake. Utaratibu uliopo sasa hivi wa kutegemea leseni kwa meli za mataifa ya kigeni zinazokuja kuvua katika bahari yetu na kupelekea samaki kwenye nchi zao au nchi za jirani kama Seychelles, Kenya, Madagasca, Mauritius unaikosesha nchi faida kubwa. Ili tuweze kunufaika na sekta hiyo, hatunabudi kuwataka wenye meli hizo kushusha samaki Bandari za Zanzibar na Tanzania

Bara, hili litasaidia nchi kupata mapato mengi zaidi na pia wananchi wengi watanufaika na sekta hiyo.

Mhe. Spika,miongoni mwa faida zinazoweza kupatikana iwapo meli za uvuvi zitashusha samaki kwenye Bandari zetu ni pamoja na.

- Meli itatoa ajira kwa wale watakao hudumia ushushaji wa samaki.
- Itatoa ajira na pia malipo kwa wale watakaosafirisha samaki kwenda kwenye sehemu za kuhifadhia.
- Meli itatanunua mafuta, maji salama na vyakula na hivyo wakulima wetu na wafanyabiashara wetu wa Unguja na Pemba watapata soko la kuuza bidhaa zao.
- Meli italipia kukaa Bandarini kodi na ushuru mbali mbali.
- Maajenti (Mawakala) wa meli wa Zanzibar watapata kazi.
- Serikali itaweza kukagua meli husika na mazao yake na kupata malipo ya huduma.
- Mabaharia kwenye meli watashuka na kufanya utalii na hivyo kuleta fedha za kigeni.
- Mabaharia wakiwa mjini watanunua vitu mbali mbali na hivyo kuongeza ajira na kipato.
-
- Samaki watakaoshushwa watapelekwa kwenye masoko kwa ajili ya kuuzwa na kutumika kwenye viwada, hivyo kuongeza ajira na kipato kwa wananchi wetu.
- Wananchi watapata lishe bora ya samaki kwa bei ya unafuu.
- Hakutokuwa na haja tena ya kuingiza samaki kutoka nje.
- Kutokana na kuwepo samaki viwanda vitajengwa na kutoa ajira kwa vijana wetu, aidha Serikali itapata kodi kupitia viwanda hivyo.

Mhe.Spika, hata hivyo, ili haya yawezekane jambo la msingi ni kuweka miundo mbinu yetu wenyewe na kuwawezesha watanzania kuvua wenyewe na kuleta samaki kwenye bandari zetu badala ya kuwaachia makampuni ya nje kuvua na kusafirisha, ambapo tunapoteza mapato mengi katika sekta hiyo.

SEKTA YA ELIMU

Mhe.Spika, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kuifanyia mapitio Sera ya Elimu ya mwaka 2006, hususani suala zima la mfumo mpya wa elimu ambao pamoja na mambo mengine, umeweka utaratibu wa mwanafunzi

anaemaliza darasa la sita kuendelea moja kwa moja darasa la tisa, ambapo kiujumla atakuwa kapunguza miaka miwili ya masomo (madarasa mawili). Kimsingi mwanafunzi huyo anakuwa ni mdogo sana kiumri na kiumbile kuweza kuhimili vishindo vya darasa la tisa.

Mhe.Spika, tunafahamu nia nzuri ya Serikali yetu ya kutaka kuimarisha elimu kwa vijana wetu. Hata hivyo, wanafunzi wanaotakiwa kuendelea na darasa la tisa uwezo wao unakuwa ni mdogo sana kutoka na kutokuwepo misingi mizuri katika madarasa ya awali. Aidha, wanafunzi hao wanapomaliza darasa la kumi na mbili wanakuwa bado ni wadogo sana kuanza maisha mapya ya uraiani.

Mhe.Spika, inawezekana sera hiyo ikawa nzuri kwa nchi za wenzetu lakini ikawa sio nzuri kwa nchi yetu. Hivyo, tunaishauri Serikali kuifanyia mapitio sera hiyo ya elimu pamoja na kufanya tathmini kuhusu ufanisi wake, kwa kuzingatia mazingira halisi ya nchi yetu.

Mhe.Spika, Serikali ina mpango wa Kuanzisha mfuko wa Madawati kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kamati yetu inapongeza sana Serikali kwa maamuzi hayo ambapo mfuko huo utasadia sana kuimarisha mazingira ya elimu na kupunguza taizo la wanafunzi wetu kukaa chini. Kamati yangu inapendekeza juhudi hizo ziende sambamba na uongezaji wa madarasa, hii ni kutokana na ukweli kwamba kuongeza madawati kutasababisha upungufu wa nafasi katika madarasa na kupelekea haja ya kupatikana madarasa ya ziada.

VYUO VYA ELIMU YA MAFUNZO YA AMALI

Mhe. Spika,Vituo vya Mafunzo ya Amali "*Vocationa Training Centre*" vina umuhimu mkubwa katika kuandaa vijana wetu kuweza kujiajiri. Hata hivyo, bado kuna muitikio mdogo kwa wananchi katika kuvitumia vituo hivyo. Kutokana na kasoro hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuwahamasisha wananchi kuvitumia vituo hivyo ili wapate ujunzi na kuweza kujiajiri wenyewe na hatimae kuisaida Serikali katika jitihada za kupunguza tatizo la ajira, hasa ikizingatiwa kuwa Serikali haina uwezo wa kuajiri wananchi wake wote.

Mhe. Spika,Sheria ya Mamlaka ya Vituo vya Amali inaishauri Mamlaka husika kusimamia mafunzo yanayotolewa na vituo hivyo na vile vya binafsi ili ubora wa taaluma unaopatikana ukidhi haja. Kutekeleza dhamira hiyo, Serikali imeanzisha mfuko maalum (Skill Development Levy – SDL) ili Mamlaka iweze kutekeleza jukumu hilo muhimu. Hadi miezi ya karibuni, imebainika kuwa upatikanaji wa fedha za SDL kutoka Serikalini umekuwa wa kusuasua japokuwa makusanyo yanawasilishwa kwa wakati. Kamati yangu inaishauri Serikali kutekeleza maelekezo ya Sheria kwa kuanzisha haraka Mfuko Maalum wa Kuendeleza Vituo vya Amali utaosimamiwa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ili kuongeza ufanisi.

Aidha, Mamlaka husika iandae mikakati madhubuti ya kuviimarisha vituo hivyo, ambapo walimu wanaofundisha katika vituo hivyo wawe na sifa za kutosheleza na vituo visiwe vinatelekezwa kama iilivyobainika katika Kituo cha Elimu Amali cha Mkokotoni

kupatiwa vifaa na Serikali ya Iran lakini wengi kati ya walimu wa kituo hicho wameshindwa kuvitumia vifaa hivyo. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha mazingira ya vituo hivyo ili malengo ya kuanzisha vituo hivyo yaweze kufikiwa.

Mhe. Spika,Kamati yangu inatumia fursa hii kuipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuanzisha utaratibu wa kuwapa mikopo isiyo na riba vijana wetu wanaomaliza mafunzo katika Vituo hivyo ili waanze maisha. Ni imani yetu kuwa mikopo hii itawafikia na wale vijana wetu majimboni ambao hawakumaliza katika Vituo vya Serikali lakini wameweza kujikusanya kuanzisha shughuli za ujasiraamali na utaalamu wa ufundi wanao.

UTEKELEZAJI WA MIRADI MIKUBWA

Mhe. Spika, utekelezaji wa miradi mikubwa ikiwemo ujenzi wa Jengo Jipya la Uwanja wa Ndege- Terminal II, na Mradi wa E.Government imekuwa ya kusuasua sana, mbali ya tatizo la upatikananji wa fedha kutoka kwa washirika wa Maendeleo, Kamati yangu inapata hofu kwamba kuna matatizo ya ndani ya uendeshaji kwa baadhi ya taasisi zinazosimamia miradi hiyo. Kwakuwa miradi hiyo hutumia fedha nyingi ambazo mara nyingi zinakuwa ni mikopo. Hivyo, kuchelewa kukamilika kwa miradi hiyo huambatana na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji pamoja na kuengezeka kwa riba ya mikopo hiyo, kwa mfano Mradi wa Jengo Jipya la Uwanja wa Ndege kutoka na kufanyiwa '*design*' mpya imepelekea kuchelewa kukamilka ujenzi wake. Aidha, gharama zake zimeongezeka ambapo gharama za awali zilikuwa ni Dola milioni 78.4 zimeongezeka hadi kufikia Dola milioni 128. Kamati yangu inaishauri Serikali kuwa makini wakati inapoanzisha miradi, kwa kufanya upembuzi yakinifu"*fesaibility study*" wa uhakika lakini pia kuwa na usimamzii mzuri pamoja na kuwachukulia hatua watakaobainika kufanya uzembe au kukwamisha ufanisi katka utekelezaji wa Miradi ya Serikali.

SEKTA YA MFUMO WA FEDHA WA KIISLAMU

Mhe. Spika,nianze kuzungumzia hili kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa neema kubwa Wazanzibari ya kuthaminiwa na kuaminiwa sana na wenzetu katika huduma mbalimbali tunazozitoa zikiwemo zile za kibenki zinazofuata maadili ya Sharia. Sote tunashuhudia vipi Benki ya Watu wa Zanzibar inapata mwitiko popote inapofungua matawi yake, ndani na nje ya Zanzibar.

Pamoja na kasoro zilizopo katika ufinyu wa kumbi za kutolea huduma hususan mwisho wa mwezi na ATM zake kukosa ufanisi unaotegemewa, uwepo wa Divisheni ya Kiislamu ya Benki ya Watu wa Zanzibar umefaidisha wananchi wote, Waislamu na wasio Waislamu kwani huduma zake hazibaguwi.

Mhe. Spika,mwanzoni mwa mwaka huu Zanzibar ilipata heshima kubwa kimataifa pale Mzanzibari mmoja (Dkt. Mohammed Hafidh Khalfan) na taasisi mbili za Zanzibar (Shirika la Bima Zanzibar na Chuo Kikuu cha Zanzibar – Tunguu) walipopewa tuzo maalum kuhusiana na Mfumo wa Kifedha wa Kiislamu. Ingawa suala hili lilipita bila hata kupata heshima inayostahiki ya kutambuliwa ndani ya nchi, kimataifa liliinyanyua na kuitangaza Zanzibar kwa kiasi kikubwa. Hivyo, umefika wakati Wazanzibari kujitambua na kuthamini zile neema ambazo Mola Ametujaalia.

Mhe. Spika, wakati sisi tukisuasua na kupuuza fursa zilizopo katika eneo hili, tayari Serikali za Kenya, Uganda na Zambia zimepitisha sheria na kuanza taratibu za kufaidika na huduma za fedha za Kiislamu ikiwemo mifumo ya benki, bima (takaful) na hati fungate za Kiislam (Sukuk). Wengi wa watendaji katika taasisi hizo tumewasomesha wenyewe hapo Tunguu. Wito wa Kamati yangu kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kulifanyia kazi suala la Bima ya Kiislamu na miamala mingine ili wananchi wetu wafaidike na fursa zinazopatikana huko. Ikiwa aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza David Cameron ameliona hilo na kutangaza rasmi kuifanya London kuwa Kitovu cha Huduma za Kifedha Kiisalamu, Watanzania tuna lipi linalotutia khofu hadi kuzikosa fursa za kupata mitaji mikubwa kuendeleza nchi yetu?

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

Mhe. Spika, naomba kwa idhini ya Baraza lako tukufu, sasa nitowe maoni ya Kamati yangu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

MWELEKEO WA BAJETI

Mhe. Spika,awali kabisa napenda kuipongeza Serikali kwa ujumla, kwa mara ya kwanza kufikisha bajeti yenye ukubwa wa shilingi za kitanzani trilioni 1.08 ambayo ni sawa naongezeko la 23% ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017. Hii inaonesha jinsi gani Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar inalengo na azma kubwa ya kuhahakisha inaleta mabadiiko katika hali ya maendeleo kwa wananchi wa visiwa vya Zanzibar, ukizingatia kwamba takriban nusu ya bajeti hii (TSH 496.6) sawa na asilimia 46% ya bajeti yote, zimetengwa kwa ajili ya shuguhuli za maenedeleo ambayo moja kwa moja yanamgusa mwananchi wa kawaida. Hivyo nikusema hii ni bajeti ya wananchi inayoakisi matarajio ya mwananchi wa kawaida.

Mhe Spika, hofu ya Kamati yangu ni juu ya uhalisia wa bajeti hii hususan kwa upande wa shughuli za maendeleo, ambapo uzowefu unaonesha kumekuwa na ugumu wa kupatikana kwa fedha za maendeleo ambazo huathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa miradi mbali mbali inayopangwa kutekelezwa.

Mhe. Spika,naomba Baraza lako lifahamu kuwa, bajeti ni kupanga, na kupanga ni kuchagua, lakini kuchagua kuwa na bajeti kubwa haimaanishi kuwa tutapiga hatua kimaenendeleo, ikiwa bajeti tunayoipitisha haina uhalisia kutokana na kukosa uhakika wa upatikanaji wa fedha. Ni imani ya Kamati yangu kuwa ni kheri kuwa na bajeti ndogo lakini yenye kutekelezeka na uhalisia wa upatikanaji wa fedha, kuliko kuwa na bajeti kubwa ambayo inaishia kulipia mishahara, na matumizi mengine ya uendeshaji wa ofisi yaani OC, bila kuwafikia na kuacha athari chanya kwa wananchi.

UIMARISHAJI WA UKUSANYAJI WA MAPATO

Mhe. Spika,ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ni jambo la msingi katika bajeti yoyote ile, hasa kwa bajeti ya nchi changa inayotegemea kukusanya na kutumia kwa mujibu wakinachopatikana *"cash budget"* ambao Zanzibar ndio mfumo tunaoutumia, hii ni sawa na kusema kuwa pasipo na ukusanywaji wa pamato, hakuna utekelezaji wa mipango

yoyote ya Serikali. Ni ukweli usiopingika kuwa bajeti zetu zina changamoto kubwa ya ukusanyaji wa mapato ambayo ndio kiashiria kikubwa kinachotumika kuchagua mipango ipi itekelezwe kwa mwaka upi wa fedha ili kuleta tija kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

Mhe. Spika,kutokana na maenedeleo ya sayansi na teknolojia, hatuwezi kuzungumzia kuimarisha mapato ya nchi bila ya kugusia suala la utumiaji wa vifaa vya EFD yaani "*Electronic Fiscal Devices*", sambamba na kuachana na mfumo wa ulipaji kodi, na ada mbali mbali kwa mfumo wa "*cash*" ambao kwa ujumla unatoa mwanya wa kufanya udanganyifu kwenye malipo, uchelewashaji wa malipo husika na kudumaza ubora wahuduma zinazotolewa na taasisi zetu za Serikali, kutokana na kuwa tunaishi nyuma ya muda kiteknolojia, tunaendelea kutumia mifumo ya kizamani ambayo kwa kiasi kikubwa inakosesha Serikali mapato.

Mhe. Spika**,**kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali imeeleza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa katika suala la ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kiwango cha asilimia 108 ya ukomo, na kufanikiwa kukusanya jumla ya shilingi za kitanzania bilioni 362,242.48 kati ya bilioni 482,400 zilizokusudiwa kukusanywa kwa mwaka husika[1]. Aidha, mafanikio hayo ya mefikiwa bila ya kutumika kwa vifaa vya EFD katika zoezi la ukusanyaji huo. Ni imani ya Kamati yangu kuwa, licha ya mafinikio hayo bado Serikali inapoteza mapato mengi sana yanayoishia kwenye mifuko ya baadhi ya watendaji wa Serikali wasiokuwa waaminifu, kutokana na kushindwa kwa Serikali kutimiza azma ya kuanza kutumia vifaa vya EFD kama ilivyoelezwa na kuahidiwa mbele ya Baraza hili katika bajeti ya mwaka 2016/2017, ambapo Serikali iliahidi kununua na kuanza kutumia jumla ya mashine za EFD 1000 ili kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Mhe. Spika, Ili kuweza kukuza ufanisi katika vyanzo muhimu vya Mapato, kama vile Bandarini na Uwanja wa Ndege, vyanzo vya mapato viwekewe mazingira mazuri, kwa kuimarisha miundo mbinu na kuweka mifumo rasmini ya kisasa ya ukusanyaji wa mapato.

Kamati yangu inashauri Serikali, kwa majaribio kuiga mfano wa mafanikio yaliyofikiwa katika ukusanyaji wa ada za Viza unaofanywa na wakala (Benki ya CRDB) kwenye Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume, ambapo kupitia wakala huyo mapato yameongezeka kutoka wastani wa Dola laki tatu (3) hadi tano (5) kwa mwaka (Kabla ya CRDB) na kufikia Dola laki tano (5) hadi milioni moja kwa mwezi (Baada ya kupewa uwakala CRDB)

VIPAUMBELE VYA KITAIFA

Mhe. Spika, bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 inakadiriwa kufikia trilioni 1.08, ambapo jumla ya vipaumbele kumi na moja (11) vimependekezwa ikiwa kama ni dira ya muelekeo wa utekelezaji wa bajeti hii ya Serikali. Kwa ujumla vipaumbele hivi vinagusia sekta zote muhimu ikiwa ni pamoja na sekta ya maji, elimu, afya, miundo mbinu ya barabara, viwanja vya ndege, nishati, uekezaji wa viwanda, kilimo mafuta na gesi asilia, utafiti, na utawala bora. Idadi hii ya vipaumbele kumi na

moaja (11) ni zaidi ya vipaumbele vitano (5), vilivyoainishwa na Serikali kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 ambayo kwa ujumla haikutekelezeka kwa kiwango kilichokusudiwa.

Aidha, licha ya kupata maelezo kuwa kuongezeka kwa idadi ya vipaumbele hivi, kumezingatia kuvifanya vipaumbele husika kuwa ni vyenye kuimarisha zaidi katika maeneo maalum, Kamati yangu bado inaona ipo haja na inashauri Serikali kuvipitia upya vipaumbele hivyo kwa lengo la kuvifanya kuwa mahsusi zaidi. Mapitio hayo yatasaidia sio tu kuwa na mipango yenye kutekelezeka zaidi, lakini pia yenye kuzingitia uwezo wa taasisi, mwenendo wa uchumi na matarajio yanayoakisi uwezo wa utekelezaji wa bajeti kwa Serikali yetu.

MUELEKEO WA MAPATO

Mhe. Spika, Mwelekeo wa Mapato kwa mwaka wa fedha 2017/2018, unaonekana kukuwa kama ilivyoelezwa katika Waraka wa Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2016/2017 pamoja na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kutoka shilingi za kitanzania bilioni 482.4 kwa mwaka 2016/2017, hadi kufikia shilingi za kitanzania billion 672 ikwa mapato ya ndani. Hii ni hatua kubwa mno ya makadirio ya mapato ya ndani ambayo yana mchango wa moja kwa moja katika kuifanya bajeti ya Serikali kuwa ni yenye kutekelezeka.

Mhe. Spika, tunapozungumzia kuhusu ukusanyaji wa mapato kwa upande wa Zanzibar, nil lazima kuizungumzia Bodi ya Ukusanyaji wa Mapato Zanzibar (ZRB), ambayo kimsingi ndio mas'ul wa ukusanyaji wa mapato kwa Zanzibar. Kwa miaka kadhaa, ZRB imekua ikivuka malengo inayojiwekea katika ukusanyaji wa mapato, kwa mfano mwaka 2016/2017, ZRB na TRA wamevuka lengo kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kiwango cha asilimia 108, mafanikio haya ya mamlaka ya ukusanyaji wa mapato ya Zanzibar, yametiliwa mkazo pia katika nukuu ya hutuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt Ali Mohammed Shein, ambae alieleza kuwa, mnamo mwaka 2010 mwanzoni mwa awamu hii ya sita ZRB walikua wanakusanya wastani wa shilingi za kitanzania bilioni 13 kwa mwezi, ikiwa sasa kunakusanywa jumla ya wastani wa bilioni 50 kwa mwezi. Makisio haya ni sawa na wastani wa bilioni 600 kwa mwaka. Aidha, ilisisitizwa zaidi kuwa ni matarajio ya Serikali kuwa, mnamo mwaka 2020, ZRB watakusanya wastani wa bilioni 800 kwa mwaka.

Mhe. Spika, Licha ya mafanikio haya makubwa, Kamati yangu bado inaamini mamlaka ya ZRB, ina uwezo wa kukusanya mapato zaidi, ikiwa nidhamu ya fedha itakuwa ni msingi wa utendaji kazi wa bodi hiyo. Aidha, iwapo watumishi wasiokuwa na maadili ndani ya bodi hiyo watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria, sambamba na uwekaji wa malengo (*targets*) ya kukusanya yenye uhalisia, badala ya kuweka malengo yaliyo chini ya uwezo halisi wa Bodi hiyo. Umefika wakati sasa ZRB na TRA zipangiwe malengo kitaalamu badala ya utaratibu wa sasa wa kujipangia wenyewe malengo.

Mhe. Spika, Katika bajeti hii ya mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imekusudia kutoongeza kodi mpya badala yake msisitizo zaidi umelenga kwenye kuimarisha

ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vile vile vilivyotumika kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kamati yangu inaunga mkono azma hiyo ya Serikali, kwani inaonesha ni kwa kiasi gani Serikali haikusudii kumuongezea mzigo wa gharama za maisha mwananchi wa kawaida kupitia kodi zinazotozwa kwenye bidhaa na huduma mbali mbali. Licha ya azma hiyo ya Serikali kutoengeza kodi kwa mwaka huu wa fedha, Kamati yangu imebaini kuwepo kwa vyanzo halali vya mapato ambavyo havikusanywi kodi na kupelekea Serikali kukosa sehemu ya mapato halali ya mapato yake ya ndani.

Mhe. Spika, kwa idhini yako, naomba kuorodhesha baadhi ya maeneo ambayo kwa sababu ya kukosa udhibiti au mfumo mzuri, Serikali inakosa mapato. Maeneo hayo ni pamoja na :-

a. Kodi/tozo za Leseni za Benki zinazofanya biashara ndani ya Zanzibar; kwa sasa benki zinazotoa huduma zanzibar zinatoa huduma bila ya kuwa na leseni, kinyume na utaratibu unaotumika Tanzania Bara, ambapo mbali na kibali cha BOT Benki hizo zinatakiwa kuwa na leseni za biashara.

b. Kodi/tozo ya kuhaulisha umiliki wa vyombo vya moto ambao mpaka sasa mauziano yanafanyika kienyeji bila ya kuwepo mfumo rasmi wa kuhaulisha, pia ni hatari kiusalama, ambapo vyombo hivyo vinaweza kutumika katika matukio ya uhalifu.

c. Kodi/tozo za mauziano na uhaulishaji wa umiliki wa nyumba za Serikali zilizo chini ya watu binafsi, ikiwa ni pamoja na nyumba za michenzani na nyenginezo mfano wa hizo ambazo watu wanauziana bila ya kuishirikisha Serikali.

d. Kodi/tozo za viingilio vya magari ndani ya eneo la hifadhi ya mji mkongwe, hii ni pamoja na tozo inayokusudiwa kutozwa kwa gari zinazopita kwenda mkunazini-Sunni madrasa, kwa lengo la kupunguza msongamano katika eneo hilo, tozo ambayo haikusanywi kwa sasa licha ya kuwa kianzio rasmini cha mapato kinachotambulika.

e. Kodi/tozo za maegesho ya magari ndani ya mji wa Zanzibar, makusanyo ambayo Kamati yangu inayatilia mashaka juu ya usimamizi wake, na uhalali wa makusanyo hayo nyakati za usiku na mwisho wa wiki.

f. Kodi/tozo za lesni tofauti, Leseni za biashara ndogo na za kati zisizotolewa kabisa au kutolewa na mamlaka tofauti kwa viwango na gharama tofauti

g. Kodi/tizo za Mabango ya matangazo ya biashara kandokando ya barabara za ndani ya mji wa Zanzibar

Mhe. Spika, **s**ambamba na vianzio hivyo Kamati yangu inashauri Serekali ifanye mapito ya mapato ya vikosi vya SMZ yanayopatikana kutokana na huduma zinazotolewa pamoja na shughuli za uzalishaji ambazo zinafanywa na vikosi hivyo. Kamati imepata hofu juu ya uwazi na uhalisia wa fedha zinazopatikana na fedha ambazo zinaingia katika mfuko mkuu wa Serikali kupitia mapato yanayotokana na hudma na biashara zinazotolewa na vikosi hivyo.

Mhe. Spika, eneo jengine muhimu la mapato ni huduma za makampuni ya simu**,** mbali na Kampuni ya Zantel kuna makampuni mengi ya simu yanayotowa huduma Zanzibar, Kamati yangu ilipata hofu namna Serikali inavyonufaika kimapato yanayokusanywa kutokanana huduma zinazotolewa na makampuni hayo. Hata hivyo, Kamati yangu kwa dhati kabisa inaipongeza Serikali kwa adhma yake ya kuja na mswada wa ushuru wa bidhaa ambao pamoja na mambo mengine utasaidia kuhakikisha inapata nguvu ya kukusanya baadhi ya kodi au mapato kutoka katika makampuni hayo pamoja na mapato ya huduma zinazotolewa na makampuni hayo ikiwemo huduma ya kutoa na kutuma pesa, ambapo kabla ya Sheria hii Serikali haikuwa na Nguvu za kisheria za kukusanya baadhi ya kodi hizo, hivyo kupelekea kukosa fedha nyingi kutokana na kukosa uhalali wa kisheria wa kukusanya mapato hayo**.**

Mhe. Spika, wakati Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania likipitisha Mswada wa Fedha wa mwaka 2016/2017 pamoja na mambo mengine mswada huo uliifanyia marekebisho Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), sheria No 5 ya mwaka , 2014 kwa kulibadilisha utaratibu wa malipo ya kodi ya VAT, ambapo kufuatia mabadiliko ya sheria hiyo; bidhaa zitakazosafirishwa kutoka T.Bara kwenda Zanzibar hazitolipiwa kodi ya VAT Tanzania Bara yaani zitakuwa " *zero rate at the origin*" badala yake zitalipiwa kodi Zanzibar "*at destination point*", vile vile bidhaa biashara zitakayosafirishwa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara hazitolipiwa kodi Zanzibar badala yake zitalipiwa kodi Tanzania Baraza. Aidha, kwa mujibu wa sheria hiyo utaratibu huu unawahusu wafanyabiashara ambao wamesajiliwa kodi ya VAT tu (VAT register), na hauwahusu wale ambao hawajasajiliwa VAT. Hivyo, iwapo mfanyabishara ambae hajasajaliwa VAT atasafirisha bidha kutoka Tanzania Bara kupeleka Zanzibar, atalipia kodi ya VAT mara mbili, Tanzania Bara na Zanzibar. Hali hii imeathiri sana wafanyabiashara wa Zanzibar hususani ambao hawajasajiliwa kodi ya VAT.

Mhe. Spika, Kutokana na hali hiyo, Kamati yangu inashauri kuwepo na mashirikiano na mawasiliano ya karibu baina ya Mawaziri wa Fedha wa pande mbili za Muungano, hususani wakati wanaposhughulikia masuala ya fedha na mapato ambayo yanahusu Muungano au maamuzi yake yana athari kwa pande mbili za Muungano.

NIDHAMU KATIKA MATUMIZI YA FEDHA ZA UMMA

Mhe. Spika, Zanzibar ni miongoni mwa nchi zinazokusudia kufika uchumi wa kati mnamo mwaka 2020, lengo hili litafikiwa kwa kuangalia viashiria mbali mbali vya kiuchumi ikiwa ni pamoja na pato la mtu mmoja mmoja, mfumuko wa bei, na viashiria vyengine vya kiuchumi vilivyowekewa viwango vya kimataifa. Hata hivyo, Mipango na makadirio tunayojiwekea pamoja na matarajio ya wananchi tunaowaongoza hayatafikiwa bila ya kuwa na nidhamu katika matumizi ya fedha za umma.

Mhe. Spika, kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu (*CAG*) iliyotokana na agizo la Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi juu ya matumizi ya fedha za mishahara katika wizara na taasisi za Serikali kumebainika upotevu mkubwa wa fedha. Kwa mujibu wa taarifa ya Katibu Mkuu Kiongozi wizara zinazohusika na upotevu huo wa fedha ni pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya

Amali, Wizara ya Kilimo Mifugo na Mali Asili, na Wizara ya Afya. Katika ukaguzi huo mambo mbali mbali yamebainika ikiwemo tofauti ya fedha zilizongizwa kwa ajili ya mishahara na fedha zilizotumika, kubainika baadhi ya watumishi waliochukua likizo bila ya malipo lakini wanaendelea kulipwa, kuwepo kwa watumishi ambao wamestaafu au kuacha kazi lakini bado wanaendelea kulipwa na baadhi ya wafanyakazi kutojitokeza kwa ajili ya zoezi la kuhakikiwa.

Mhe. Spika, mambo mengine yaliyobainika ni kubainika kwa watumishi ambao wamefikia umri wa kustaafu lakini bado wanaendelea na utumishi wao, kuwepo kwa watumishi ambao hawahudhurii kazini kwa muda mrefu lakini bado wanapokea mishahara pamoja na watumishi ambao hawawezi kufanya kazi kutokana na maradhi ya muda mrefu lakini bado hawajastafishwa kwa mujibu wa sheria, jambo jengine lililobainika ni wafanyakazi waliokwenda masomoni muda mrefu na hawajarudi makazini lakini bado wanalipwa mishahara na Serikali.

Mhe. Spika, ripoti hii ni ushahidi tosha kuwa, hakuma nidhamu ya matumizi ya fedha za umma, hasa ikizingatiwa kwamba ripoti hii imelenga eneo moja tu la mishahara ya watumishi wa umma, bila kugusia maeneno yenye mianya mikubwa ya upotevu wa fedha za Serikali kama maeneo ya ununuzi na ugavi, sambamba na eneo la miradi mikubwa ya maendeleo. Ni imani ya Kamati yangu kwamba, uchunguzi kama huu hautaishia kwenye mishahara ya watumishi wa umma pekee, bali utakua endelevu katika maeneo yote ya matumizi ya fedha za umma. Aidha, katika kuhakikisha Serikali inarudisha nidhamu katika matumizi ya fedha za umma, ni lazima hatua kali zichukuliwe kwa mujibu wa sheria, kwa wote wanaohusika na upotevu wa fedha za umma ili iwe mfano kwa wengine. Sambamba na hilo, ili kuongeza ufanisi katika masuala ya ukaguzi, Kamati yangu pia inaishauri Serikali kuiongezea nguvu Afisi ya Mdhibiti na mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa kuiwezesha kuajiri wakaguzi wa mahesabu ambao wana sifa, kwa mujibu wa mahitaji ya Afisi hiyo.

UGATUZI WA MADARAKA:

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018 Serikali inatarajia kutekeleza dhana ya Ugatuzi wa Madaraka ambayo ni upelekaji wa madaraka kwa wananchi, kutoka Serikali kuu kwenda Serikali za mitaa kwa lengo la kusogeza karibu zaidi huduma muhimu kwa wananchi na kuimarisha uwajibikaji wake. Kwa ujumla, azma na lengo la mpango huu ni nzuri kama inavyojieleza.

Mhe. Spika**,**mpango kama huu unatekelezwa pia na nchi za jirani kama Kenya, ambao pia wamekumbana na changamoto katika utekelezaji wake. Hivyo, wasiwasi wa Kamati yangu upo juu ya uhalisia na ulazima wa mpango huu kwa Zanzibar licha ya kuwa Serikali imeazimia kuanza rasmin kuutekeleza ndani ya mwaka huu wa fedha. Ni ukweli usiofichika, nchi kama ya Kenya, ni nchi yenye idadi kubwa ya watu inayokwenda sambamba na changamoto nyingi za kijamii na za kiutendaji, tofauti na Zanzibar ambayo ina idadi ndogo sana ya watu na pia eneo lake kijografia sio kubwa kama nchi za jirani.

Mhe. Spika,Kamati yangu inaamini Serikali ina wataalum na washauri wazuri na kwa kuwa tayari mpango umekwisha azimiwa kutekelezwa ndani ya mwaka huu wa fedha, ni

vyema basi, suala la kuwawezesha kielimu na kuwajengea uwezo likapewa kipaumbele kwa watendaji wa Serikali za mitaa watakaohusika na Mpango huu, hususani katika maeneo ya Elimu ya Maandalizi na Msingi, Afya ya Msingi na Huduma za (Ugani) kutoka wizara inayosimamia Kilimo na maeneo mengine ambayo ugatuzi utafanyika. Kwa kuwa mpango huu utahusisha wananchi wa ngazi ya chini, ni vyema basi Sekta Binafsi na Asasi ya Kiraiya zikashirikishwa mapema ili ufanisi upatikane ipasavyo.

ONGEZEKO LA MISHAHARA KWA WATUMISHI WA SERIKALI

Mhe. Spika, Kwa niaba ya Kamati yangu, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, kutimiza ahadi yake aliyoitoa katika kampeni za uchaguzi mkuu wa uraisi wa mwaka 2015, juu ya ongezeko la mishahara kwa watumishi wa Serkali wanaopokea kima cha chini cha mishahara kwa asilimia mia moja. Hii inaonesha ni kiasi gani kiongozi wetu wa nchi, ana wajali watumishi wanaotumikia Serkali yake, hususani wa kipato cha chini, kwani tayari watumishi wa umma wameanza kufaidika na utekelezaji wa ahadi hiyo mwanzoni mwa mwezi wa Aprili kama ilivyokuwa imeahidiwa. Hii ni mara ya nne sasa kwa Mhe. Rais kuongeza kiwango cha mishahara kwa watumishi wa umma tangu aingie madarakani mnamo mwaka 2010.

Mhe. Spika, pamoja na umuhimu wa ongezeko hili la mishahara kwa watumishi wa umma katika kuwahamasisha watumishi wa umma kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi, lakini pia kuwapunguzia ukali wa maisha, Kamati yangu inapenda kuikumbusha Serikali kuzingatia athari hasi "*negative effect*" za kiuchumi zinazoweza kutokea kutokana na ongezeko hilo. Kwa kawaida, ongezeko la mishara hupelekea kuongezeka kwa mzunguuko wa fedha katika Uchumi "*Money Circulation"* ambao pia hupelekea kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa yasiyokwenda sambamba na kasi ya uzalishaji na hatimae kupelekea kuongezeka kwa kasi ya bei za bidhaa na huduma yaani "*Inflaton".*

Mhe. Spika, Kwa ujumla ongezeko la mishahara hii halitakua na maana sana kiuchumi ikiwa leo mishahara imepanda, lakini kesho bei za bidhaa na huduma zinazotumiwa na watumishi wa umma na wananchi kwa ujumla zikapanda. Kamati yangu inatoa indhari hii ikiwa na imani yetu kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ina wataalamu wa uchumi imara na wenye uzoefu wanaoweza kuandaa mipango mizuri zaidi ya kuepusha athari hizo zisitokee kabisa au kukabiliana nazo pindi zitakapotokea.

Mhe. Spika, Kamati yangu inaishauri Serikali kuandaa Sera ya maalum ya Kipato cha Nchi (Income Policy) ili ndio iwe mwongozo wa mapato ya mwananchi badala ya kumuweka rehani kiongozi wa nchi kila siku ya Mei Dei kwa wananchi kutegemea ajifunge kwao kwa kutamka ongezeko la mshahara. Kwa lugha ya moja kwa moja, tuache kuifanya mishahara kuwa nyenzo ya kisiasa kwani ni hatari. Ili muengezeko wa mshahara uwe na faida iliyokusudiwa basi uwe kimya kimya wakati wake ukifika. Hilo likifanyika litaipunguzia pia Serikali jukumu kubwa la malipo kwa wakati mmoja.

Mhe. Spika, unathamini dhamira njema ya Serikali katika kuongeza mishahara ya wafanyakazi wake na Kamati yangu haipingi hilo. Tukumbuke tu kuwa wanaopokea mshahara wa Serikali ni wachache miongoni mwa wananchi wetu, hawafiki hata asilimia

kumi ya wakazi wa Zanzibar. Kamati yangu inaiagiza Serikali ifanye tathmini yakinifu kujua kwa njia gani muongezeko wa Pato la Taifa utafaidisha raiya wake ikiwemo kwa kuwapunguzia kodi mahitaji yao ya muhimu kama vile umeme, mafuta na vyakula. Hii ni kwa sababu mishahara huongezewa wachache lakini mfumko wa bei unawakuta wanaopokea mishahara na wasiopokea.

MISAMAHA YA KODI KIPINDI CHA RAMADHANI

Mhe. Spika, kamati yangu inaipongeza Serikali kwa utaratibu iliojiwekea wa kutoa misamaha ya bidhaa za vyakula vinavyotumika sana kipindi cha Ramadhani, kimsingi nia na lengo la Serikali ni zuri sana ambalo linakusudia kuwapunguzia ukali wa maisha wananchi hususani katika kipindi hicho muhimu**.** Hata hivyo, mara nyingi lengo na nia ya kutolewa misamaha hiyo haifikiwi walengwa. Imekuwa ni kawaida, na inaeleweka wazi hata na taasisi zinazotoa misamaha hiyo ya kodi kuwa, wanaofaidika na misamaha hiyo ya kodi ni wafanyabiashara wenyewe, kwani ndani ya mwezi wa ramadhani, vyakula hupanda bei mara dufu licha ya misamaha ya kodi inayotolewa ambapo pia Serikali hukosa fedha nyingi kutokana na misamaha hiyo, fedha ambazo zingeweza kutumika katika shughuli nyengine za maendeleo. Kamati yangu inapenda kutoa wito kwa mamlaka husika, kuandaa utaratibu wa kuwadhibiti wafanyabiashara ambao wanapatiwa misamaha na kutoa bei elekezi kwa bidhaa zinazopatiwa misamaha baada ya kufanya uchanganuzi wa gharama, ili kuhakiksha misamaha hiyo pia inawanufaisha wananchi wa kawaida kama ilivyo kusudiwa.

MAZINGATIO YA MAAGIZO YA SERIKALI

Mhe. Spika,katika bajeti hii ya mwaka 2017/2018, jumla ya maagizo kumi na nne(14) yametolewa na Serkali kwa azma ya kuwa yatekelezwe na wizara au taasisi husika. Aidha, jumla ya Tsh. Bilioni 56.2 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa maagizo hayo. Uanzishaji wa bima ya afya ni moja wapo ya maagizo hayo ambapo jumla ya shilingi bilioni 2 zimetengwa kwa azma ya utekelezaji wake. Kamati yangu inapongeza azma hiyo, na pia inapendekeza suala hilo lipewe uzito unaostahiki katika kulitekeleza.

Mhe. Spika, ni ukweli usiofichika kuwa, kwenye ulimwengu tunaoishi kwa sasa suala la bima ya Afya kwa watumishi wa umma sio tena suala lenye mbadala bali ni suala la lazima, kwa kuwa sasa ulimwengu unaitazama fursa hiyo kama haki ya lazima kupatiwa kwa mfanyakazi yeyote wa umma, ukizingatia mazingira hatarishi yaliyozunguka maeneo ya kufanyia kazi kwa taasisi za Serikali. Bima ya Afya ni sehemu ya motisha ambazo hupelekea mtumishi wa umma ajihisi kuwa ni sehemu ya wizara au taasisi anayofanyia kazi. Hivyo kuna kila sababu kwa Serikali kuharakisha jambo hilo badala ya kusubiri kummtupia mfanyakazi malalamiko ya utendaji mbovu wa kazi ambao kwa mtazamo wa Kamati yangu, sio tu unachangiwa na mazingira mabaya ya ufanyaji kazi, lakini pia kukosa haki zake za msingi ikiwemo sula zima la Bima ya Afya

Mhe. Spika, kwenye maadhimisho ya siku ya wafanyakazi duniani ambayo kwa Zanzibar yaliazimishwa Mahonda, Wilaya ya Kaskazini B, kauli mbiu ilikuwa ni *"*Ukuaji wa Uchumi wa taifa lolote lile unategemea wafanya kazi, hivyo haki zao zilindwe ili wawajibike". Ikiwa Serikali imeanza na uimarishaji wa mishahara ya wafanyakazi ambayo kwa ujumla ni midogo kulingana na ukuaji wa gharama za maisha, Kamati

yangu inaunga mkono kauli mbiu hii. Aidha, Kamati inashauri suala la bima ya afya, ambalo limewekwa kwenye bajeti hii ya mwaka wa fedha 2017/2018, lipewe mazingatio maalum na kuanza kutekelezwa ndani ya muda uliopangwa, hasa ukizingatia nchi jirani nyingi tayari zina bima ya afya kwa wafanya kazi wake wa umma.

Mhe. Spika, mchango wa Sekta Binafsi katika maendeleo ya nchi yoyote ile ni muhimu. Hapa kwetu, sekta binafsi tunaitegemea kwa huduma mbalimbali za kiuchumi kama vile usafiri wa nchi kavu, angani na baharini; huduma za kifedha, za mahoteli na ujenzi; kilimo, mifugo na uvuvii; bali hata katika elimu iliyo bora na huduma za afya. Haya ni baadhi tu ya maeneo ambayo yana mchango mkubwa katika kutoa ajira na makusanyo ya Serikali.

Inakuwaje basi mchango wa Sekta Binafsi ni mkubwa kiasi hicho, na kimapato nambari zinajieleza lakini bado hatuna mpango mkakati wowote wa kitaifa wa kuiendeleza Sekta hii? Wakati umefika Zanzibar ipate Sera na Mipango ya Kuendeleza Sekta Binafsi ili ushiriki wake katika maendeleo ya nchi uwiane na Dira yetu ya 2020. Tunaishauri Serikali iwe makini kuijenga Sekta Binafsi ambayo ndio muhimili mkuu wa kiuchumi kwa kuitengenezea mikakati imara ya kuweza kuzalisha na mazingira bora ya kulipa kodi.

Mhe. Spika, umakini pia unahitajika pale watendaji wa Serikali wanapochukua maamuzi ili wasiwasababishie wananchi usumbufu. Kwa ufupi, waige umakini wa Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar. Biashara ni roho ya uchumi wa Zanzibar. Inasikitisha kuwa leo ni zaidi ya mwaka mmoja tokea eneo la Darajani liondolewe makontena lakini hakujafanyika lolote zaidi ya kuikosesha Serikali mapato, vijana wetu kukosa fursa za ajira na familia zao kuzipunguzia kipato cha halali. Kabla ya Darajani kuimarishwa, tayari chanzo chengine cha mapato hapo Michenzani kimefikwa na masaibu yale yale! Na je haya maamuzi hayana wakati muafaka kuchukuliwa ila karibu na siku kuu!. Ni imani ya Kamati yangu kuwa hautopita muda mrefu wananchi wataona kwa vitendo vipi maeneo hao yanarejesha haiba ya Zanzibar kibiashara na kuwapunguzia wakusanya kodi wetu kuumwa na vichwa juu ya wapi watapata mapato ili kufikia malengo waliyoekewa.

Mhe. Spika, haitokuwa busara kumalizia hotuba yangu bila ya kuligusia Baraza la Biashara la Zanzibar "*Zanzibar Business Council"*. Kamati yangu inaamini kuwa Sekta binafsi zina mchango mkubwa sana katika uchumi wa nchi kupitia kodi na tozo mbali mbali zinazochangiwa na sekta hiyo pamoja na ajira zinazozalishwa kupitia miradi mbali mbali, hivyo kuna kila sababu kwa Serikali kuhakikisha inaishirikisha sekta binafsi wakati wa kuandaa sera pamoja na sheria mbali mbali za kodi na uekezaji. Baraza la Biashara la Zanzibar ni jukwaa "*forum*" nzuri ambayo sekta binafsi hupata fursa kukaa pamoja na Serikali kubadilishana mawazo juu ya mambo mbali mbali yanayohusu biashara, kodi pamoja na kuendeleza uchumi wa nchi kwa jumla, lakini pia kuelezea changamoto zao kutokana na utekelezaji wa sheria na sera mbali mbali za nchi. Hata hivyo, kumekuwa na kusuasua kufanyika vikao vya Baraza hilo, ambapo kwa kipindi kirefu Baraza hilo halijakaa. Ili kutimiza malengo ya kuanzishwa Baraza hilo, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe Baraza hilo linafanya vikao vyake kwa mujibu wa Sheria na maazimio yake kufanyiwa kazi.

Mhe. Spika, kwa kumalizia napenda kuwashukuru tena kwa dhati Wajumbe wa Kamati yangu, Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu na wananchi wote wanaonisikiliza kwa kunistahamilia wakati nikiwasilisha maoni ya Kamati yangu kuhusu Mpango wa Mendeleo na Mwelekeo wa Bajeti kwa mwaka 2017/2018. Aidha, nawaomba waichangie na kuishauri Serikali ili bajeti hii iwe bora na yenye tija kwa wananchi na hatimae waipitishe ili Serikali ikaweze kuitekeleza malengo iliyojiwekea.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana kabla sijawaita wajumbe ambao wataanza kuchangia hii hotuba ya bajeti naomba kwanza nisome wageni ambao tunao.

Mgeni wa kwanza ni mgeni wa Mhe. Suleiman Makame Ali Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Zawani ni Ndugu Mohamed Kassim Haji ambaye ni Katibu wa CCM Wadi ya Kwale kama yupo hapo anaweza kufika.

Wageni wengine waliopo ni wageni kwa ajili ya mafunzo wanatoka Chuo cha Utawala wa Umma IPA jumla yao ni wanne wanachukuwa Kozi ya Utunzaji Kumbukumbu na Nyaraka kwa sasa wako hapa Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya mafunzo ya vitendo. Karibuni sana.

Ahsante baada ya tangazo la wageni sasa tunaendelea Waheshimiwa Wajumbe wachangiaji waliomba mpaka sasa hivi wapo kiasi watu 15 lakini bado nafasi ipo kwa sababu tunachangia siku tatu kwa hiyo mchangiaji wetu wa mwanzo leo hii atakuwa Mhe. Shehe Hamad Mattar ambaye atafuatiwa na Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata na Mhe. Hassan Khamis Hafidh ajiandae.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kuturudishia uhai sote na tukaweza kufika hapa tukiwa makini katika kuchangiua hotuba hii ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini naomba tumtakie rehma Mtume wetu Muhammad (SAW) pamoja na sahaba zake na tuombe Mwenyezi Mungu atuweze kutuwezesha shughuli yetu hii ya leo tuweze kuifanya kikamilifu.

Mhe. Spika, kwa vile na mimi mjumbe katika Kamati ya Bajeti nitakuwa na maoni yangu mafupi sana katika masuala ya hotuba hii kwa ufupi sana nitakwenda haraka haraka lakini pia nianze moja kwa moja katika ukurasa wa 30 *paragraph* 63 inayongeza suala la mapato na mimi nendelee kuipongeza Serikali kwamba kwa kweli Wizara ya Fedha imejitahidi sana kupitia vyombo vyake mbali mbali kuona kwamba mapato ya Serikali yameongeza sana kutoka bilioni 483,000,000,0000 mpaka hadi 675.8 ambapo yakadiriwa kupatikana, ni hatua kubwa sana iliyofanya Serikali chini ya usimamizi chini ya usimamizi Waziri makini ambaye kuwa anaipenda nchi yake sana na ni Waziri ambaye kuwa ametosheka sana.

Lakini Mhe. Spika katika hotuba hii wakati akitaayarisha bajeti hii nimeona kidogo kuna kasoro fulani ambayo kuwa sikuiona lile gawiyo ambao kuwa ni matarajio ya mapato yetu tunayotegemea gawio la *BOT* halikuoneshwa pale sijui kwanini, halioneshwa mapato kutoka *BOT* nimuombe Mhe. Waziri atakapoona kwamba hili ni jambo ni vyema kulitolea ufafanuzi lakini pia vile vile suala zima la kodi inayotowa na wafanyakazi kutoka SMT nimeona imewekwa ile ile Shs.21,000,000,000 wakati wafanyakazi hawa wanaweza kubadilika mishahara sijui kwanini hatuongeza haya mapato katika sehemu hii.

Hata hivyo mapato ya nje yameshuka lakini bado uchumi wetu unaendelea na unandelea kulinganisha uchumi wa nchi jengine ambazo kuwa tumepakana nazo za Afrika Mashariki, Zanzibar bado inaonyesha kupiga hatua.

Mhe. Spika, niende katika suala zima mambo ya tarakimu katika kitabu hiki ukichukuwa tarakimu zinavyoonyesha pale katika suala zima hesabu zilipo katika kitabu ya mapato ya trilioni 1.087 ukisesabu piga hesabu zake vizuri pale ina kasoro ya pointi moja sasa sijui ilikuwa ni makosa ya maandishi au la, ni vyema kitu kama hiki kwanza nayo tukaipitia kwa sababu hesabu ndogo inaleta maana kubwa katika matumizi.

Hata hivyo naipongeza Serikali kwa hatua iliyofikia ni kubwa sana matumizi yameongezeka na mapato hali kadhilika yatakuwa yameongezeka. Aidha bado Serikali inayo vyanzo vya mapato ambavyo kuwa ikivisimamia vizuri vinaweza kuongeza pato na tukaondokana na suala la tegemezi kadiri miaka inavyokwenda mfano katika sehemu za mapato yanayotokana na umiliki wa vyombo imekuwa ni kawaida yetu kwamba tunanunua vyombo kutoka kwa wamiliki mbali mbali na kubaki na majina yale yale lakini hatuwezi kubadilisha ni vyema kwamba Serikali ione kwamba hapa tuna mapato mengi sana katika mapato ya kubadilisha umiliki wa vyombo hivi au mali nyengine Serikali inaomba iangalie sana hapo ili tuweze kupata mapato ambayo kuwa yatasaidia kutaka kunyanyua uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, niende katika *pharagrap* 73 Bajeti ya Elimu ya Maandalizi ya Msingi bado imewekwa kwa Wizara ya Elimu jee kuhusu maandalizi ya Skuli za Maandalizi za Jamii ambazo kuwa mijini kwetu na vijijini zimeanzishwa kwa nguvu za wananchi hizi sijaona vipi Serikali imezipa kipau umbele na ukiangalia zimetoa mchango mkubwa sana ambao kwa hadi sasa zinaendelea, walimu wale wamejitolea karibu miaka kumi, kumi na tano mapato yao ni madogo mwalimu anaondoka pale katika skuli zile za maandalizi za jamii anapata shilingi elfu mbili, elfu tatu, shilingi elfu ishirini au elfu kumi ni vyema hapa Serikali ikaangalia pamoja kuwa inazipa kipau umbele Skuli za Maandalizi ya Serikali lakini na hizi za jamii na jamii ninazo zizungumza sio zile ambazo zilikuwa zimewekwa na wawekezaji, zile za jamii kabisa zilizojengwa na wananchi na ikawa bado zinafanya kazi na zina mchango mkubwa sana kwa Serikali hii.

Skuli kama zile zimetoa mpaka wanafunzi ambao wamefika Vyuo Vikuu na imekuwa mara nyingi sana inatowa watu wanaoanza michupuo kupita skuli zile za maandilizi kwa hivyo Serikali inaomba sana iangalie zile nazo kwa namna moja au nyengine ziweza

kuzisaidia ama kuzipa ruzuku za kuendesha katika shughuli zile, wazee ni wanyonge wana mambo mengi sana na hali ya uchumi wao bado inasuasua.

Mhe. Spika, niende kwenye mchango wa SMZ bilioni 1.4 kati ya bilioni 6.3 ni mdogo sana huu jee kama wahisani wao hawakutoa pesa hizi ni shilingi bilioni 4.9 tutafanya nini katika masuala mazima ya ugatuzi, hapa tumetegemea kwamba Serikali inatoa mchango wa bilioni 1.4 na kweli kuweza kupata hizi bilioni 6.3 sasa kama hatukuzipata wahisani hawakutoa shilingi bilioni 1.4 hazitoweza kufanya suala zima la ugatuzi.

Niende moja kwa moja Mhe. Spika suala zima kwenye *paragraph* 76 inavyoeleza kuhusu ni TShs. bilioni 500 kuhusu ujenzi wa viwanja vya michezo. Mhe. Spika, fedha hizi bilioni 500 kwa viwanja vya Wilaya zote za Unguja na Pemba kwa kweli ni fedha ndogo sana hapa tume *overlook* kidogo kwa sababu leo tukiangalia kiwanja kimoja tuu ni fedha nyingi sana zitazotumika jee bilioni 500 hizi zitaweza kujenga viwanja au tutakwenda kutaka kusafisha maeneo ya viwanja, naomba sana hapa Serikali ituangalie tena namna gani tunaweza kuhaulisha sehemu ambayo kuwa fedha hizo zitaweza kupatikana.

Kwa mfano tukiangalia hapa Kitogani sasa hivi kuna kiwanja kinatengenezwa kile pale cha Wilaya pale tuanze kujipima pale tutaweza kutumia shilingi ngapi pale na hivyo vyengine tunataona kwamba tunafanya nini.

Mhe. Spika, niende kwenye ukurasa *paragraph* 82 kuhusu fedha ambazo kuwa tumetenga shilingi milioni 500 ambazo tutakuwa tutajenga nyumba ya Makamo wa Rais Pemba fedha hii ni ndogo hiyo nyumba tutakayojenga wa kukaa kiongozi mkubwa kama hii wa nchi kwa kweli shilingi milioni 500 ni fedha ndogo ambazo kuwa hata nyumba ya mtu wa kawaida basi inapita, hapa labda iwe nao tunataka kutengeneza viwanja na kupima tuu lakini fedha ni ndogo sana naomba sana tuone kwamba tunafute namna katika mfuko wowote ule ama tuwe tunaanza hatua ya mwanzo tuu.

Mhe. Spika, niendelee katika *paragraph* 93 kuongeza kuhusu inayozungumza kuongeza ada za magari. Mhe. Spika, Mhe. Waziri aliondowa katika sehemu hii alieleza kwamba magari yale yanayotumia nambari za majina kwa mfano mimi nataka nambari yangu nataka nambari yangu inandikwe *Mattar* pale nilikuwa nalipa shilingi 3,000,000 kwa mwaka sasa imewekwa shilingi milioni 15,000,000 ili lengo la Waziri alivyo tueleza hapa ni kwamba kuondoa ile utabaka wa watu sote tunaka kujenga kwamba watu wawe kitu kimoja lakini katika hapa bado kwamba tumeweka shilingi milioni 15,000,000 kwamba mtu atakayeweka jina lake pale kwenye *plate number* kule jambo hili bado litandelea watajitokeza watu kwasababu wamo nchi hii wana fedha za kutosha wataweka hapa ndiyo tutawaongeza zaidi kwamba ile kujionyesha kwamba mimi ndiye natamba katika nchi hii hata kama ni wawili watatu.

Lakini kama tutabakisha ile milioni 3,000,000 basi watajitokeza wengi kumbe na fulani yumo na fulani yumo lakini leo milioni 15,000,000 wanatajitokeza humu nchini wataweka nambari hizo na kutulipa milioni 15,000,000 pamoja na kwamba tutakuwa tunaongeza mapato, lakini lile lengo la kuona kwamba tunaondoa huu utabaka wa watu halitafikiwa.

Mhe. Spika, mwisho nimalizie katika majina yaliyopendekezwa katika bajeti hii, alisema kwamba ni bajeti kuhusu huduma za jamii lakini mimi naona tuongeze kwamba hii ni bajeti ya miundombini ya huduma za jamii, kwa sababu ukiangalia bajeti ya miundombinu ina fedha kubwa sana karibu milioni 297,000,000 ukilinganisha kama na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa hivyo, naomba hili jina Mhe. Waziri aone kwamba pamoja na kuwa ni bajeti ya huduma za jamii, lakini na miundombinu. Hapa lengo ni kwamba miundombinu ni wazi nayo itaboreshwa kwa hali ya juu kabisa.

Mhe. Spika, baada ya hayo niombe kitu kimoja cha mwisho kuhusu vipaumbele vilivyotolewa pale. Nimeona kuwa utalii ndio jambo linalotuingizia mapato katika nchi yetu na kuonesha sura nzima ya ukuaji wa uchumi, lakini imeoneshwa bilioni 1.5, fedha hizi kweli tunataka kuipa kipaumbele kwa bilioni 1.5 sehemu ya utalii. Sehemu ambayo ilikuwa tunasema tunataka kuangalia mambo mbali mbali ya ukusanyaji wa mapato, uingiaji wa wageni kwa hivyo shilingi bilioni 1.5 naona ni ndogo sana. Kwa hivyo Mhe. Spika, na hapo tuangalie ni namna gani tutaweza kuona kwamba kipaumbele hiki kinapata nguvu sana. Baada ya hayo naunga mkono hoja mia juu ya mia. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Shehe Hamad Mattar sasa naomba kumwita Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), atafuatiwa na Mhe. Hassan Khamis Hafidh na Mhe. Abdalla Maulid Diwani ajindae.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa katika Baraza lako tukufu na kuchangia hotuba hii ya mipango na maendeleo ya serikali yetu kwa bajeti ya mwaka 2017/2018. Lakini pia Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kazi nzuri waliyofanya ambapo leo tunaona kwamba taarifa au hotuba hii ya mipango na maendeleo ya serikali kwa bajeti hii yako mazuri na yana mwelekeo mzuri wa kusaidia wananchi wetu juu ya shida mbali mbali ambazo tunamuomba Mwenyezi Mungu aizidishie baraka nchi yetu na uwezo uwe mkubwa zaidi ili kuyaondoa matatizo yote katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi napongeza kwa dhati kabisa hotuba hii na kwa mujibu wa tulivyosoma katika mipango na hotuba ya maendeleo sina tatizo nayo, kwa sababu kubwa linalojadiliwa humu hasa tukizingatia kwamba bajeti zetu za sekta zimepita sasa tunaingia katika bajeti kuu kutoa maoni yetu mbali mbali juu ya mustakabal mwema tunaokwenda nao huko mbele. Niipongeze kwa dhati kabisa serikali yetu hii kwa kuzingatia mambo mbali mbali ya umuhimu juu ya kusaidia jamii yetu katika nchi yetu.

Mhe. Spika, katika ulimwengu wetu wa leo kila taasisi ina umuhimu wake tukienda kwenye afya, elimu, maji, barabara, umeme, ulinzi wa nchi yetu pia na mambo mengine mengi mengi ya makusanyo yanatuwezesha kwenda katika hizo nilizozitaja ili zifanikiwe. Kwa hivyo nampongeza Mhe. Waziri nawapongeza watendaji wote kwa kazi nzuri wanazofanya hasa sehemu ya mapato ya nchi yetu wanakwenda vizuri katika

makusanyo yao na nawaomba tu wazidishe bidii ili harakati zetu za maendeleo zikue vizuri zaidi tunapokwenda.

Mhe. Spika, lakini katika mazingatio maalum makubwa ya serikali yetu yaliyowekwa katika kipindi cha 2017/2018 kuna mengi, lakini kubwa ni suala la umeme ambalo tuna deni kubwa *TANESCO*. Niipongeze kwa dhati serikali yetu kuliona hili ni kero na kero kubwa sana kwa wananchi wetu. Kwa hivyo, niseme tu kwamba kwa kuliona hilo imekubali serikali yetu kujitolea yaani Wizara ya Fedha kuwasaidia *ZECO* kila mwezi kutoa bilioni 1, na *ZECO* wenyewe wajitahidi kutoa bilioni 2 kunusuru ongezeko la deni letu lisitokee. Kwa hivyo, mimi nampongeza Mhe. Waziri lakini nawapongeza na wataalamu wote walioliona hili ili liondoke.

Mhe. Spika, na tumeambiwa katika kitabu hiki kwamba inategemewa sana deni hilo tuna 65 bilioni hivi sasa, lakini mpaka kufika Juni tukijaaliwa tutakuwa tumepunguza 40.4 bilioni. Kwa hivyo, ni hatua kubwa ambayo tunafaa sisi kama viongozi na wananchi kwa jumla tuione serikali yetu imo mbioni katika kuliondoa tatizo hili. Lakini ikasema katika ukurasa wa 36 halafu kuna 25.2 bilioni itaendelea kulipa kwa kipindi cha mwaka ujao wa fedha. Naipongeza sana serikali na wizara yetu kwa kuliona hili liondolewe ili mzigo ule mkubwa waliokuwa nao wenzetu wa *ZECO* liondoke na wafanye kazi zao kwa ufanisi zaidi katika shughuli zao.

Mhe. Spika, jengine serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango pia imeona kwamba pana haja kuwa na meli nyengine ambayo itawasaidia sana wananchi wetu. Ukurasa wa 37 imesema tu kwamba zimetengwa bilioni 18 za kuanzia sio tatizo mengine najua yataendelea. Mimi niseme tu kwamba naipongeza serikali na kwa kuliona hili hasa tukizingatia kwamba Zanzibar asili yetu ni visiwa tunategemea usafiri wetu wa bahari na kupitia anga. Lakini kubwa tuseme tu kwamba hili ni suala zuri na limefika kwa wakati wake kwa kuwa meli tunayo moja nzuri ambayo inasaidia sana Unguja na Pemba pamoja na kuanzisha safari ya kwenda Comoro na kwengineko, hiyo ni hatua ya maendeleo na kuleta uchumi wa katika nchi yetu. Kwa hivyo, tuipongeze serikali yetu kwa kuliona hili wakati wake umefika wa kufanya shughuli hiyo.

Mhe. Spika, nasema tu kwamba kama hili Mwenyezi Mungu atuwezeshe na akituwezesha basi hatua za kibiashara pia zitaendelea vizuri, kwa sababu sasa hivi Mhe. Spika ukiacha Tanga watu wanakwenda Mtwara na kurudi na ongezeko la bidhaa kutoka Mtwara kuja Zanzibar linahitajika sana hii saruji yetu wanaoleta Dangote. Mheshimiwa huu ni mradi mkubwa na unasaidia sana nchi yetu, hivi sasa Mhe. Spika saruji imeshuka bei sana na tumuombe Mwenyezi Mungu zaidi ishuke na zaidi ili wananchi wetu waweze kumudu katika maisha yao ya kila siku ya ujenzi. Mheshimiwa tunajua ujenzi wa kimasikini hujengi siku moja, unaanzia mwaka mmoja mmoja au pengine miaka kumi kidogo kidogo, lakini kwa kuwa saruji ipo na imeteremka bei kwa sasa ni shilingi 13,000 unapata saruji. Kwa hivyo, tuipongeze serikali kwa kusimamia vyema hili na kuzidisha kutoa fursa kwa wafanyabiashara walete bidhaa hizo ili wananchi wetu wapate kujihudumia.

Mhe. Spika, suala jengine serikali yetu ilisema tu kwamba kuna uimarishaji wa makaazi wa askari, ukurasa wa 37 Idara Maalum ya vikosi vyetu. Mhe. Spika, mimi niipongeze serikali kwa sababu askari wetu wengi wanakaa uraiani, lakini pia askari hao hao wanahitajika wakati wa kazi za dharura inakuwa tabu kuwapata. Kwa hivyo, mimi niiombe serikali hili walililoliona ni suala zuri ambalo litaleta faraja kwa askari wetu kuwa karibu na kazi zao, pia kuwahi matokeo yanayotokea wakati wowote ili waende salama na shughuli zao na warudi salama. Kwa hivyo, hili namuomba Mhe. Waziri wameliangalia na lipo kwa hivyo niseme tu kwamba kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu *inshaallah* tutafanikiwa.

Mhe. Spika, lakini jengine serikali inaanzisha uanzishaji wa bima ya afya Tanzania, kuna bilioni 2 hapa zimetengwa ukurasa huo huo. Naipongeza tena serikali kwa kuliona hili, tena naipongeza kwa dhati kabisa kwa sababu wafanyakazi wetu watakuwa salama katika maeneo yao na mtu atafanya kazi anajua Mungu atuepushie likitokea la dharura lolote pakukimbilia anapo. Sasa tuamini kwamba bima ya afya ni kinga na bima ya afya ni msaada mkubwa kwa wafanyakazi na wananchi wetu kwa jumla. Kwa hivyo, naipongeza serikali kwa kuliona hili kwamba linafaa kutokana na shughuli mbali mbali.

Mhe. Spika, lakini kwa kuwa wananchi wetu ndio wanahitajika katika nchi yetu na wananchi wetu wanategemea huduma bora za afya katika hospitali zetu. Nampongeza tena Mhe. Waziri kupitia wataalamu wake kuongezwa kwa bajeti ya ununuzi wa dawa, chanjo na vifaa vya tiba kufikia Tanzania shilingi bilioni 8. Mheshimiwa hiyo ni hatua kubwa na naomba tuongeze bidii katika makusanyo yetu fedha hii ipatikane ili wananchi wetu wanapokwenda katika hospitali zetu wasipate shida ya kupata huduma hizo.

Mhe. Spika, kwa jumla nilisema tu kwamba serikali yetu ina maelekezo mazuri au maeneo mazuri waliyoyatunga katika bajeti inayokwenda ili wananchi wetu wapate faraja maisha yao yawe bora. Ukurasa wa 38 kuna kumalizia visima vilivyojengwa kwa msaada wa Ras-al-Khaimah Tanzania shilingi 1.5 bilioni. Mheshimiwa mimi bado naipongeza serikali na nasema hili ni suala kubwa ambalo tunapiga kelele Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, mmoja ikiwa kwa jimbo langu la Kijitoupele. Mhe. Spika, nina visima vitatu vikubwa nasema kila wakati kama vitatengenezwa hivi tatizo la maji katika Jimbo la Kijitoupele itabakia historia. Kisima cha Tomondo, Uzi, kisima cha Kijitoupele na kisima kimoja ambacho kipo hapa Magirisi kwenye hospitali mpya.

Mhe. Spika kama vitatengenezwa visima vitatu hivi basi maeneo ya Kwarara, Kijitoupele, Tomondo, Melinne Uzi mpaka Melinne nasema maji itakuwa kwetu sisi ni historia na sitolaumiwa tena na Mamlaka ya Maji, kwa sababu unajua tatizo letu katika nchi hii ukisema kweli unaonekana adui. Lakini mimi nasema tu mwananchi wangu aliyenichagua na asiyenichagua mimi ndiye msemaji wake hapa na kuelekeza kero zao ili zitengenezwe. Naiomba serikali kupitia hili ambalo ni wazo zuri Mamlaka ya Maji wapewe fedha hizo na waanze kazi zao mapema ili wananchi wetu waondokane na adha hii ya kila siku. Kwa hiyo, hilo ni suala zuri ambalo naamini kwamba wananchi wetu watapata maendeleo mazuri.

Mhe. Spika, michezo ni sehemu ya ajira tuna vijana wetu wako Mwanza sasa hivi wamekwenda katika mashindano mbali mbali ya Umiseta**.** Kwa hivyo, niishukuru serikali pia kuona kwamba michezo iko aina kwa aina lakini kwa Zanzibar au duniani michezo mikubwa inayopendelewa ni mchezo wa mpira wa miguu hatufichani. Ukienda Marekani unakuta *basketball* lakini kwa kwetu sisi ndio mchezo wetu mkubwa huo. Kwa hivyo, niipongeze serikali kuona kwamba ukurasa wa 39 ujenzi wa viwanja vya michezo Wilaya vina bilioni 5. Hili ni suala kubwa na suala zuri ambalo tunaona wazi kwamba serikali imejidhatiti kweli kweli kuliona hili kwamba limefikia wakati wake ili kuimarisha michezo mbali mbali kwa ajili ya vijana wetu, kwa sababu ajira inaanzia kwenye michezo. Hili walililoliona pia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwamba sasa hivi umefika wakati vijana wetu waendelezwe katika fani mbali mbali za michezo ili kuongeza vipaji vyao, naipongeza serikali kwa hili.

Mhe. Spika, jengine kuna uanzishaji wa mfuko wa elimu Tanzania shilingi bilioni 2.5 na hili nalo ni kubwa, na hii inaonesha dhahiri kwamba serikali imejidhatiti kwamba kuekeza katika elimu ili vijana wetu wajitayarishe na hali ya ulimwengu ilivyo sasa hivi, kwa sababu elimu ni msingi na elimu ni mwanzo wa kuhakikisha kwamba kila kinachofanyika dunia ya leo uwe na elimu ambayo itakusaidia katika maisha ya kila siku.

Mhe. Spika, ukizingatia hilo mheshimiwa kuna suala ambalo ni zuri tu, vijana wengi hivi sasa Tanzania ilishiriki katika mashindano ya kombe la vijana chini ya umri wa miaka 17. Tulishuhudia kwamba Tanzania Bara imeingia katika nane bora na imetolewa kwa bahati mbaya ingawa ilikuwa kama Simba na Yanga tumeshikana kwenye *point* lakini tulizidiwa kutokana na magoli. Kwa hivyo mimi niipongeze timu yetu ile ilifanya vizuri kwa niaba ya Tanzania kwa sababu sote ni Watanzania, lakini kitu kinatakiwa kuzingatiwa kwamba tujitayarishe na sisi katika michezo hii hivi sasa hivi, kwa sababu tunakokwenda mheshimiwa kuna mashindano mbali mbali. Kuna Afcon kuna nini, lakini bado mpaka leo sisi Zanzibar tumepata uanachama bahati nzuri tunashukuru tunawaomba viongozi wanaohusika na mambo ya michezo *ZFA* na Baraza la Michezo la Taifa wajiandae kufanya haraka katika kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri na tunakwenda na kalenda yetu ya Shirikisho la Soka la Afrika ili tuhakikishe kwamba hatukosi mashindano ya aina yoyote. Mechi za wanawake, vijana, hayo yote tunataka tuyaandae vizuri ili tufanikishe kujiunga huko.

Mhe. Spika, lakini jengine kitu kikubwa ambacho tunasema tu kwamba mapato ni maendeleo ya nchi, na bila ya mapato huwezi kufanya lolote. Lakini niseme kwamba serikali yetu imejitahidi na inaendelea kujitahidi. Mimi nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote kama nilivyosema mapema lakini nitoe wito sasa kwamba kamati imefanya kazi nzuri, nawapongeza kamati kwa kuzipitia bajeti zetu zote na kuona kila panapostahiki ili paongezwe bidii au paongezwe juhudi kufanya vizuri zaidi. Mheshimiwa ninaloliomba natoa wito kwa serikali tuzidi kusimamia watendaji wetu wa sekta za fedha, lakini pia wafanyakazi wetu wote. Mhe. Rais kwa imani yake na kwa kauli yake aliahidi kwamba nikishinda katika uchaguzi si vibaya na mimi nina mengi nilitoa ahadi katika jimbo langu lazima niyatekeleze kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu ataniwezesha, alisema nitaongeza kima chini asilimia mia moja, hilo amelitekeleza.

Kwa hivyo, nitoe wito kila taasisi inayoshughulikia wafanyakazi wake, wafanyakazi wote wafanye kazi kwa uimara, wafanye kazi kwa uangalifu, wafanye kazi kwa juhudi ili tumpe imani Rais wetu kwamba kile alichokitoa kakituoa kwa nia njema kwa wananchi wake na kujali hali ya maisha tuliyo nayo katika nchi yetu. Tukifanya hivyo na tukienda hapo Mhe. Spika itakuwa tumemfanyia haki na tumeifanyia haki serikali yetu. Nimuombe Mhe. Waziri wafanyakazi wetu wawe makini, wafanye kazi vizuri ili tija ya serikali iongezeko na pato la nchi lizidi kukua.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache kwa heshima kabisa mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wote wa Jimbo la Kijitoupele walionichagua na wasionichagua lakini naamini mwaka 2020 watanichagua kwa sababu *speed* ninayokwenda nayo kama ya Mhe. Magufuli. Naomba kuiunga mkono kwa asilimia mia moja taarifa hii sina wasi wasi nayo hotuba nimeipokea. Ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Shihata kwa mchango wako naomba sasa nimwite Mhe. Hassan Khamis Hafidha atafuatiwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Suleiman Sarahan Said ajiandae.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Spika, na mimi naomba nichukue fursa hii kukupongeza wewe kwanza kwa kunipa nafasi hii ya kuichangia bajeti maalum ya iliyokuja kwa kipindi maalum cha Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeongoza awamu ya saba Dkt. Ali Mohamed Shein.

Mhe. Spika, nimetumia sana neno maalum kwa sababu hii ni bajeti maalum. Jana tulipokuwa tunazungumza kuhusu hii bajeti Barazani alisema kwamba kwa kweli Mhe. Rais wa Zanzibar anahitaji kupongezwa lakini pamoja na mawaziri wake wote lakini akiwemo Dkt. Khalid Salum aliyeleta bajeti iliyokuja na lengo kuu lile walilotuachia wazee wetu la kuyatunza, kuyalinda na kuyatekeleza Mapinduzi Matukufu ya Januari, 1964 kwa maendeleo ya wakwezi na wakulima.

Mhe. Spika, ukiangalia bajeti hii imemgusa kila mtu, kila mtu atafanikiwa na bajeti hii kama tutaifanya kama mwenyewe Waziri wa Fedha na Mipango alivyoileta humu. Ukiangalia bajeti imemgusa mkulima ina lengo la kumletea maendeleo mkulima, ina lengo la kumletea maendeleo mkwezi, ina lengo la kumletea maendeleo mfanyakazi, ina lengo la kumletea maendeleo mfugaji, ina lengo la kumletea kila mtu Mhe. Spika. Kwa hivyo, mimi nachukua fursa hii kwa dhati kabisa pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Welezo la kuipongeza Serikali ya Awamu ya Saba kwa kutuletea bajeti iliyofikia Trillioni moja na *points something*. Hii ni faraja kubwa na tunaona jinsi gani serikali yetu imejipanga katika kuleta maendeleo endelevu kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, sasa naanza kuchangia bajeti, kwenye hiki kitabu cha Hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Khalid Salum Mohamed kuwasilisha hali ya uchumi wa maendeleo kwa mwaka 2017/2018. Ukifungua ukurasa wa 8 kuna kitu kinasema 'Mfumko wa Bei'. Mheshimiwa sote ni mashahidi nchi nyingi duniani zikiwemo zilizoendelea na zisizoendelea hasa nchi zisizoendelea zilihama kutoka kwenye mfumo wa kijamaa na kuhamia katika mfumo wa kibepari. Mfumo wa kibepari maana yake nini?

Mfumo wa kibepari maana yake njia kuu za uchumi zitamilikiwa na Matajiri, ma-Bwannyenye au ma-*Bourgeoisie*. Kwa hivyo, wao ndio watakuwa waendesha biashara na wao ndio watakaomiliki mambo mengi.

Mhe. Spika, sio siri nchini kwetu tumekuwa tunashuhudia mfumko wa bei usioeleweka, mwaka mmoja na nusu au miwili nyuma tulishuhudia upandaji wa bei ya mafuta ya petroli na dizeli, wafanyabiashara walikuwa wanafanya wanavyotaka katika kupandisha mafuta, wanayazuwia siku mbili yasitoke halafu yakitoka tayari wameshapandisha shilingi mia au mia mbili, lakini leo naipongeza sana *ZURA* imeweza ku-*control* suala hilo. Naiomba sana *ZURA* iendelee kufanya hivyo kwa maslahi ya wananchi wetu wakwezi na wakulima.

Mhe. Spika, juzi Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango alipokuwa akisoma hotuba yake alisema naomba ninukuu, kwamba: "Serikali imeamua kuwaondoshea au kuwapunguzia ulipaji wa kodi kunako bidhaa kama mchele, sukari, tende na mafuta".

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu mimi na wenzangu tumefanya utafiti wa hali ya juu kuona kweli vitu hivi vimeondoshewa kulipiwa kodi hasa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Je, vimepungua bei? Mheshimiwa utafiti unaonesha bei imezidi, bei ya vyakula licha ya kwamba Mhe. Waziri wa Fedha kawaondoshea kodi wafanyabiashara lakini la kushangaza bei ya vyakula imezidi.

Natoa mfano, tende kabla hawajaondoshewa kodi ilikuwa inauzwa shilingi 64,000 kwa lile katuni, mpaka jana saa 6 na dakika 20 tende inauzwa shilingi 96,500. Mhe. Spika, tende imeondoshewa kodi ilikuwa ishuke bei lakini imepanda bei.

Mhe. Spika, ndio niliposema huu ni ule mfumo wa kutoka katika ujamaa kwenda katika ubepari bila ya kuangalia wafanyabiashara watatuumizia wananchi wetu, imekuwa kama wanawakomoa. Nchi za wenzetu zina kitu kinaitwa Tume ya Bei, Tume ya Bei inapokuwa *strong*, Tume ya Bei inapokuwa inafanya kazi zake huwezi kupandisha bei za vyakula kiholela unavyoamka wewe.

Mhe. Spika, nilitoa mfano bajeti iliyopita kwamba mfanyabiashara hana dini, dini ya mfanyabiashara ni *profit*, faida na kitabu chake ni ghilba. Leo Mwezi Mtukufu wa Ramadhani tulitarajia baada ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwaondoshea kulipa kodi wafanyabiashara sote tulitarajia bei zitashuka. Mhe. Spika, bei zimezidi naomba sana Mhe. Waziri wa Fedha jambo hili anapotaka kulifanya tena alifanye kwa umakini na alifanye kwa uangalifu sana.

Mhe. Spika, naomba kutoa ushahidi mwengine. Katika nchi yetu kuna kadhia kubwa sana ya mchanga, juzi siku tatu zilizopita tulikuwa tunafanya utafiti wa mchanga, ninayo karatasi humu inaonesha bei za mchanga unavyouzwa kule shimoni nimekwenda kuchukua kwa kufanya utafiti. Mheshimiwa kama sikosei gari ya tani kumi kule shimoni inauzwa shilingi 71,600 unatakiwa ukalipe benki, hii ni gari ya tani kumi na kule shimoni unapakiliwa kwa shilingi 65,000 na kuna pahali unalipa shilingi 5000, ukijumlisha unakuta kama shilingi 141,000 kama sikosei. Mhe. Spika, hii ndio bei ya mchanga plus

mafuta ya gari labda shilingi 50,000 kwa shilingi 210,000 tani kumi ya mchanga upo Mwanakwerekwe.

Mhe. Spika, sio siri mfanyabiashara kwa sababu hakuna tume ya bei *strong* anauza shilingi 480,000; Mheshimiwa wafanyabiashara tusipowatizama kwa macho mawili, tusipowaangalia wataifanya serikali yetu kila siku isemwe vibaya, wataifanya ichukiwe na wananchi, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha ingawa ipo Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inayoshughulikiwa tume ya bei, lakini nathubutu kusema leo nafikiri kazi yake idara hiyo haiijui kwa sababu bei haziko *regular* bei zinapanda na kushuka kama sijui niseme kitu gani. Mheshimiwa bei haishuki bei inapanda tu nchi hii na mfano huo wameondoshewa wafanyabiashara kulipa kodi lakini ndio kwanza mchele, sukari, unga na tende vimezidi bei, leo mchanga unam-*cost* mfanyabiashara shilingi 210,000 yeye mfanyabiashara anauza shilingi 480,000. Huu ni wazi kwamba wafanyabiashara wanataka kutukomoa sisi wananchi na kutukomoa kwao sisi wananchi *outcome* yake ni kuitia mdomoni serikali yetu, kuifanya serikali yetu isemwe vibaya hali ya kuwa inajitahidi kila uchao kuhakikisha wananchi wake wanaishi salama na wanapata huduma zote muhimu lakini wafanyabiashara wanawakomoa wananchi wetu.

Mhe. Spika, naomba kusema leo, naomba kupendekeza Mhe. Waziri wa Fedha anaposamehe hizi bei asibakie kusema si kazi yangu, asione hii ni kazi ya Wizara ya Biashara bali afuatilie kujua kwamba kile alichikifanya je, kimefikia lile lengo lililokusudiwa? Mhe. Spika, serikali yetu imesamehe mapato chungunzima kwa wafanyabiashara kwenye unga lakini leo hatimaye imekuwa ni kuwakomoa wananchi bei kuzipandisha licha ya kuwa serikali imesamehe kodi. Hii sio sahihi na hii haiwezekani, naiomba sana Wizara ya Fedha ndio iliyosamehe wafanyabiashara kodi ifuatilie ijue kwa nini wafanyabiashara hawa wameongeza bei za vyakula na kama yuko aliyeongeza bei za vyakula wamo wamejaa afutiwe kibali nchi hii asifanye tena biashara katika nchi hii akatafute kwengine afanye biashara. Haiwezekani serikali inajitahidi ili wananchi wake waishi vizuri atokee mtu au kundi la watu awe anawakomoa wananchi. Mhe. Spika, namuomba sana Waziri wa Fedha hili alifuatilie na sisi kwa sababu tumeletwa humu kwa maslahi ya wananchi kwa hili hatutokaa kimya. Naiomba sana Wizara ya Biashara ndio yenye tume ya bei ifanye kazi tume hiyo zamani ilikuwa inafanya kazi katika kuhakikisha bei zinakuwa elekezi zilizotolea zinafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, ushauri wangu tume ya bei irudi kama zamani, haiwezekani ni hatari imekuwa bei zinakwenda kiholela sana wanazipandisha vibaya. Kama tutakuwa tuna tume ya bei *strong* mambo haya hayatokei.

Mhe. Spika, pili napenda kuchukua fursa hii kuipongeza sana serikali bajeti hii nilisema imemgusa kila mtu, Mheshimiwa kuna shilingi bilioni kumi za mishahara ya wazee pencheni zile za wazee zinapanda shilingi bilioni kumi zipo, naipongeza sana serikali kwa kuwaona wazee wetu nao waliofanya Mapinduzi, waliotulea, waliotusomesha wakatufikisha hapa tulipofika na wao wametizamwa kwa kuwaongezea viwango vyao vya pencheni yao.

Mheshimiwa nilisema mwanzo bajeti hii ni bajeti iliyokuja kuwaokoa wana Mapinduzi, bajeti iliyokuja kuwaokoa wakulima na wakwezi na ushahidi tumeuona wazee nao wamekumbukwa pencheni zao keshokutwa zitapanda.

Mhe. Spika, ukiangalia kuna kuimarisha mapato, naomba kushukuru sana katika kuimarisha mapato lakini tunatakiwa tuangalie vitu viwili vikuu; tuangalie kitu kinachoitwa kwa Kizungu *structure adjustment program* ambazo tuzifanye. Kwanza kama kwenye ile hotuba ya Rais aliposema atahakikisha kwamba yale matumizi yaliyokuwa si ya lazima katika serikali yatakuwa hayafanyiki. Lakini namba mbili nchi nyingi zinashindwa kufanya mambo yake yaliyojipangia kutokana na kama hilo alilolisema Mhe. Rais katika hotuba yake ya mwanzo katika kulizindua Baraza la Wawakilishi kukata matumizi yaliyokuwa sio ya lazima. Jengine lile tunalolikataa sisi wana CCM, Rushwa. Kwenye ahadi za mwanachama wa Chama cha Mapinduzi tunasema sitatoa na sitapokea rushwa.

Mhe. Spika, ili tuweze kuitekeleza bajeti hii kama tulivyokusudia mambo haya mawili lazima tuwe waangalifu sana, tukitizama kitabu hiki pana pahali kinaeleza waziwazi kuna miradi ya maendeleo. Mheshimiwa kama hatujakuwa waangalifu naomba kwa Waziri wa Fedha miradi ya maendeleo kwa mfano ya ujenzi wa barabara, ujenzi wa nyumba, ununuaji wa mambo mbali mbali, huku ndiko wale wajanja wanapokuwa tena wanatafuta kutupiga changa la macho. Sio siri nitatoa mfano Wizara ya Fedha ilitaka kujenga jengo kule Pemba inasemekana akapewa fundi mabomba aombe ile *tender*, akaomba lile jumba leo limeporomoka lote.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri ndiye anayetoa fedha sasa asitoe pesa za maendeleo kununua, kujenga au kufanya mradi wowote akasema ndio nimeshawapa ana jukumu bado la kuzifuatilia pesa zile zimetumikaje ili *value for money* ipatikane, haitopendeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetoa shilingi 20 bilioni katika kujenga nyumba lakini wajanja wameijenga nyumba ile wamenunuliwa magari wengine ili *tender* itolewe kwa mtu yule imejenga kwa shilingi 11 bilioni na shilingi bilioni tisa zote watu wamekula.

Mhe. Spika, bado jukumu hili litakuwa ni jukumu la Waziri wa Fedha kwa sababu yeye ndiye anayetoa pesa, ahakikishe alichokitoa hata kama shilingi, Waingereza wanakwambia *'even pens counts,* hata kama shilingi lazima awe na jukumu la kuhakikisha kwamba pesa yetu tuliyoitoa imekwenda katika lengo lililokusudiwa. Kwa utaratibu huu ndio tutafika lakini kwa utaratibu wa kwamba nimetoa tu, halafu hajui kamuachia mwenye sekta hatutofika ndio itakuwa kila siku tuna mashaka. Leo tumetoa pesa ya kujenga jengo kama Limbani ukiangalia pesa zilizotolewa kujenga jengo hilo Pemba na pesa zilizotumika hazifanani lazima ujanja upo; ukiangalia pesa zilizotolewa kujenga jengo lile la watu wenye kutumia madawa ya kulevya kule Kidimni 1.4 bilioni zimetumika katika kujenga jengo la kuwasimamisha watu wenye kutumia madawa ya kulevya 1.4 bilioni ukiangalia haifanani, hata shilingi 600 bilioni haifiki kwa ule uchafu uliojengwa pale watu wametupiga changa la macho pale.

Mhe. Spika, ukiangalia miradi mbali mbali ya serikali pesa iliyotolewa na aina ya lile jengo au kile kitu kilivyo havifanani. Mfano mwengine pale Shirika la Magazeti jengo jipya lililojengwa walikuwa wamepanga kutumia shilingi 270 milioni kwa kufanya *repair* haiwezekani, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha bajeti yetu ni nzuri lakini kama tutakuwa tunafuatilia utaratibu wa matumizi ya pesa kwa ukaribu sana bila ya kumuonea haya mtu, bila ya kumuonea aibu mtu mimi namwambia tutaendelea na tutafika; lakini kama tutakuwa tunaonekana haya, aibu, akiwaachia *Tender Board* Mheshimiwa hatutofika.

Mhe. Spika, lakini chengine katika kupata ufanisi wa utendaji katika serikali na matumizi mazuri ya pesa lazima haya mambo ya *purchasing* hii sheria ya manunuzi, mambo ya *tender* haya lazima yabadilike. Kuna ushahidi usiopingika kama mtu anataka kuomba *tender* anawajua wale watu wa bodi ile wanaopitisha ile *tender* wengine anawanunulia magari, wengine anawajengea nyumba, ili ile *tender* aipate. Juzi kuna mtu mmoja anasema namjua mtu fulani alinunuliwa gari akanunuliwa na nyumba ili apitishe *tender* fulani. Mhe. Spika, utaratibu huu upo unafanyika na tumeona jinsi gani leo ripoti iliyotolewa na Kamati ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayohusu mchanga wenye madini tumeiona. Na mimi nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wale wote waliohusika kuitia Tanzania ambayo ni nchi masikini kuiibisha rasilimali yake basi huwa Ndugu yangu Mhe. Nadir Abdul-latif hapa anayo *proposal* yake anakuwa anaitoa na mimi namuunga mkono, wa kunyomngwa tu. Kwa sababu watu wangapi wamekufa Muhimbili, wangapi wamekufa Mnazi Mmoja na waliopsababisha vifo ni wao kwa sababu wao ndio waliyoifanya Tanzania iibiwe pesa zake na wajanja Wazungu leo hii Watanzania wanakufa na pesa zao wanazo.

Mhe. Spika, Zanzibar namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha ahakikishe pesa anayoitoa imetumika kwa lengo lililokusudiwa na sheria ya kununua ile wanayoiita Sheria ya Manunuzi zile bodi lazima ziundwe tena, zitizamwe ziwe *screened* walivyoona Waingereza *'very well screened* tuwajue kina nanio wanaopitisha hizi *tender*.

Mhe. Spika, bodi ya kupitisha *tender* China, bodi ya kupitisha *tender* Ujerumani, ni bodi aina watu wa vyombo vya ulinzi na usalama watupu, watu na majaji watupu ndio wanaopitisha matumizi ya hizo *tender*. Leo hii unapomleta mtu tu hapa unamtia katika bodi ya kupitisha shilingi bilioni za pesa mtu mwenyewe keshachoka keshafanya kazi mpaka keshachoka hajapata, leo hii anakuona kuwa Mjumbe wa Bodi kwa kupitisha *tender* njaa imemshika. Mhe. Spika, akiambiwa kuna gari mbio anachukua gari, akiambiwa kuna kiwanja mbio anataka kiwanja kwa sababu ya njaa keshafanya kazi miaka 30 au 40 hana alichokipata leo hii anakuwa mjumbe wa bodi ile hana isipokuwa anatafuta kututia changa la macho tu Mhehsimiwa.

Mhe. Spika, umefika wakati *to be honest with you* utaratibu huu uishe ili Zanzibar tuendelee, Mheshimiwa tuache muhali atakayetupeleka kuzifanya pesa zetu zitumike vibaya ikibidi tumnyonge Darajani tumnyonge Darajani watu wote wamuone, haiwezekani kwa sababu anatufanyia watu wengine wanakufa kwa nini yeye tumuache haiwezekani. Mimi naungana mkono na Mhe. Nadir Abdul-latif Zanzibar sio nchi ya

kuwa masikini, lakini wapo kama alivyosema Nelson Mandela *poverty is a man made*, wako wanaosababisha umasikini Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sio siri wapo wanaousababisha umasikini Zanzibar, umasikini haukuumbwa aa, umasikini *is a man made* kama alivyosema Nelson Mandela ni kitu kinachotengenezwa na wanadamu. Kwa hivyo, Mheshimiwa Baraza hili la Tisa tunadhamiria sote kwa pamoja kuwatafuta, kuwafichua na kuwaanika wale wote wanaotengeneza umasikini ambao umeshatutosha Zanzibar.

Juzi unakwenda Hospitali ya Mnazi Mmoja unamkuta mtu pale anayayatika na ukitizama ukifanya utafiti unajua hasa huyu sababu yake ya kifo itakuwa ni umasikini sio chengine, kama Ulaya, Marekani na Canada hafi huyu, lakini hapa anakufa kwa sababu ya umasikini na umasikini ambao umeletwa na mwanadamu. Namuomba sana Waziri wa Fedha amechaguliwa na wananchi wa Donge.

Mhe. Spika: Bado dakika moja Mheshimiwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Rais kamuona kwamba anafaa akazisimamie pesa zetu za wakwezi na wakulima shilingi moja wale waliozowea kupiga changa la macho safari hii wasiipate, hapo ndipo tutakapomjua Dkt. Khalid Salum na namuamini ameanza kufanya kazi vizuri Wizara ya Fedha, amewatoa watu wameiba 1.1 bilioni kwa maneno yake mwenyewe kasema hawa waliosababisha wizi wote amewasimamisha kazi.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri aendelee hivyo. Zanzibar si nchi masikini lakini wapo watu wanaoifanya Zanzibar iwe masikini, tumechoka nao, tumechoshwa, hatutaki kuendelea hivyo tunataka kuiona nchi yetu kwa lengo lile lile alilotupindulia Mzee Karume kwa manufaa na maendeleo ya wakwezi na wakulima ndio nchi hii. Leo hii tumeondosha ukoloni nchi hii ili tuje kuendelea lakini bado baadhi ya watu wanauleta ukoloni mambo leo kututawala na kutaka kutuchukulia pesa zetu, kwa hili namuamini sana Mhe. Waziri na naamini hili litakuwa la mwisho

Baada ya hayo machache kwa leo Mhe. Spika, naipongeza sana serikali kwa kutuletea bajeti ya maendeleo, naipongeza sana serikali lakini naiomba sana serikali, namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha awe makini, awe macho, ili vitabu hivi tulivyoviandika kwa madaha na umakini viweze kufikia lengo.

Baada ya hayo naomba kuiunga mkono bajeti yote ya serikali na naiomba sasa tukaisimamie katika kuitumia na sisi wengine tumo humu tutakayemuona, tutakayemsikia tutatumia spika zetu kumtaja yule mpinga Mapinduzi na mpinga maendeleo. Naomba kuwasilisha.*(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako naomba sasa nimwite Mhe. Abdalla Maulid Diwani akifuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said lakini simuoni badala yake atakuja Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Spika, ahsante sana nakushukuru kwa dhati ya moyo wangu kunipa fursa hii kuchangia hotuba ya bajeti ya serikali. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kusimama mbele ye Baraza lako tukufu kupata nguvu, kusema yale machache nitakayojaaliwa kusema katika bajeti hii. Kama ninavyosema kwamba tumeshachangia bajeti hizi zote hiki kitabu ni cha majumuisho kwa matumizi yale yote yatakayofanywa. Kwa hiyo, itakuwa sio mazungumzo makubwa sana kwa sababu yote tumechangia katika wizara mbali mbali.

Vile vile kwa dhati ya moyo wangu kabisa nimpongeze Mhe. Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa namna ambavyo alivyoelekeza serikali yake kupitia mawaziri wake hatimae leo hii kuletwa bajeti iliyovunja rikodi kwa Zanzibar ni rikodi ya mwazo ya *1. trillion* kuondoka kwenye maziro 7 mpaka 8 tumekwenda kwenye 9 mpaka 10. Hongera sana Mhe. Rais kupitia Waziri wako wa Fedha daktari Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Donge Dr. Khalid Salum Mohamed na watendaji wake, hatutofanya haki kama tunamsifu Mhe. Waziri peke yake bila ya kuwasifu na watendaji wake katika wizara ile kaangu Khamis Mussa na wengineo.

Nawashukuru sana wamekaa pamoja kutuletea bajeti hii ambayo ni bajeti ya kwanza kufika katika *Digital* ya *trillion* ni bajeti imekuwa mkombozi kwa Wazanzibari kama ilivyoandikwa katika kitabu chao. Vile vile ni bajeti iliyosheheni matumaini kama alivyotangulia mtangulizi wangu kwamba imejaa au imesheheni matumaini kupitia wakulima, wakwezi, wavuvi na wengineo bajeti hii ya mwaka 2017/18.

Tunakuomba sana Mhe. Waziri usiimamie kwa dhati ili lile lengo lililokusidiwa kwenye bajeti hii linafikiwa na kwa uwezo wako na uaminifu wako tunaamini kwamba yote yanawezekana. Hongera sana Mhe. Waziri.

Vile vile niendelee katika hotuba yangu nisipoteze muda sana nakwenda katika suala zima la biashara. Mhe. Spika, ili tupate hizi fedha zote asilimia kubwa sana imo katika biashara. Wakati tunachangia Wizara ya Biashara tuliona namna gani biashara ilivyoanguka bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Bara ya bilioni thamanini na nne kutoka bilioni mia nne na moja na kumi na mbili. Mhe. Waziri pamoja na bajeti hii lakini alipofika kwenye malengo haya makadirio uliyoleta kama hatuaangalia azma nzima kwenye upande wa biashara tumejikwa wapi tumeanguka wapi ili kuona kwamba biashara yetu 2017/18 inaendelea kukua sio kupungua. Huku nyuma tuliona 2016/17 ilikuwa bilioni mia nne na moja. Lakini sasa hivi tunakwenda katika bilioni thamanini na nne ni ndogo na bajeti hii ni kubwa.

Ningekuomba sana Mhe. Waziri katika hicho ujitahidi sana *at least* kuweza kurudisha matumaini kama bajeti yetu inavyotuoneshea. Bajeti hii vile vile imekuja katika suala la ukusanyajiwa mapato vianzo vyetu vikuu *TRA* na *ZRB* wanafanyakazi vizuri. Lakini kipindi si kirefu tu imetokea changamoto ambayo tunaweza kusema kwamba uelewa au tuseme uthubutu wa wafanyabiashara wetu kwamba bidhaa unaponunua Zanzibar katika maduka ambayo yamekuwa *VAT Registered*, yule mnunuzi hana matatizo na biashara ile kwa sababu *VAT* yake keshailipa kwa aliemuuzia kama mzigo ule utaenda kuuchoma

moto, utaugawa, utautupa ni wa kwako wewe, wewe huna kesi na *ZRB* kwa sababu tayari kule umeshalipa.

Sasa vereje wafanyabiashara wetu wanaponunua bidhaa ile pale wakisema wanasafirisha tu kwenda upande wa pili wanakamatwa na wakati wale hawalipi *VAT*. *VAT* tayari ameshaicha kwa alimuuzia biashara kuna changamoto hiyo Mhe. Waziri. Nakuomba sana kwamba hilo ni tatizo kwa sababu mtu akienda kununua biashara tayari *including VAT* ndio maana *VAT* yako tayari umeshachukuwa mimi nimechukuwa mzigo wangu ninakoupeleka ni wa kwangu mimi taratibu nimezifata sio nikamatwe kule niambiwe sijalipa *VAT* haiendani hiyo hiyo ni changamoto moja ya biashara zetu. Nakuomba sana Mhe. Waziri katika hilo uliangalie.

Lakini vile vile kuna *non tariff barrier* ambazo sio za msingi kwa upande wa Tanzania Bara kwenye bidhaa zetu na wewe ni shahidi wa kutosha juzi tu hapa imekaa sukari iliyozalishwa Mahonda zaidi ya miezi miwili na siku kadhaa mfanyabiashara kanunua sukari kiwandani kapata *document* halisi katengeneza *transfer form* yake kupeleka Tanzania Bara hawaamini kama Zanzibar kuna kiwanda cha Sukari. Inashangaza sana serikali hizi mbili haijulikani hata mwenziwe anafanya kitu gani kwa sababu unakwenda kwenye biashara Mhe. Waziri hiyo ni changamoto imeleta usumbufu katika hii biashara, watu wanaogopa kufanya biashara kwenye bidhaa ambazo zinazalishwa ndani ya nchi yetu hususan biashara ya kipusa ya sukari nchi hii.

Unapopteleka biashara Tanzania Bara sukari iliyozalishwa Zanzibar basi unatafuta kiama utakwenda na kila pale *certificate voucher* utakwenda nayo in *tax invoice* utakwenda nayo, lakini wale kule hawaamini kama kweli bidhaa ile inatoka Zanzibar. Sasa ningeomba sana mnapokaa wakubwa mueleweshane kwamba na sisi tuna kiwanda cha sukari toka miaka hiyo, kilikufa tu lakini kwa azma ya Dr. Ali Mohammed Shein kimefufuka kiwanda kile na kinaanza kuzalisha tena sukari nzuri, wenzetu mara kwa mara wanapata matatizo ya sukari waje Zanzibar wanunue sukari yetu ile ili liongezeke pato katika nchi yetu. Tutapojikaza katika kile cha sukari afadhali kitasaidia kununua uchumi wa nchi hii hiyo bajeti yake Mheshimiwa ikakidhi katika masuala hayo.

Lakini si hilo tu katika bajeti yako Mhe. Waziri *non tariff barrier* kwa upande wa bidhaa zetu tulizungumza wakati tunachangia Wizara ya Biashara kuhusu bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara *local production* bidhaa za ndani kwa mfano maji. Mimi nitasema sana katika hilo kwa sababu nina *interest* katika kiwanda kimoja cha maji. Hatuwezi kupeleka bidhaa zetu za maji Tanzania Bara kulikoni, kwa nini wenzetu wale wanakuja na magari yako pale bidhaa za maji ikifika pale havihisabiwi vizuri hata *ZRB* pengine kama hawaangalii mzigo ule mzigo uliokuwemo na *document* ziliokuwemo zinaona kuweza kutoka katika soko letu za Zanzibar.

Sisi kupeleka kule hatuwezi kupeleka tatizo nini tumerogwa na nani ili tunashindwa kutoa bidhaa yetu ya maji hapa ikiwa *drop, cool* na nyenginezo kuingia kwenye soko la Tanzania Bara ila wenzetu wanaweza kutoa bidhaa zao kule kuingia kwenye soko la Zanzibar ambalo lina-*demand* ndogo. *Demand* yetu ni ndogo sana ukilinganisha na viwanda tuliokuwa navyo, tutakwenda baada ya siku tutasema viwanda vimekufa. Ni

kweli hatuwezi kuhangaika kwa kutegemea soko la Zanzibar tu, utalii *season* na *low season* na wananchi wetu wanaonunua maji hawafiki hata laki tatu wakanunua maji wakanywa, tunagemea soko la Tanzania Bara ambalo lina watu wengi kuna msongamano wa watu tukaweza kuuza bidhaa yetu ile. Nitakuomba sana Mheshimiwa katika hilo.

Juzi tu tulipelekea bidhaa ya maji imeweza kukaa pale zaidi ya mwezi mmoja kama *ZBS* tayari basi *TBS* ipo. Sasa kuna tatizo gani wale *TBS* sisi *ZBS* kutubaliane na changamoto nyengine ambazo hazina msingi. Ningekuomba sana Mheshimiwa tunaipenda nchi yetu au tunapenda nchini zote mbili na sote ni ndugu kabisa katika upande wa biashara ya sisi angalau tuachiwe tujifurukute kidogo katika hicho. Najua Mhe. Waziri ulewedi mnakaa kila siku mnapitia mambo mbali mbali katika suala hilo, lakini ningekuomba sana.

Chengine kuna suala la *double taxation* suala la *VAT*. Hapa hujaizungumza katika hotuba yako. Changamoto ipo kubwa mpaka dakika hii basi tungeomba tungeandaliwa utaratibu mzuri kwa wale wafanyabiashara wetu ambao wanakwenda kununua bidhaa Tanzania Bara katika wale wafanyabiashara au viwandani ambapo wako *tax registered* ili kule wasilipie ile *VAT* ije ilipwe huku inakofikia kwa walaji watu wa mwisho. Iondokane na kufanya *double taxation* kwa upande wa *VAT* ni tatizo toka bajeti iliyopitishwa 2016/17 mpaka dakika hii tunapitisha 2017/18 kero hiyo ipo badi haijaondoka.

Mhe. Waziri nakuomba sana najua nakuamini mia juu ya mia sina mashaka na wewe ningekuomba sana uzungumze ili hizi kero ndogo ndogo zinazowakabili wafanyabiashara wetu ziweze kuondoka.

Nikienda mbele nakuta vipaumbele vya bajeti kuimarisha ubora wa huduma ibara ya 61 zikiwemo Elimu, Afya. Nilipata wasi wasi wakati napitia hivi vitabu kwa sababu hapa viko vitabu viwili 2016/17 na 2017/2018. Kuna baadhi ya *data* naona kama hazioani haziendani sambamba. Naomba pengine niseme *data* zenyewe kama mbili tatu kwenye suala zima ya hii hii biashara ya ndani, biashara ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar naomba ninukuu;

"Kutoka thamani ya bilioni tisini na nne nukta saba mwaka 2015 hichi kitabu ni cha 2017/18 ina hesabu ya bilioni tisini na nne nukta saba. Lakini ukienda katika kitabu chako hicho hicho cha 2016/17 mwaka ule ule unazo bilioni sabini na tatu nukta nane". Nitaomba hapo kidogo nifahamishwe mwaka ule ule huku kwenye kitabu chako cha 2017/18 inasemaa umefanya biashara ya bilioni tisini na nne nukta saba, lakini huku mwaka ule ule umefanya biashara ya bilioni sabini na tatu nukta nane. Hapa kidogo mimi sijafahamu naona kama nimechanganyikiwa sijaifahamu. Kwa hivyo, kidogo utakapokuja najua sina mashaka utanijibu tu najua nakuamini wala sina mashaka tafauti kama wale wenzetu tuliona juzi wanasema kwamba Ndalichako afanye kazi yake, wewe humo katika kundi ile.

Mheshimiwa nikiendelea mbele niende katika suala zima la uwekezaji binafsi nakwenda kwenye suala la ajira. Katika kitabu hicho hicho chako wewe Mhe. Waziri cha Bajeti 2017/18 naomba kunukuu hapa kidogo nisiende mbali sana niseme kwamba:

"Idadi ya ajira zilizozalishwa katika mwaka 2016 zimepungua kutoka ajira 1,597 mwaka 2015". Lakini ukienda katika kitabu chako wewe mwaka jana ulichopitisha hapa ulitwambiwa ajira ile imepungua kutoka ajira 1515, napata wasi wasi kidogo nikisema neno kwamba nichukuliwe wala nisikuliwe vibaya wala nisihukumiwe kwa lugha hii lakini ndio lugha yenyewe. Hapajakuwa na umakini katika kuziweka hizi *data* nitakuwa sijakosea.

Naomba sana nisielewee vibaya katika lugha hiyo kwa sababu sina lugha nyengine ya kutengeneza zaidi ili ikawa nikisema uzembe nimetukana zaidi. Kwa hivyo, nimetumia hapajakuwa na umakini wa kutosha katika suala hili la hizi *data*. Ningeomba tu Mheshimiwa laa kama mimi nimekosea vile vile niko tayari kuja kurekebishwa katika suala hilo.

Lakini vile vile nikiendelea mbele katika hayo hayo maendeleo ya uchumi tunakuta kwa mfano maendeleo ya uchumi hapa kwenye mwaka wa fedha 2016/2017 kwenye suala zima la kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi, katika kitabu chako naomba ninukuu tena Mhe. Spika, kwamba walioandikishwa inasema. "Wanafunzi walioandikishwa katika skuli za msingi na binafsi kutoka 2,052,938 mwaka 2014 hadi kufikia 2,061,212 mwaka 2015".

Lakini nikichukua kitabu chako wewe wewe ulichokuja nacho hapa hapa katika mwaka ule ule ongezeko la wanafunzi walioandikishwa katika Skuli za Serikali kutoka wanafunzi 36,608 mwaka 2015 hadi wanafunzi 45,394 mwaka 2016 lakini hapa 2015 napo vile vile nataka ufafanuzi juu ya suala hili la wanafunzi, kwa sababu linazungumzwa kwamba ukuwaji wa uchumi. Sasa lazima nyanja zote hizi uzikamate ili kuweza kuona namna gani tunakuza uchumi wetu.

Lakini vile vile katika hilo hilo tunakwenda katika suala zima la kuimarika kwa utoaji wa huduma kwa madaktari, nasoma kitabu cha 2017/2018 kuimarika kwa utoaji wa huduma katika sekta ya afya kwa kuongezeka kwa madaktari kutoka 110 mwaka 2015 kitabu cha kwako Mhe. Waziri hadi madaktari 151 mwaka 2016, hichi kitabu cha 2017 ambayo ndio hii bajeti yetu hii mpya. Lakini nikienda katika kitabu chako wewe katika mwaka ule ule niliozungumza kuimarika kwa utoaji wa huduma ya sekta ya afya kuongezeka kwa madaktari kufikia 155 mwaka 2015 kutoka madaktari 148. Sasa bado hizi *data* hazijakaa sawa kabisa kwa mujibu wa maelezo ya vitabu viwili. Kwa sababu tunachangia bajeti tulinganishe hivi vitabu vyote vinasemaje cha mwaka huu kiko vipi na mwaka jana kiko vipi nafikiri pale ndio unapata hoja ya kujenga kulikoni.

Lakini hata katika suala zima la wauguzi liko vizuri halina shaka imeajiriwa vizuri na nimeona wako wale wale 1,089 mwaka 2015 naipongeza. Nilitaka niseme hayo kidogo katika hivi vitabu lakini wakati naendelea mbele vile vile Mhe. Waziri Zanzibar tunajijua namna gani watu wetu uwezo wao kumekuwa na changamoto mbali mbali katika wafanya biashara wetu, ni ukweli usio fichika kwamba nitaizungumzia Benki ya *NBC* ambayo benki hii najua iko chini Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wana *percent* yao pale na ile nyengine anayo ASAS ya South Africa imeleta usumbufu mkubwa sana hata

kuwapatia watu maradhi yasiyokuwepo, wengine wamethubutu kuwaua kwa wizi au upotevu uliofanywa na watendaji wa benki ile.

Mhe. Waziri najua hilo unalifahamu na kama hufahamu chukua kutoka kwangu mimi kuna upotevu wa fedha nyingi sana za wafanyabiashara wetu katika benki ya *NBC*, imepelekea kusimamishwa baadhi ya watu lakini bado wale watu wenye fedha zao pale bado hawajapata ufafanuzi wa malipo, ukiwa kama Waziri wa fedha wa nchi hii nakuomba sana Mheshimiwa utoe kauli juu ya kadhia ya wale watu wote waliodhulumika na wizi uliofanyika kwenye benki ya *NBC* wale watu wetu wanapata vipi kurudishiwa pesa zao.

Tunafahamu kipindi kama hichi cha Mwezi mtukufu wa Ramadhani mpaka sikukuu huna cha kutwambia kitu Wazanzibari kwenye kipindi hichi, leo hii mtu anakwenda kutoa fedha zake anaambiwa kwenye *account* hamna fedha lakini *slip* za kuingizia akitaka *bank statement* anapewa *amount* kadhaa imo ndani ya *account* yako. Mhe. Waziri jangamoyo kubwa sana katika benki ya *NBC* imesababisha hata kupoteza maisha kwa watu nina ushahidi wa kutosha, nina rafiki yangu wa karibu zaidi katika benki ile baada ya kwenda Benki kukuta ile hali alianguka ndio chanzo cha kupata *stroke* mpaka kupoteza maisha kwa mshutko jinsi pesa zake zilivyokuwa nyingi anakwenda pale anaambiwa pesa hamna.

Mhe. Waziri najua katika hilo linajulikana, lakini limefinywa finywa tu halizungumzi, lakini madhali nimelizungumza hapa watu wamesikia serikali imetambua nitaomba jibu la msingi ili wale watu wananufaika vipi na zile fedha zao ambazo walizoziweka kule. Sio benki ya *NBC* hata kuna benki ya *FME* benki ile imefungwa kutokana na sababu mbali mbali wanazozijua wao wenyewe.

Lakini *still* watu wanapesa zao pale kipindi hichi ni lini serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar angalau itasimamia wale watu wenye akiba zao pale waweze kuzipata hatujui kama pesa zitalipwa halafu uzuri wenyewe ile benki haijafililisika imefungwa tu kutoka na miundo mbinu yao na namna gani ilivyofanyika kuna watu wana mpaka *point 2 billion* ziko pale. Sasa ukiwaambia kwamba sheria ya benki huwa haulipwi zaidi bilioni mia moja na kumi na namna gani unawatia simanzi wale watu wenye pesa zao pale, ningeomba nipate maelezo mazuri kuhusu kadhia hyo ambayo iliyothibitika.

Mwahali mwengine kote Mhe. Waziri iko vizuri kama nimevyokuambia kwamba maongezi yaliyozungunzwa hapa au yaliomo kwenye kitabu hichi takribani ni yale yale yote yaliyozungumzwa kwenye wizara zote ambazo tumeshazichangia.

Nilitaka niseme hayo machache tu ili nisipoteze muda naunga mkono hoja kwa sababu huku nyumba nimeshazungumza katika wizara zile au taasisi za serikali nitakuwa mkosefu wa akili au nikisema kwamba hii bajeti siiungi mkono. Itakuwa si vyema naunga mkono hoja lakini naomba tu Mhe. Waziri utakapokuja uje na majibu mazuri katika hii kadhia yangu. Ahsante sana Mhe. Spika, kwa fursa hiyo. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Abdalla Maulid Diwani, ahsante kwa muda uliotumia vile vile naomba sasa nimwite Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini atafuatiwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa na Mhe. Omar Seif Abeid ajiandae.

Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyowasilishwa kwa ufasaha na ukakamavu kabisa wa Mhe. Waziri wa Fedha Dr. Khalid Salum Mohamed.

Nampongeza sasa yeye kwa hotuba zote mbili ya Mipango pamoja na ile ya Mapato na Matumizi. Kwa kweli kama walivyosema wenzangu hotuba hizi mbili zimetuomesha muelekeo wetu na hasa imetuonesha tulikotoka kimapato tukoje na kimipango tukoje na hasa napongeza sana Mipango mizuri ambayo serikali imeandaa.

Naomba kwa mintarafu hiyo nimpongeze sana Kiongozi wetu Mkuu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi...

Mhe. Spika: Samahani Dr Mwinyihaji Makame kabla hujaanza naomba nimpishe Mwenyekiti halafu baada ya hapo utaendelea. Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa, tunaendelea.

Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame Mwadini: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na ninakupongeza kwa kuchukua kiti. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naendelea kwa kumpongeza jemedari wetu mkuu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia vyema sera zetu za kiuchumi na kuendelea pale ambapo awamu nyengine zilianza kwa hatu ambali mbali. Kwa kweli tulipofikia hasa suala la kuweza kulipa mishahara wetu wenyewe tena kwa wakati, tena sio mishahara maana yake kidogo, lakini mishahara ambayo imetukuka.

Mhe. Mwenyekiti, leo tunaambiwa mishahara iko to the tune of shilingi bilioni 325.9 kwa mwaka huu wa 2017/18, sawa na asilimia 48.2 ya makadirio ya mapato ya ndani. Hilo Mhe. Mwenyekiti sio suala dogo ni suala zito na kubwa kabisa kuweza kukidhi mishara wenyewe tena kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, niliona kwenye mitandao Rais Kenyata wa Kenya akijisifu kwamba katika nchi za Afrika ya Mashariki na Kati, yeye tu katika *Region* hii ndiye anaweza kulipa mishahara bila ya msaada mwengine. Tunamwambia aje na Zanzibar, tumeweza kulipa wenyewe bila ya kumtegemea mtu kwa suala hilo, na sasa *OC* tunalipa wenyewe na tunakwenda kwenye *Development Budget* tuweze kulipa wenyewe. Hilo Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana jemedari wetu kwa kuendeleza na kusimamia sera zetu vyema. Tunasema yeye ndio kapokea kijiti kwa Rais wa Awamu ya Sita, Awamu ya Tano, Awamu ya Nne, Awamu ya Tatu na wote walianza kwa viwango mbali mbali. Kwa hivyo, nampongeza sana yeye kwa kuendeleza kusimamia vyema na kuweza kwenda zaidi pale ambapo walianzisha wenzake.

Mhe. Mwenyekiti, Dk. Khalid Salum Mohamed alizungumza vizuri Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, ni lazima tujivunie tulipo na tunachovuna sasa. Lakini nataka nimuombe sana wazungu wanasema *acknowledge*, yaani atambuwe juhudi za nyuma zilizopita, sera za nyuma ambazo ziliwekwa. Nimekuja na kitabu cha bajeti cha aliyekuwa Waziri wa Fedha na ni jemedari yupo hapa hapa, bahati mbaya leo hayupo cha mwaka 1995/1996 Mhe. Amina Salum Ali, kitabu chake cha bajeti hiki anazungumza kupendekeza kuundwa kwa Bodi ya Mapato *Revenue Board* ili ishauri na isimamie ipasavyo sera za mapato, taratibu za ukusanyaji wa mapato, pamoja na kuishauri serikali juu ya mambo ya kodi na mengineyo. Wakati huo ofisi maalum ya kodi ya ndani yaani *Inland Revenue* ilianzishwa ili kuwarahisishia walipa kodi kulipa kodi moja kwa moja katika ofisi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, niliona ninukuu hotuba hii ya bajeti ili kuonesha tulipotoka, na wakati kwa mwaka huo, naomba kunukuu tena kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, kwamba serikali iliendelea kutafuta mbinu za kuongeza mapato kwa kuweka mkakati wa kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kwa njia ya kupanua vianzio vya mapato vya hapa ndani. Baadhi ya sheria za viwango vya kodi vilirekebishwa ili vilingane na wakati, usimamizi na mapato ya Forodha kwa bidhaa zilizoimarishwa. Mapato kwa wakati huo yaliongezeka kutoka shilingi 982.5 milioni, hadi shilingi 3,991 milioni kwa mwaka 1994/1995. Leo Mhe. Mwenyekiti, tunazungumza bajeti ya mapato ya shilingi trilioni kwa miaka 10 iliyopita.

Mhe. Mwenyekiti, tunapongeza sana. Ninachotaka kusisitiza ni kwamba hili zoezi la kuimarisha na kuboresha vianzio vya kuendeleza vya usimamizi ni endelevu, *sustainable development*. Tunapozungumza maendeleo endelevu ndio haya, unaendeleza pale ambapo mwenzio ameanza. Kwa hivyo, mimi namshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, naishukuru sana bodi ya mapato Zanzibar, kwa kweli misingi ya zile sera zetu kwa kuziendeleza na kuona wapi *bolt* imeregea wakakaza, kuona wapi watu kidogo hawafanyi kazi wakaweka sawa. Hilo nalipongeza sana na kwa kweli nilitaka niitaje ile timu ya wale *founders* wenyewe pioneers wa *Revenue Board* wakati huo na sio vibaya kuwataja haraka haraka.

Mwenyekiti wake wa kwanza alikuwa ndugu Othman Masoud na katibu wake alikuwa ndugu Assa, kuna wajumbe kabambe wenye timu hiyo Katibu Mkuu wa Fedha hivi sasa ndugu Khamis Mussa, wakati huo pia alikuwemo Dk. Mwinyihaji Makame, wakati huo pia alikuwemo ndugu Omar Sheha Mussa, alikuwemo ndugu Omar Yussuf Mzee, alikuwemo Jaji Mkuu wa Zanzibar hivi sasa wakati huo bwana Makungu na yeye alikuwa mjumbe. Nani nimemsahau. Chini ya mwenyewe Kamishna marehemu bwana Nassor Khatib.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hiyo timu itizame ilikuwaje. Ndio wakaweka ile *symbol* yao chungu, kupokea yale mapato kwa chungu, yaani wameyakusanya yale mapato. Mimi nampongeza sana Dk. Khalid kwa kuendeleza pale tulipotoka hizi *brains* zipo na anazitumia vizuri. Katibu Mkuu wake wa Fedha yupo ndugu Assa upande mwengine yupo, bwana Makungu yupo. Kwa hivyo, hii ni *team work* na hili ni somo zuri sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba tufanye kazi hasa suala la mapato linamgusa kila mmoja wetu, kila

mmoja wetu tuhakikishe haya maendeleo ya mishahara tunawalipa wazee wetu leo, tunaweza kumudu wenyewe *OC* zetu ni mambo ya msingi na mambo ya kupigiwa mfano.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee kwengine haraka haraka. Naomba sana Alhamdulillah tumeweza sasa kuongeza ajira. Kwenye ukurasa wa 29 amezungumzia suala la wataalamu, katika fani kuna upungufu, kwenye afya, kilimo, viwanda na mafuta na gesi. Naomba kusisitiza Mhe. Mwenyekiti, tuongeze ajira lakini tuangalie suala la kweli wataalamu gani wanahitajika mahala gani. Tulipofanya utafiti mdogo kulikuwa na *redundancy* katika maofisi yetu. Kuna kazi ambazo badala ya kufanya mtu mmoja wanafanya watu 11, wengine hawana kazi. Sasa *wage bill* yetu imekuwa kubwa kwa wengine kwa kweli hawastahiki wawepo. Tusioneane haya. Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wamezungumza kwamba tusioneane haya huo ndio ukweli, haidhuru tunaona pana *vacancy* pana uwazi pale nafasi ipatikana, lakini kweli yule anakuja kufanya kazi gani.

Sasa hilo naomba Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu kwa nia safi kabisa, kama tunavyoongeza ajira mpya basi tuangalie kweli tunastahiki. Lakini na hao wataalamu tunaowaajiri kweli vyeti vyao ni vya uhakika. Kwa kweli siku hizi kidogo mambo yanatisha, *forgery* zimekuwa kubwa sana, hilo naomba nalo tuliangalie. Matokeo yake utaona kijana anaajiriwa ana *degree* lakini hawezi ku-*perform*. Sasa matokeo yake kazi ya mtu mmoja, maafisa wengi wanasikitika wanafanya watu 11.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee kwenye suala la *ZIPA*. Tunawashukuru sana *ZIPA* wamefanyakazi nzuri sana na wanaendelea kufanya. Kwa mwaka 2016 *budget speech* ya Mhe. Waziri imetuambia kwamba waliidhinisha miradi 16 yenye thamani ya shilingi dola za Kimarekani 150 milioni. Kwa mwaka 2015 waliidhinisha miradi 36, 16,16. Lakini 2015 miradi 36 yenye thamani ya shilingi 346. 8 bilioni ni dola za Kimarekani hizo, hii ni sawa na punguzo la asilimia 56.6. Mhe. Mwenyekiti, nataka kufahamu tu, kwa nini mwaka huu 2016 uliopita miradi imepungua ukilinganisha na mwaka 2015. Ingekuwa vyema Mhe. Waziri atuambie ni nini sababu iliyosababisha *ZIPA* kuwa na miradi michache.

Lakini hapo hapo Mhe. Mwenyekiti, kwenye *ZIPA* tumepata habari kwamba kuna miradi ya *Tour Guide* ambayo kikatiba yetu au kitaratibu zetu ile miradi ifanywe na wazalendo Wazanziabri. Lakini kuna wageni wana makampuni ya *Tour Guide* na wamo ndani kwenye *Board of Directors* ama uongozo wa *ZIPA*, nasikia wamechukuliwa na wao mule kama washauri, lakini wana miradi yao na ni wageni. Sasa hii wanatunyima fursa wazalendo kwa miradi ile. Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, hili nalo tulitizame kama ni kweli tulirekebishe.

Mhe. Mwenyekiti, tupo kwenye *ZIPA* naomba niende moja kwa moja nyumbani. Mradi wetu wa Mji Mpya wa Fumba. Tunaishukuru sana serikali yetu kwa mradi ule, kwa kweli kutafumbua kule sio Fumba tena sasa hivi kutafumbuka, na hali tushaiona. Sasa kubwa ambalo namuomba sana Mhe. Waziri, sikumsikia kuzungumza hatma ya wanavijiji wa vijiji vya Fumba, Bweleo, Dimani na Nyamanzi ambao wao wame- *sacrifice* wamekubali kuachia ardhi zao kwa maendeleo ya nchi. Sasa ile ardhi iliyobaki waruhusiwe

kuiendeleza, wako *at stern still* sasa hivi hawajui wafanye nini, wanaambiwa wasubiri mpaka serikali ije iwapimie, wakati unakwenda na miradi inakwenda kila mmoja anawania maisha. Zile ardhi walizo-*sacrifice* wame-*sacrifice*, ambalo ndio wanalima walikuwa wanavua bandari zao na walikuwa na maendeleo mengine. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri hili nalo tulitafutie kauli upesi upesi ili waruhusiwe wananchi wa vijiji vile waendelee na shughuli zao za uvuvi, maendeleo na mengineyo. Mhe. Mwenyekiti, naupongeza sana mradi ule ni mkubwa na utatusaidia kiuchumi.

Vile vile niendelee hapo hapo *ZIPA* kuhusu suala la Maruhubi. Tunaishukuru serikali yetu kwa wazo la Bandari mpya ya Mpigaduri, tunashukuru sana kwa bandari hiyo mpya. Nimesoma humu kwamba tayari *Feasibility Study* imeshafanywa na upembuzi mwengine wa kimazingira unaendelea. Lakini nataka kujiuliza kuna mwekezaji mkubwa tu pale Maruhubi ana *Five Stars Hotel,* na katanua ile hoteli yake mpaka baharini.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alikwenda kuitikia wito wa wananchi wa Mtoni, kwamba wimbi sasa limekwenda upande wao na nafikiri kwa muono wao ile taathira ya lile tuta lililokwenda kule. Sasa nauliza tu Mhe. Waziri aje kutusaidia, nataka atutowe wasi wasi kwamba je, hii Bandari yetu ya Mpigaduri haitoingiliana na mradi ule, haitotuathiri kwa sababu tayari keshaji-*commit*, mkataba umeshasainiwa. Lakini kuna mwekezaji mkubwa tu ambaye tunamshukuru sana, lakini je haitoingiliana. Suala hili naomba bora tuwahi mapema kama kuna tatizo basi tuliweke sawa kabla hatujafika mbali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee kwa haraka haraka katika suala jengine ambalo nilihisi nilizungumze ni suala la pato la taifa. Nakwenda nikirudi mtanivumilia. Mhe. Mwenyekiti, tumeambiwa kwamba kwa mwaka 2015 lilikuwa kwa asilimia 6.5 na mwaka 2016 asilimia 6.8 na pato la taifa limefikia 2,628 bilioni kwa bei za mwaka 2016. Kilimo cha mazao, hoteli, mikahawa na ujenzi ndio sekta zilizoongoza kwa mchango mkubwa katika pato la taifa.

Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti. Lakini najiuliza kwa upande wa mazao kilimo kikoje, je kilimo chetu kina tija. Nimekutana na maafisa kilimo wawili watatu wanalalamika sana kwamba kidogo ule uendeshaji wa kilimo kama Idara ya Kilimo haiendi inavyopaswa na viwanda vyetu tunavitegemea hasa vitokane na kilimo (*agro processing)* hivyo ndio viwanda ambavyo sisi wenyewe lazima tuvikuze. Lakini kama kilimo hatukiangalii ipasavyo basi Mhe. Mwenyekiti tutakwama.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nahisi tulitizame ni suala la masoko. Tunaambiwa viwanda havijafanikiwa Zanzibar, lakini tujiulize kwa nini havijafanikiwa. Mimi mtizamo wangu Mhe. Mwenyekiti, soko letu la viwanda bado ni dogo. Juzi alizungumza Mhe. Diwani hapa kuhusu utaratibu. Kupeleka bidhaa Bara tunavikwazo vingi sana, lakini soko kuna la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, kuna la *SADC* liwe huru sasa. Sasa ikiwa tunabana wenzetu, na kweli *Customs Officers* pale wanakuambia Bara kwa nini hicho kiwanda hamkileti huku na viwanda vingi vimeondoka Unguja vimekwenda kufunguliwa Bara, au wengine wamekwenda Mozambique. Bwana Bakharesa kapeleka Mozambique na chengine. Sasa suala la *marketing* Mhe.

Mwenyekiti, nafikiri ni sekta moja wapo ambayo inaathiri sana kuweka kiwanda vyenye viwango vikubwa Zanzibar. Wengi wanataka kuzalisha, wanataka kuweka lakini suala la masoko ni lazima tulifanyie kazi ipasavyo.

Deni la *TANESCO* Mhe. Mwenyekiti, nakwenda haraka haraka. Kwa kweli naipongeza sana serikali yetu kwa mkakati mzuri tuliojiwekea kulimaliza hili deni la *TANESCO*. Kwa kweli ni vyema kwanza kuli-*establish* lile deni lenyewe la shilingi 65,656 bilioni kwamba tumesema Juni mwakani 2018 tunalimaliza. Nawapa hongera sana serikali kwa kupanga hilo na naamini *In Shaa Allah* tutafanikiwa. Lakini sasa ukusanyaji wa *ZECO* wenyewe nao unaridhisha, bado kuna mita nyingi za kizamani za *bill* watu hawapelekewi ipasavyo, wengine makisio tu, hebu tu-*invest* kidogo mji mzima, nchi nzima wapewe *TUKUZA* mtu unakusanya kwa uhakika. Unauhakika mtu mwenyewe halipi basi halipi umeme, suala hili namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha hata kama mtawakopesha *ZECO*, basi tuwakopeshe watafute mita za TUKUZA tufunge tukusanye mapato ipasavyo. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema hili litatusaidia kwa haraka sana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie naona unaniangalie, nimalizie la mwisho kabisa katika suala zima la utendaji wetu kwa ujumla katika serikali. Mimi nimefanya utafiti, mheshimiwa kumradhi. Kaa wewe saa mbili katika ofisi tatu tu, basi kama utapata watu 10 walioingia saa mbili za asubuhi mule bahati yako. Kwanza nakaa Mazizini mimi hapa, ipo Ofisi ya Maalim Haroun pale. Mimi hukaa pale nikafanya mazoezi kama utapata watu 10 walioingia pale saa mbili basi ushukuru. Sasa mcheza kwao hutunzwa, Mhe. Rais keshajitahidi keshapandisha mishahara, lakini utendaji uko wapi, lazima hili Mhe. Mwenyekiti tulisimamie ipasavyo, lazima kila mmoja wetu afanye kazi na atoke jasho achume kila alichokipata, kama utendaji hakuna, basi narudia *point* yangu tutawaajiri watu wengi tutawaweka lakini *efficiency* haipo na hatutofanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kukushukuru sana na ninasema kwa kweli ninamtakia kila la heri Dk. Khalid, namtakia heri kwa bajeti nzuri ya Kimapinduzi na ninamuomba sana Mhe. Rais wetu na yeye nimpongeze kwa imani yake anayoionesha na suala zima la amani na utulivu ndio litaleta yote hayo. Kwa hivyo, sote tushikamane kujenga umoja, amani na utulivu katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono bajeti *speech* hii kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mhe. Miraji Khamis Mussa na baadae Mhe. Bi Panya Ali Abdalla ajitayarishe. Mhe. Miraji Khamis karibu sana.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba hii ya Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali, kwa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2017/2018, lakini pia imewasilishwa na hali ya uchumi wa mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2017/2018 na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi ya mwaka 2017/2018. Vitabu vyote hivi vina lengo na dhamira moja ya kusogeza nchi yetu mbele.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango Dk. Khalid, lakini pia niwapongeze watendaji wakuu Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Katibu Mtendaji na Makamishna wote na watendaji waliobakia wa Wizara hii wametuletea vitabu vyenye mwelekeo mzuri na mpango mzuri wa Serikali yetu, naomba niwapongeze sana katika maeneo haya na Mwenyezi Mungu awajaalie waende vizuri kama ambavyo wanaendelea sasa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye aya ya 61 ya kitabu hichi cha Makadirio na Mapato ya Matumizi ambayo imezungumzia vipaumbele vya kitaifa, kwanza naomba niipongeze Serikali kwa kuainisha vipaumbele vyake vya kitaifa kwa ujumla wake vimeashiria na vimetuonyesha mwenendo mzuri na hatua nzuri ya mwelekeo wa Serikali, hapa niombe sana kuipongeza lakini nianze na kile kipaumbele cha kuimarisha ubora wa huduma za kijamii ikiwemo Elimu, Afya, Makaazi na upatikanaji wa Maji safi na Salama. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili baada ya pongezi zile lakini naomba niekee tu mchango wangu kwa kuweza kuishauri Serikali zaidi kwa sababu tumeona.

Naomba nianze katika eneo la makaazi katika kipaumbele hichi kinachozungumzia eneo hili la makaazi kimetengewa fedha na najua mambo yatakwenda vizuri, lakini mara nyingi ukiangalia ule mpango mkuu ule hasa wa Wizara husika mara nyingi unatupeleka katika ukataji wa viwanja kimoja kimoja sasa ukiangalia tunaendelea kukata viwanja lakini maeneo tunayoyakata viwanja baadae yanaweza kuwa pia ni maeneo ambayo tunaweza tukayahitaji kwa hatua nyengine, tunaangalia *plan* ziliopo unakuta ule upangaji wa miji unaambiwa tu kuna Ng'ambo tuitakayo. Lakini ukija ukiuliza kitengo cha *plan* kimoja ile shamba tuitakayo wanaipata lini hamna wananchi kule wanakata viwanja na wanajenga kiholela sana.

Sasa ningeomba tu katika mpango huu ambao Serikali inapanga basi uwe mpango wa nchi nzima, tusi-*focus* mjini tu baadae tunawaachia wananchi vijijini wanajenga sasa tukija tukifika huko yale maeneo muhimu ya kilimo tunakuwa tumeyatumia kwa matumizi yawezekana yakawa tunaweza kuyadhibiti kwa wakti muafaka na wakati wenyewe ndio huu, kwa hivyo tunapofanya huu mpango basi uwe mpango wa nchi nzima tukigawa viwanja maana yake viwanja vile viwe vina maendeleo ya sasa, tukiangalia nchi za wenzetu wanatumia eneo dogo katika kujenga lakini wanabakisha maeneo yao ya kilimo wanayapima kabisa.

Lakini leo sisi tukirudi huku katika mpango wetu yale maaneo ya kilimo tunayatambua tu lakini hatujayapima na tukayatambua ipasavyo lakini na wananchi tukawaelekeza kunako maeneo haya Serikali yote nzima pamoja na zile Serikali za Mitaa yakaweza kuyasimamia ili kulinda ule mpango mkuu wa Serikali, katika matumizi ya ardhi katika maeneo hayo, kwa hivyo leo utakuta kuna muingiliano humu huko leo tunakwenda juzi tu tumeanza kuratibu kuona tunakwenda katika ng'ambo tuitakayo Serikali imeandaa mpango mzuri, kuondoa nyumba zile kujenga nyumba za kisasa ambazo watu wote tunaweza tukawahamisha katika eneo moja. Sasa mpango huu kwa nini usiwe mpango endelevu kwa nchi nzima yako makampuni mengi sana tunaweza tukaingia nayo

mikataba ambayo tunaweza tukaja tukajenga wananchi tukawaingiza pale tukatumia eneo dogo lakini na kodi zile zikaweza kurejesha ujenzi wa nyumba zile.

Kuna ujenzi wa nyumba nafuu lakini leo tunasema tunazijenga Fumba kuna muwekezaji tumempa nyumba ile hata huyo Mjumbe wa Wabaraza la Wawakilishi hawezi kuishi, kwa sababu huduma yake ni kubwa na lengo ni kuwafikia wale wananchi, lakini tuendelee kufanya mpango endelevu wa kuwawezesha wananchi kwa ujumla wake najua ni kazi kubwa lakini tunaweza tukaandaa mpango ambao unaweza ukatufikisha basi tukaweza hasa kudhibiti maeneo ya kilimo na tukiliweza hili hata ulinzi wa wananchi wetu basi pia unaimarika, kwa sababu tunaweka katika eneo moja na huduma zao wanapata kwa pamoja basi nchi inaenda vizuri. Sasa mimi sina tatizo sana lakini nasema nishauri katika eneo hilo ili tutenge maeneo yote kwa ujumla wake tusipime tu tukaiangalia ng'ambo tuitakayo basi na ile shamba tuitakayo ianze sasa, kwa sababu kitengo hichi cha *planning* ni kimoja vio vitengo viwili. Kwa hivyo tukianza mjini huku hata tukifika shamba yale maeneo ambayo tutakuja kuangalia kwa kilimo yashapotea, lakini niende tu katika vipaumbele hivyo hivyo katika sekta ya kilimo ambayo nayo ina uwezo wa kutusaidia katika ukuwaji wa uchumi wetu.

Niipongeze tena hapa Serikali katika ule mpango wake ambao mbele huko tumeonyeshwa kuna fedha ambazo tunaweza tukazipata kwenda kusaidia kilimo cha umwagiliaji, kupitia pesa zile za *Exim Bank*, naipongeza Serikali katika eneo hili lakini niiombe tu kwenye eneo hili tuharakishe. Kwa sababu hapa tukiweza kuongeza kilimo katika nchi yetu tutapunguza uagiziaji wa chakula na tukipunguza uagiziaji wa chakula maana yake ile *balance* ya *Foreign Currency* inabaki, kwa hivyo sio kila siku sisi tunaagiza tunaondoa pesa tunatoa nje lakini sisi wenyewe tukiweza kujipanga vizuri katika eneo hili la kilimo tutaacha uagiziaji huo.

Niende tu haraka haraka maana muda unaweza kuwa haunitoshi katika eneo jengine la vipaumbele kuna hatua nzuri tu ya kifungu (e) cha kushajihisha zaidi uwekezaji katika viwanda vidogo vidogo, mimi niipongeze tena Serikali katika azma hii lakini naomba nirejee. Ukizunguka Zanzibar unakuta maeneo yote tumezungurukwa na bahari, lakini hatujaweka mkazo kuelekea kwenye uvuvi na kutengeneza kiwanda cha samaki. Kwa hivyo tukifika katika hatua hii tukijenga viwanda vya samaki au tukianza na kimoja tutakuwa tuna uwezo sisi sasa kiwanda kile kuweza kuvua samaki wetu tuka-*process* baadae tukauza tunakuza uchumi, lakini leo tuna eneo kubwa tunaruhusu kuja meli mbali mbali tunapata pesa ndogo wanachukua samaki wakati mwengine wanakwenda kufanya *process* samaki hao hao tunaletewa kwa makontena hao hao.

Sasa kwa nini sisi tusizidishe kasi yetu ya kweda tuka- *focus* katika kutengeneza kiwanda cha samaki ili eneo hili tu-*cover* wenyewe ule uchumi maana yake tukaubakisha lakini hatua ya kuondoa samaki wetu bila ya kujua, maana yake sasa hivi tunatoa vibali samaki wanakuja kuondoshwa ndani ya bahari yetu tualipwa kodi ndogo tu ukiangalia mapato tunayoyapata kama tutajenga kiwanda hasa cha samaki tuka-*procces* wenyewe tukaweza ku-*export* basi tutapata pesa zaidi na tutaweza pia ku-*control* ule uchumi wetu katika eneo hilo la uvuvi wa bahari kuu. Sasa naomba sana Mhe. Waziri katika eneo hilo la ujenzi wa viwanda vidogo vidogo najua maeneo mengi tutaimarisha lakini kwenye uvuvi

huu tuone ule uharaka wa ujenzi wa miundombu hii ya kiwanda cha Samaki tuendelee nao.

Lakini kuna eneo juzi nililichangia katika kusaidia ukuwaji wa uchumi na naomba hili Mhe. Waziri tuliangalie kwa umakini mkubwa eneo lile la karibuni sisi tunasema tumepitisha sheria ya mafuta na gesi, na tunakokwenda tutafika pahala maana yake aidha tutachimba hayo mafuta Mwenyezi Mungu atujaalie tuyapate lakini hata kama hatukufanikiwa lakini nchi yetu inajipangaje katika angalau kuona tunaondoka katika ile *Theory* ya *Comparative Advantage* kuingia katika *Theory* ya *Michael Porter* ambayo inatupeleka katika *Problem Fixed Approach*, tuwe hatuna mafuta lakini leo ukijenga *Refinery* ya usafishaji wa mafuta maana yake wewe utanunua *crued Oil* utaleta nchini kwako utaisafisha maana yale lami utapata mle, mafuta mengine ya aina mbali mbali utapata mle na sisi tutaweza kuziuzia nchi jirani. Sasa huo mpango tuingize katika mipango yetu ya kitaifa hata kama hatujachimba lakini tuweke na hilo.

Ukiangalia nchi ya Korea mafuta lakini ndio nchi ambayo imejenga mtambo wenye ubora kokote duniani, wanachukua huku na sasa hawaagizi mafuta unakuta watu hao katika utaratibu hawaagizi lami sasa kwa nini sisi tusielekee huko, ukibahatika huku tukizalisha wenyewe tutasafisha ndani ya nchi yetu hatukuzalisha lakini itakuwa mpango wetu ule unandelea. Lakini pia nilizungumzia katika mipango ya Serikali tukazungumzia suala la *study* iliyopo ya masuala ya umeme niipongeze Serikali tunaambiwa tu mwaka huu au mwishoni mwa mwaka au mwanzoni mwa mwaka ujao watakamilisha huo mpango wa utafiti na upembuzi yakinifu kuhusu umeme gani tunataka tuzalishe hapa, hapo serikali naipongeza lakini hatua hii iende na kasi nzuri.

Maana tunaweza tukasema tunakwenda kufanya *Study* hiyo lakini unakuja kuambiwa hiyo sera tu yamabadiliko ya matumizi ya umeme ili tusinunue *TANESCO* ili tuje tuzalishe umeme wetu wenyewe pengine ikaja ikachukua na miaka mitatu mingine, sasa kwa nini vitu hivi wanapenda kusema mipango mizuri lakini utaratibu wa kuviratibu haviendi pamoja ili kuongeza ile kasi ya kuongeza uchumi wetu, maana hapa tutakapoweza kufua umeme sisi tutawarahisishia wananchi wetu kupunguza yale makali ya maisha katika matumizi ya umeme. Lakini tunaweza na sisi tukauza pia *cable* ile ile ambayo inatuletea sisi ile ile tukatua tukawauzia wenzetu, wenzetu wanafua umeme lakini hauwatoshi sasa sisi kwa nini tusiingie katika mpango wa kuonekana huu utasaidia uchumi wa nchi, lakini pia utasaidia kukuza yale maendeleo ya ustawi wa Shirika letu la umeme.

Lakini naomba niende katika aya ya 109, 110, 112 kwa pamoja hizi zilikuwa zinazungumzia yale mashirikiano tunayoyapata katika mashirika mbali mbali katika kusaidia bajeti kuu ya Serikali na eneo hili naomba nipongeze sana, nipongeze kwa mashirika haya umeyaainisha lakini nipongeze Serikali pia kupitia Mhe. Rais, Dkt. Ali Mohammed Shein kwa mashirikiano mazuri katika eneo hili, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais pia.

Lakini kuna eneo pia hapa naomba sana Mhe. Waziri wa Fedha tuliangalie kuna eneo la ushirikiano wa kibiashara katika Afrika ya Mashariki, wenzetu wameandaa vipaumbele

vingi ambavyo wafanya biashara wetu sisi naamini wanavikosa kwa asilimia kubwa sana, katika vipaumbele ambavyo wamevitengeneza kupitia *SADC* kuna vipaumbele ambavyo vimepatikana sasa kupitia ule utatu ule wa *COMESA, SADC* pamoja na *EAC* sasa hapa pana kipengele cha *FTA* ambacho nakizungumzia maeneo haya Mhe. Waziri labda ukija utwambie tunafaidika vipi sisi katika uwekezaji mana ukijikita katika ushirikiano huu wa Kimataifa basi katika uwekezaji unafaidika sasa ukija utwambie tunafaidika vipi katika fursa hii ya makubaliano haya ambayo yamepatikana. Maana leo hii makubaliano yaliyokwisha kukubalika katika *SADC* tayari katika huo utatu niliokwisha kuuzungumza tayari na karibuni tunakwenda katika mashirikiano mapya ambayo yanatupeleka kwenye *AU*. Sasa hebu tuone fursa zipi ambazo tumezipata sisi katika utaratibu mzima wa kuimarisha uchumi wetu katika uwekezaji, lakini fursa wanazozipata wafanyabiashara wetu katika *FTA* hii sasa Mhe. Waziri ukija naomba utuambie ili tuone hatua njema ya Serikali katika kukuza uchumi kupitia kwa wafanya biashara wake.

Lakini nataka niende eno la ukuwaji wa uchumi ambao ulitoka katika asilimia 6.5 kwenda katika asilimia 6.8 naomba na eneo hili pia niipongeze Serikali angalau tumeweza kuongeza kasi ndogo ya ukuwaji, lakini pia tumeweza angalau ku-*balance* hiyo *Situation* ya asilimia ya uchumi ndani ya nch yetu, lakini katika eneo hili naomba pia napo nichangie tu kwa ujumla jumla pamoja na maeneo ambayo naona tunarudi nyuma sana ni ule utaratibu mzima wa ukusanyaji wa kodi, kodi kweli tunaipata na mapato yanaongezeka lakini mfumo hasa wa ukusanyaji wa kodi ndani ya nchi yetu hauko vizuri. Mimi nauchukulia mfano wakati mie niko katika taasisi moja na sipendi kuitaja katika utaratibu mzima wa zile *Property tax* walikuwa wanakusanya kodi za *trading license*, wanakusanya kodi za *Driving License*, lakini anakusanya kodi za *road lincense*.

Taasisi hii ilikuwa ina mfumo niseme si rafiki katika mazingira ya ukusanyaji wa kodi wenzetu wa *ZRB* wakaandaa mfumo angalau wa kuweza kuboresha eneo lile, wameboresha na tumeona jitihada zao mambo yanakwenda vizuri pesa zinapatikana vizuri. Sasa eneo lile ni moja lakini tuna vianzio vingi ambavyo havina mifumo ya ukusanyaji wa kodi na mfumo huu tulikuwa tunategemea kwa ujumla wa Serikali tutaipata kwenye hii *E-government* lakini mpaka sasa hivi leo tunatenga pesa bajeti ijayo tutatenga pesa lakini hatufiki katika matarajio. Lakini katika mfumo ule tumeona kodi zetu zinapatikana zimeondoka katika taasisi fulani tumezisogeza katika taasisi nyengine ambayo imetoa mfumo bora na fedha katika maeneo yale zinapatikana, lakini leo tukiuliza katika mashirika ya Serikali ambayo pia nayo kuna sehemu yanazalisha kodi zetu wana mifumo ambayo inakwenda sambamba kama kasi ya *ZRB* inavyotumia ule uwakala wa kuisaidia Serikali kufanya kazi yake vizuri.

Sasa katika hatua hiyo lini jitihada ile ya Serikali za kuwezesha mifumo hii kabla ule mfumo wa kitaifa ambao hatujaanza kuutumia, maana saa hivi mifumo tunayokwenda nayo fedha nyingi zinapotea. Sasa nataka nikwambie Mhe. Waziri katika utaratibu wa *ZRB* wana mifumo mizuri kodi zinapatikana lakini vipi taasisi nyengine za Serikali hebu ukija twambie utatusaidia vipi katika kuwatengenezea mifumo ambayo itakuwa rafiki katika kusogeza uchumi wa nchi yetu katika ukusanyaji wa mapato vizuri kwa hivyo nakuomba eneo hili…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika mbili zilizobakia.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Hi nina dakika mbili, haya Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba tu Mhe. Waziri wa Fedha katika utaratibu huu mzima wa ukusanyaji wa hizi kodi katika maeneo yote ambayo nimeyataja sina tatizo na *ZRB* na mfumo wake, lakini mifumo mingine katika taasisi nyengine ambazo kodi zetu zinatakiwa zikusanye nini jitihada ya Serikali katika kwenda kuhakikisha na wao wanatoa mfumo endelevu wa kutusaidia sisi. Tujaalie naweka mfano tu kama tuna wakala ambae tumempa utaratibu karibuni wa *ZBS* wanakusanya katika utaratibu ule ule wa percentage wise wao wanachukua hii kiuwakala na hawa wanachukua asilimia fulani na huku asilimia fulani inakuja Serikalini, lakini mfumo bora tumewawekea kile wanachokifanya kinapatikana lakini pia yapo mashirika mengine lakini na huku huku *ZRB* ule mfumo ambao tunakwenda nao katika utaratibu huu wa *E-Government* naomba sana ukamilike ili tuone hawa watu ambao tunawadai kodi zetu leo wanakuja kutulipa kwa makisio wanayoyafanya wenyewe.

Maana sisi tunampelekea makisio anayakataa wakati biashara anafanya mwenyewe wananchi wetu washakwenda kununua vitu washalipa kodi lakini anatukadiria sisi, wakati zile *Transaction* zinatakiwa zote zisomeke anazozifanya lakini na ule uhalisia upatikane, sina tatizo na hatua hiyo lakini hatua tuiboreshe katika kusogeza mbele kasi ya uchumi wetu Mhe. Mwenyekiti, usije ukaniwashia taa tena naomba sana niunge mkono bajeti hii kwa asilima mia moja nasema sina tatizo na bajeti ya Mhe. Waziri, lakini pia katika maeneo hayo niliyomuomba angalau asogezee kasi basi Mwenyezi Mungu amjaalie asimamie vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Miraji na sasa tunamuita Mhe. Bipanya Ali Abdalla na Mhe. Omar Seif Abeid ajitayarishe akifuatiwa na Mhe. Said Omar Said Ahsante Mhe. Bi Panya tafadhali.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti awali ya yote na mimi nishukuwe fursa hii kumshukuru Mwenye ezi Mungu ambaye ametujaalia uhai tukaweza kukutana hapa, lakini pia nichukuwe fursa hii niweze nikushukuru wewe kunipatia na mimi nafasi hii angalau niweze na mimi kuchangia machache katika bajeti yetu hii kuu ambayo ni mtazamo wetu wote uko hapa.

Mhe. Mwenyekiti kwanza nami nianze kwa kumpongeza sana sana sana Mhe. Waziri kwa kazi kubwa na nzuri yeye pamoja na watendaji wake wote wa Wizara hii, tunawatakia kila la kheri na Mwenye ezi Mungu ishallah awape nguvu na uwezo mzuri ili waweze kuiweka nchi yetu hii katika kuiondosha hasa niseme katika bajeti tegemezi na kuiweka katika bajeti itakayoweza kujitegemea wenyewe. *(Makofi)*

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti niseme hilo linawezekana wala si miujiza ni usimamizi mzuri, na ukushanyaji mzuri wa mapato hilo tutaweza kutufikisha kutuondoa katika bajeti tegemezi. Ishallah Mwenye ezi Mungu wenzetu hawa awape nguvu na fikra zaidi na sisi tuko nyuma yao tunawasaidia tutakapoona miyanya inavuja tutaendelea kupiga kelele kusema ili miyanya hiyo izidi kuzimba.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze mchango wangu katika ukurasa wa 18 aya ya 31 ambayo inaelezea Usimamizi wa Uchumi Mkuu, katika kifungu hiki kuna programu ndogo mbili ambazo zinasema “Uchumi Mkuu na Takwimu” na “Uratibu wa Mashirikiano baina ya Sekta za Umma na Sekta binafsi”. Mhe. Mwenyekiti mimi hapa mchango wangu nilikuwa nataka kusisitiza mimi napenda kusisitiza takwimu kwa sababu hapa hii ndo bajeti yetu kuu kabisa ambayo ina mipango yote mikuu ya Serikali ipo hapa, sasa takwimu ni kitu muhimu sana, mimi napenda kusisitiza takwimu kuwa na takwimu zilizosahihi ili takwimu hizo zikipatikana katika usahihi wake zitaweza kusukuma mpango wetu wa Maendeleo wowote ambao tutaupanga utaweza kwenda vizuri. Na utaweza kukwamua ile mchanganyiko wa kuja kuifanya , maana tukiwa hatuna mipango mizuri katika takwimu maana yake tutakuwa na wakati mgumu katika utekelezaji wake, ambacho tulichokipanga tutakishinda kukitekeleza kwamba hatuna takwimu sahihi.

Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti mimi nimuombe Mhe. Waziri na namjua mtu makini sana, anajitahidi kwa kadri ya uwezo wake ishallah nimuombe kwamba uwekaji wa takwimu sahihi ni kitu ambacho kitaweza kuendesha taasisi zetu hizi na kuipeleka Serikali katika Mipango mizuri ya Maendeleo. Mhe. Mwenyekiti nije tena katika ukurasa wa 22 ambapo kuna udhalilishaji wa wanawake na watoto, Mhe. Mwenyekiti nataka niliseme hili kwa upana wake kwa sababu suala hili ndio ambalo sote tunatutikisa sana na niseme hata katika utekelezaji wa majukumu yetu, inawezekana tusiwe tunayafanya vizuri kwa kufikiria hili ambalo linajitokeza la udhalilishaji wa wanawake na watoto. Hata wale wenzetu wanaojikita katika ujasiri amali lakini wakizingatia watoto wao hawako katika usalama mzuri au hapa huo utafutaji wa mapato unakuwa ni mdogo.

Kwa hivyo nikuombe sana Mhe. Waziri suala hili tuweze kulishughulikia kwa umakini wake ili hichi kifaa nia imeshaonekana na naona kipo, lakini kumpata mtalaamu haraka wa kuweze kulishughulikia suala ili tukaona kipimo hichi kinafanya kazi na lile jakaya moyo ambalo linasemwa mimi naona kuna kipindi kinatolewa siku hizi kuna jakaya moyo la kukosekana DNA kwa hiyo lile jakaya moyo niliweze kutuondoka na iweze kupatikana vipimo vya vinasaba ili watu waweze kuwa huru na familia zao, na waweze kujikita katika suala zima la uchumi kujitafutia riski wao lakini, hata kukuza uchumi katika taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti niende tena katika suala zima la afya ambapo hapa sisi tunasema kila siku tuwe na utawala bora. Na utawala bora utapatikana kupitia huduma zetu zikiwa bora, huduma zikiwa bora maana yake utawala bora utaweza kupatikana Mhe. Mwenyekiti niende katika hii Wizara ya Afya, kwanza nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Afya kwa kufanya ziara ya mchtukizo ambayo yeye mwenyewe ameweza kushuhudia yale aliyoyashuhudia. Na hii itamthibitishia sasa kama wawakilishi wanapokuwa wanasema hapa Barazani kuhusu huduma zinazotolewa sasa yeye mwenyewe ataweza kujipanga, na mwenyewe ameshasema kwamba ziara ile itakua endelevu nampongeza sana, kitendo hichi ndicho kitaweza kutupeleka katika huduma bora. Kwa sababu watu wamejiachia sana, sasa leo wakipata kupitiwa kila mara kila mmoja ataweza kusimamia kazi yake na kufanya ule wajibu wake, na akifanya hivyo atakuwa tayari anaipatia sifa nchi yake lakini atapatia sifa viongozi wake. *(Makofi)*

Kwa hiyo tukijikita katika suala zima hilo la afya, katika kufanya ziara za mshtukizo ambazo tunajua changamoto nyingi zinawakuta wananchi wetu pale tukiona wananchi wetu wanaweza kupata huduma bora, maana yake hata Serikali yenyewe itakuwa nayo inatembea kifua mbele katika kujinadi, kwamba tayari tuna huduma bora kwa wananchi wetu na wananchi watakuwa wanafaidika kupitia matunda yao ya Mapinduzi. Mhe. Mwenyekiti niende tena katika mchango wangu, niende tena katika suala zima ambalo tunasema hapa tuko katika mipango mikuu ya Serikali. Mhe. Mwenyekiti mimi niiombe sana Serikali niiombe, Serikali kwa nataka kusema kumbukumbu ndio roho ya nchi kuwa na majengo mazuri yeye hadhi, ambayo yataweza kuhifadhi kumbukumbu zetu lakini pia kuwa na usalama mzuri katika majengo yale yenye kumbukumbu zetu. Mhe. Mwenyekiti utaona kwa sasa kuna ma-*watchman* tu ambao wanaangalia pale ana kirungu cheke tu.

Mimi niiombe Serikali ile ni sehemu muhimu sana kupotea potea nyaraka pale inakuwa ni tatizo kwa hivyo sasa niiombe kuwe na ulinzi tupate vikosi vyetu vilinde sehemu zile na kuwachana na ulinzi ule ambao unaweza ukaleta madhara wakati wowote. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti wenzetu wanaofanya kazi katika sehemu zile wanatumia sana kemikali nikuombe sana Mhe. Waziri na sio wao niseme wafanyakazi ambao wanakumbana na utumiaji huu wa kemikali katika kazi zao, hasa ni watu wakuangalia katika afya kwa hivyo tuweze na wao kuwapatia maziwa waweze kujengeka kiafya na wasipate wasije, kupata madhara tukaja tukapoteza wafanyakazi muhimu.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti mimi naomba kwa sababu hapa ndo Mipango yote iko hapa kwa hiyo naomba sana kuwajali wafanyakazi wetu hawa, ili tuweze kuona tuwe na wafanyakazi wenye afya. Mhe. Mwenyekiti pia niende katika suala zima la vipaumbele ambavyo mmeweza kutuanishia. Mhe. Mwenyekiti mimi niseme naipongeza hii bajeti kwa kweli imepangwa vizuri na inatupa matumaini makubwa lakini isipokuwa lazima tu, tusisitize lakini bajeti kwa kweli inatupa matumaini. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaka kusema suala zima ambalo mwenzangu ameligusia na mimi naomba nilitilie mkazo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa na ardhi ambayo tunayo hivi sasa ardhi yetu ni ndogo sana ni lazima tujikite kuwa na mipango mizuri ambayo itaweza kudhibiti ile ardhi yetu iliyobaki tuweze kuitumia vizuri. Mhe. Miraji hapa amechangia na mimi sipendi labda niseme narudia lakini kwa kutilia mkazo lazima niliseme kwa sababu kipindi kilichopita niliwahi kulizungumza hili hata ukenda katika *hansard* utalikuta. Mhe. Mwenyekiti tunapokuwa na mipango ya upimaji ni vizuri kweli hata huko vijijini tukenda tukapima. Kwa sababu tunapoacha hii nafasi wenzetu ndo wanaendeleza ujenzi, sasa hapa tukija kusema twende sisi lile eneo ambalo lilikuwa tupu halijajengwa tutakuta tayari tunaji-*cost* tena huko, kwa sababu tutakuta tayari wameshajenga kwa sababu maeneo ni hayo hayo hawana pahala pengine. Sasa niiombe Serikali kujikita katika mipango hiyo hiyo ya upimaji lakini na kujenga nyumba nafuu ambazo zitaweza kuwahudumia wananchi wetu wote kwa pamoja ambayo itaweza sasa kuwakushanya wananchi katika kijiji kimoja kidogo na kuiacha sehemu nyengine iweze kutumika kwa mipango mbali mbali ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika kifungu (h) hiki kinaeleza kufanya tafiti mbali mbali katika sekta zote zitakazosaidia utowaji sahihi wa maamuzi na upagaji wa mipango ya maendeleo. Mhe. Mwenyekiti nakubaliana moja kwa moja na kifungu hichi nikweli lazima tuwe na utowaji sahihi wa maamuzi, wewe mwenyewe utakuwa shahidi katika kuchangia wizara hapa tuliona tofauti zilizojitokeza, tulipata kauli mbali mbali hapa kutoka kwa Mawaziri huyu anasema hivi huyu anasema hivi kule naomba tatizo hili lisitokee tutakapokuwa na mipango sahihi maana yake mpango wa Serikali utakuwa ni mmoja na maamuzi yetu yatakuwa ni mamoja na tutaweza kuyasimamia sote. Tuliona hapa tulipokuwa tunachangia kwenye ardhi tuliona kauli zilikuwa zinapishana za Mawaziri wetu, sasa ile inakuwa haiko katika usahihi, ikiwa usahihi kauli yenu itakuwa moja kwa hiyo tunaomba sana hili liweze kusimamiwa na naamini katika usimamizi wako Mheshimiwa napata moyo sana, kwa sababu ni mtu ambaye unajituma sana na kuona tunataka tupipe hatua tunapata moyo.

Mhe. Mwenyekiti niendelee pia kuwapongeza katika ule mpango mzuri ambao mmejiwekea katika utaratibu, katika kulilipa deni letu tunalodaiwa na *TANESCO* hii inatupa moyo na ni kweli lazima tujipange katika kulipa deni ambalo tunadaiwa huku tukijirekebisha sisi wenyewe, kuandaa miundo mbinu mengine itakayoweza kutusaidia katika utekelezaji wa miradi yetu. Mhe. Mwenyekiti mpango huu wa kuandaa hili deni, kwa sababu deni siku zote linakuwa si zuri, deni raha yake ulipe ili pia ukitaka kukopeshwa basi uweze kukopesheka. Kwa hiyo mimi mpango huu mliouweka naupongeza na naomba Mwenyezi Mungu autie nguvu tusipate matatizo yote, hapo kati ili tuendelee kuweza kulipa deni letu hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia nitie mkazo katika ukushanyaji wa mapato. Mhe. Mwenyekiti bado tuweze kuibua vyanzo mbali mbali vipya ambavyo tutaweza kuibia kuengeza mapato yetu siku hadi siku na katika kitabu chenu hichi, mmeainisha kama mna mpango wa kujenga viwanja vyetu vile vya wilaya vya michezo. Mhe. Mwenyekiti viwanja hivi kama vitajengwa hasa, vikaweza kukidhi mahitaji hivi vitaingiza mapato kwa sababu watu wataingia kwa pesa sasa katika viwanja vile. Kwa hiyo tukiweza kulifanya hili naamini na tusilazimishe labda tukasema viwanja vyote vya wilaya tukavijenge kwa siku moja, naomba twende kwa kiwanja kimoja kimoja ambapo tutaweza kuwa na nguvu nzuri yakuhakikisha tunaingiza katika, tukimaliza hapa tutakuwa kinatusaidia kujitayarisha na ujenzi wa kiwanja chengine.

Kwa sababu hichi kitakuwa tayari kinatuingizia mapato na kila mtu akijua kiwanja fulani kipo tayari ambapo mimi naweza kwenda kukushanya pale, maana yake tunaweza sote wilaya ya kwanza tukawa tunakitumia hicho kwa ajili ya hapa tuna ukushanyaji wa mapato. Kwa hiyo mtu atakama wilaya si yakwake lakini anajua wilaya ile kule nikenda naweza nikaendesha *game* zangu hizi kwa ukushanyaji wa mapato, tuweze kujenga kimoja baada ya kimoja ili tuweze kupata nguvu ya kuweza kuzimudu hizi vyote kuvijenga.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti pia niendelee kutia msisitizo na mkazo zaidi katika uvujaji wa mapato. Mhe. Mwenyekiti pamoja na juhudi za Mhe. Waziri wetu anajitahidi na pamoja na watendaji wake lakini tunamuomba azidishe hiyo juhudi bado uvujaji wa mapato upo

bado watu miyanya wanaitumia hiyo. Mwanya mkubwa tu mtu akiupata basi anatumia katika kuona anajiwekea maslahi yake yeye, kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti bado nimwambie Mhe. Waziri na watendaji wake wajikite kabisa katika kuiangalia miyanya inayovujisha mapato yetu ili Serikali hii, iweze kujitegemea kwa bajeti zijazo ishaalah penye nia nzuri ishaallah Mwenye ezi Mungu anatatupa njia ya kuweza kupita.

Ishaallah Mwenye ezi Mungu atujaalie bajeti hii iwe ya heri na salama na tuweze kufanikiwa katika ile mipango mizuri yote ambayo tumejipagia na kwa mpango huu nasema naunga mkono kwa asilimia 100 bajeti hii na ishaallah Mwenye ezi Mungu atuwezeshe na atupe moyo thabiti katika kuijenga nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Bi. Panya Ali Abdalla kwa mchango wako mzuri sasa ninamwita Mhe. Omar Seif Abeid na baadae atafuatia Mhe. Said Omar Said Mwakilishi wa Jimbo la Wingwi.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha.

Lakini awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenye ezi Mungu mtukufu mwingi wa rehma aliyetujaalia tukakutana hapa asubuhi ya leo baada ya mapumziko ya siku mbili, tunakuomba Mwenye ezi Mungu utupe nguvu, utuwezeshe kujadili hotuba hii ya bajeti, bajeti ambayo inamuelekeo mkubwa kwa ajili ya maslahi ya wananchi wetu wa Zanzibar. Pia nakuomba Mwenye ezi Mungu wape hikma na busara viongozi wetu na wazazi wetu waliotangulia kwa rehema yako na utukufu wa mwezi wa Ramadhani iwe ni sababu ya kuingia kwao peponi – Amin.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo pia nachukua fursa hii, kumpongeza kwa dhati Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Khalid Salum na timu yake yote, timu ambayo imejikita imechukua muda mwingi kufanya kazi na kufuatilia na hatimae kutuletea vitabu hivi ambavyo wengi wamevizungumza lakini ni mara ya kwanza sijawahi kusikia kwenye Baraza hili ikawa kuna kwiri hili ni dalili tosha ya kuona kwamba sisi Wawakilishi wengi tumefurahishwa tumeridhika na mwenendo wa Wizara, chini ya Wizara ya Fedha na umakini alionao Waziri kwa hilo nasema “mcheza kwao hutunzwa” na akizidi kuongezwa kwa hiyo tunakuongezea pongezi Dkt. Khalid Mungu akupe uwezo na imani hiyo uweze kuwatumikia Wazanzibari. (*Makofi*)

Lakini Mhe. Mwenyekiti mimi kabla ya hapo nataka niingie katika kitabu cha Hali ya Uchumi ukurasa wa 8 kuliangalia pato la mwananchi. Mhe. Mwenyekiti katika kitabu kilichopita au bajeti yetu ya mwaka 2016/2017 tuliona kwamba pato la mwananchi lilikuwa ni shilingi 1,600,033 lakini kwenye mwaka huu wa bajeti wa 2017/2018 tumeliona pato hilo kwamba limeongezeka hadi kufikia 1,800,006 ni hatua kubwa ni ongezeko kubwa, ongezeko ambalo nikiashiria cha kukuwa kwa uchumi. Na hiki ndio kimoja katika kigezo cha kuona kama kweli uchumi unakuwa kwa sababu kama pato la mwananchi halikuongezeka tusingeweza kama uchumi umekuwa, lakini pamoja na hayo kunakitu ambacho kimetajwa hapa ambacho ndio kimoja katika kilichochangia ukuwaji

huo katika *page* ya 7 ibara ya16 ambayo naomba niinukuu "kwamba nasema kwa upande mwengine sekta ya huduma imeendelea kuwa na mchango mkubwa katika pato la taifa na kufikia asilimia 45 ikilinganishwa na sekta ya kilimo yenye asilimia 25 na viwanda asilimia 18".

Hapa ndio mchango wangu Mheshimiwa unapoanza. Mheshimiwa kama hivi ndiyo ilivyo kwenye bajeti hii sekta ya kilimo ni sekta muhimu ingawa hatukuwambiwa ni kilimo cha mazao ya aina gani kwa sababu yote ni mazao ya biashara ni mazao na ya kilimo pia ni mazao, lakini mimi nafikiria hapa lengo kubwa ni vilimo vyote vilivyo vya biashara na kile kilimo cha mazao ya chakula. Tukianza na mazao ya chakula mimi Mhe. Mwenyekiti napenda kuishauri Serikali kwamba sasa iyone kwamba ipo haja ya kuweka mpango mkakati wa kuziwezesha taasisi za fedha kutoa mikopo kwa ajili ya kuwaendeleza wakulima wadogo wadogo ambao ndiyo kundi kubwa. Wakulima wadogo wadogo hawa ndiyo watu ambao wanapaswa kuendelezwa. Ukitilia maanani kama nilivyosema kwamba hili ndilo kundi kubwa. Tutakapofanya hivyo tutakuwa tumepata faida kubwa sana, serikali itapata faida sehemu mbili au tatu.

Kwanza katika kutoa ajira serikali iwapo itatilia mkazo kutoa mikopo kwa ajili ya wakulima, wenzetu Bara kule walikuwa wana Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini (*CRDB*) ilikuwa inatoa mikopo mikubwa kwa wakulima. Wakulima wakaweza kutoka kwenye ukulima wa zamani wakaingia kwenye ukulima wa kisasa baadaye wakulima wale wakabadilika wakawa wafanyabiashara kwa mikopo waliyokuwa wakiipata kutokana na biashara. Iwapo serikali tutafanya hivi tunaweza kuwatoa wakulima kwenye steji wa kuwa wakulima wadogo wadogo, tukawaweka kwenye hatua ya kuwa wakulima wakubwa au wakulima wa kati. Baadae kipato chao kikakuwa kikubwa wakaingia kwenye biashara na serikali ikaendelea kupata kodi kubwa kutoka kwa vianzio vya kilimo.

Faida ya Pili ni kwamba serikali itapunguza uwingizaji wa chakula, tutaweza kulima, tutazalisha zaidi na serikali itapunguza idadi ya kuagiza chakula kutoka nje. Waziri wa Kilimo katika bajeti yake ya mwaka jana alisema kwamba ana niya ya kuhakikisha kabla ya 2020 Zanzibar iwe inajitosheleza kwa chakula. Mimi kwa upande wangu naishauri sana serikali tuzitumie vyema taasisi za fedha kuweza kutoa mikopo kwa ajili ya wakulima kwa kuwanunulia pembejeo za aina zote na zana za kilimo ili waweze kulima tutokane na ukulima ule wa zamani twende na ukulima wa kisasa.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo nilikuwa naishauri serikali kupitia hii Wizara ya Kilimo iwatumie vyema mabwana shamba na iyongeze mabwana shamba, inaonekana bado tuna tatizo la upungufu wa mabwana shamba. Tutakapokuwa na mabwana shamba wa kutosha na tukaweza kuwatumia vizuri tutaweza kuzalisha zaidi. Naiyomba sana serikali iongeze mabwana shamba na mabibi shamba warudi vijijini wakawasaidie wakulima wetu waweze kuzalisha zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia katika kitabu hicho hicho ukurasa wa 8, utakuta kuna tofauti ya mapato ya ndani, tunakwenda kwenye bajeti ya mwaka 2016/17 na utekelezaji wake na makusanyo kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2017. Nimeona kwamba

makusanyo haya ya ndani yamefikia kwa kipindi cha wastan kwa miezi tisa kuwa ni shilingi 448.2 bilioni, ukifanya hesabu utakuta kuwa ni sawa na sh. 49.8 bilioni kwa mwezi ambapo kama ukusanyaji huu utaendelea na serikali itaweza kufikisha hadi sh. bilioni 597.6 na serikali inaweza kufikisha hali hiyo, tutakuwa tumefanya kazi kubwa sana, tutakuwa tumefikia lengo kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, imani yangu kwamba kutokana na bajeti hii na kitabu kilivyoeleza kwamba serikali inampango wa kununua zile mashine za kielectroniki za kukusanyia kodi, hili linawezekana. Namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na serikali iangalie na iharakishe kuleta mashine za kielectroniki za kutolea risiti ili tuweze kukusanya kodi na kufikia lengo la hilo milioni 597 ambalo kimtiririko unaliona linawezekana kufikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, tukirudi huko naingia kidogo kwenye kitabu hichi cha Mapendekezo ya bajeti ya Makadirio kwenye ukurasa wa 8 nikiangalia mapato ya ndani nakuta zimeandikwa kodi ya mapato *ZRB* imechangia milioni 237.4 bilioni, Mamlaka ya Mapato 188.8, Mapato ya Wizara 26.4 bilioni, mpaka mwisho *section* ya (F) kuna gawiwo la faida kutoka kwenye Mashirika ya SMZ yana bilioni 4.8.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu uko hapa. Tukiangalia kwa hapa gawiyo kutoka na faida ya Mashirika ya SMZ mimi hapa naona bado roho yangu haijaridhika. Naiyomba sana serikali kwa hapa iangalie yale mashirika ya serikali ambayo yamepewa mamlaka ya kukushanya na kutumia yaweze kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye mfuko. Tukiachilia mbali, mimi najua Shirika kama la Bandari makusanyo mengi ya *TRA* na *ZRB* yanatokea Bandari lakini bado kwa wenzetu Shirika kama la Bandari, watu wenye bandari ukiangalia Kenya, ukiachilia mbali mapato ya *KRA* yanayokusanywa pale Bandarini Kilindini. Utakuta ile wanayoita (*port charge)* ada ya ushuru wa bandari inachangia asilimia karibu 20 ya Bajeti ya Kenya.

Mhe. Mwenyekiti, na sisi iko haja ya kubadilika tukaifanya bandari ikaweza kukusanya (*port charges)* nyingi ile ada ya bandari ikaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, inaingia lakini ikaongeza kwa kiasi kikubwa. Pia kuna jambo jengine ambalo naomba serikali iliangalie sana na najua na nina imani na litatekelezeka. Napenda kusoma kidogo kwenye kitabu pale Mwenyezi Mungu alivyoambiwa na Nabii Ibrahimu kwamba nionyeshe jinsi unavyouwa na unavyohuisha. Mwenyezi Mungu akamuuliza Ibrahimu wewe huamini kama mimi naweza kufisha na kuhuisha. Akamwambia naamini lakini nataka nione ili na mimi moyo wangu uridhike.

Na mimi naamini kwamba serikali itafanya lakini nataka kusisitiza kwamba ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri ni kitu ambacho kinahitajika kupewa kipaumbele kulikoni miradi yote kwa sasa. Bandari ya Mpigaduri iwapo itaweza kujengwa ikawa kama tulivyokusudia inaweza ikachangia kwa asilimia 40 ya pato letu kwenye mfuko mkuu wa serikali. Naiyomba sana serikali kwenye vipaumbele vyake vyote ilivyonavyo katika miradi ya maendeleo iweke mradi wa Bandari ya Mpigaduri kama ndicho kipaumbele Nam. 1 cha mradi wa maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumza haya kwa sababu najua kwamba serikali ina nia nzuri ya kuijenga na itaijenga. Tuna vijana wengi ambao hawana kazi itatusaidia sana kupunguza tatizo la ajira lakini pia itaongeza kwa kiasi kikubwa pato la serikali. Sasa Waziri naomba unambie lini kazi hii tutaianza. Ili na mimi roho yangu itulie niweze kujua kwamba mwezi fulani bandari ya Mpigaduri inaanza kujengwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nilikuwa nina jambo jengine ambalo nimeliona mimi halinifurahishi. Najua serikali hili inalo na inalifanyia kazi lakini ni kukuta kwamba kwenye maeneo ya wawekezaji tunachukua wawekezaji wengi, wawekezaji tunakuwa tunao lakini badala ya kuwapa ardhi zetu kwa bei ndogo ardhi hizi wanazitia kwenye *internet* wanaziuza kwa bei kubwa. Hali hii haifurahishi sambamba na kuchukua maeneo wakayaweka bila ya kuyaendeleza. Wito wangu na ushauri wangu kwa serikali kwamba wawekezaji wote ambao wamepewa maeneo na najua kwa sababu sheria ipo wayatumie, ikiwa haiwezekani kuyatumia kwenye muda uliotajwa na sheria, serikali isione shida kuyabadilisha wakawapa watu wengine. Jambo hili tumelisema kwa muda mrefu na leo naomba tena katika bajeti hii hotuba hii nilichangie kwa ajili ya maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, ardhi ndiyo mali wenzengu wamesema sana na mimi nasema sana kwamba kama hatukukaa makini hapa, mimi nampongeza sana Mhe. Jonh Pombe Magufuli...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mheshimiwa niongeze kidogo japo dakika tano.

Alipoliona tatizo la mchanga wa madini alilichukulia hatua mara moja na leo wale ambao wamehusika na yale wamekubali kulipa. Sasa na sisi wale tuliowapa maeneo yetu wakawa wameyaweka tuyachukue au wakubali kulipa kodi kwa muda wote mara mbili. Sisi tuliwapa maeneo kwamba wayaendeleze ili vijana wetu wapate kazi, serikali ipate kodi ingawa wao wanatulipa kodi ya ardhi lakini je, kodi nyengine za kibiashara walizokuwa wanafanya, sisi tumezikosa kwa hivyo zile kodi tuwafanyie makisio watulipe, ikiwa hawawezi serikali maeneo yale iyachukuwe iwape watu wengine. Lengo ni kuona kwamba serikali inakusanya mapato zaidi kutokana na vianzio vyake vya mapato ikiwa kimoja ni hiki.

Mhe. Mwenyekiti, mambo yaliyokuwepo ni mengi mengine nitapeleka kwa maandishi. Mimi nitoe wito la mwisho kabla ya kunipigia kengele nazungumzia makimbilio ya wanyonge *ZSSF*. Mheshimiwa *ZSSF* ni Shirika ambalo linatakiwa lijiendeshe kibiashara na litunufaishe, limeonesha muelekeo mzuri na wakutunufaisha. Wazee wetu wakimaliza kustaafu wanahitaji kupata mafao mazuri. Kwenye bajeti hii imeelezwa kwa undani na mimi naishauri sana *ZSSF* isiangalie upande mmoja tu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa malizia, Mheshimiwa malizia.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mheshimiwa, kwa heshima na taadhima kubwa Mhe. Mwenyekiti, natamka rasmi kwamba nimeunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia

na nawaomba Wawakilishi wenzangu tuiyunge mkono hotuba hii ili tuweze kumuwezesha Waziri wa Fedha afanye kazi zake, atekeleze majukumu yake tuliyompa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana tunamwita sasa Mhe. Said Omar Said, Mwakilishi wa Jimbo la Wingwi na baadaye atafuatia Mhe. Sada Ramadhan Mwenda na atafuatiwa na Mhe. Tatu Muhamed Ussi ajitayarishe.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa na mimi nafasi kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kwa kuona mpaka sasa hivi ninayo amana yake. Pia kuniwezesha nikawepo katika Baraza hili kwa siku ya leo. Lakini pia nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya serikali. sight. slice. site, cite

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa jinsi alivyoiwasilisha hotuba hii kwa fasaha kabisa na tukaielewa, tukamsikia na tukamfahamu. Pia nichukue nafasi hii kuwapongeza wote waliomsaidia wakamrahisishia kazi hii ya kukusanya taarifa hizi na kuziwasilisha mbele ya Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niishukuru sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kueleta bajeti hii iliyo safi kabisa. Bajeti hii imewajali watumishi wa serikali kwanza, bajeti hii imewajali wastaafu wa serikali, bajeti hii pia imewajali wakulima.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze mchango wangu kwenye Sekta ya Uwekezaji, kwa kuwa moja ya malengo ya uwekezaji hapa Zanzibar ni kuinua pato la uchumi wetu hapa Zanzibar na kuwapatia vijana wetu ajira.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tunavyo visiwa viwili Unguja na Pemba, mimi niishukuru sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kupeleka maendeleo kila ncha ya visiwa vyetu. Inapoamua kuweka nyumba za maendeleo Unguja na Pemba zipo, nyumba za kulelea watoto Unguja na Pemba wanajenga zipo, nyumba za kulelea wazee Unguja na Pemba pia zipo. Nasema tuishukuru na tuipongeze sana serikali yetu kwa uwadilifu wake huo. Pia inapoamua kuweka maeneo ya uwekezaji Unguja pia inaweka na maeneo hayo Pemba. Lakini tuu ningeomba kitu kimoja hapa ile shabaha yetu ya Serikali kuhusu uwekezaji ifanikishe kisawasawa kama ilivyopangwa nataka tuangalie hali ya kiuchumi ya Unguja na hali ya kiuchumi ya Pemba yumkini ni dhahiri kwamba Unguja hali ya kiuchumi afadhali kuliko hali ya kiuchumi iliyoko Pemba.

Kwa mfano hii gari ya abiria kutoka Darajani hadi Bububu Shs. 400 tuu lakini ikifika jioni tajiri anafurahi mapato aliyopata japo mia nne tuu lakini Pemba daladala hiyo yenye masafa kama hayo nauli yake ni shilingi 1000 lakini ikifika jioni dereva hana hata mafuta, hii ni kutokana na hali ya kiuchumi ilivyotafautiana sasa kama hivyo ndivyo Mhe. Mwenyekiti mimi ningeiomba Serikali kwamba kidogo pakafanya unafuu wa bei yaani ya kodi wanaokodishwa hawa wawekezaji hii sehemu ya ardhi baina ya Unguja na Pemba yaani hapa kidogo pafanywe unafuu kule Pemba pafanye mabadiliko marekebisho kidogo ya hii kodi.

Kwa mfano ikiwa muwekezaji wa kigeni anatozwa dola kati elfu 7,000 na alfu 5,000 kwa hekta moja na alfu 3,500 na alfu 2,000 kwa muwekezaji mwenyeji basi hiyo isiwe sawa bei hiyo na kule Pemba yaani kule Pemba kuwe ni chini ya bei hiyo, kwasababu aliyechukuwa eneo Zanzibar hapa Unguja na aliechukuwa eneo kama hilo Pemba basi yule Pemba atachelewa kuleta maendeleo kule kwa eneo lake lile lile eneo lake kama la mwenzake huku wakati mwenzake huku analipatia manufaa, hii ni kutokana na hali ya kiuchumi.

Kwa hivyo ningeomba Serikali ili hii sekta ya uwekezaji na kule Pemba imarike basi ifanyiwe wale wa kule wawekezaji watakao kwenda kule Pemba waone kuna punguzo fulani hii ndio ikatayo walazibisha wao wale wawekezaji wa nje pia wawekezaji wa ndani, ningeliomba hilo sana Mhe. Mwenyekiti ili na sisi kule tupate uimara wa uwekezaji, uwekezaji uimarike kama ambavyo umeimarika hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nende kifungu cha 57 ukurusa wa 26 kuhusu Kuimarisha Huduma za Jamii mimi niendelee tena kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuimarisha Miundo Mbinu ya Wizara ya Elimu. Mitaala ya elimu imeboreshwa ipasavyo ambao ilikuwa tofauti tukipiga kelele sana tukisema mishahara haiendani hali yetu leo mitaala imeboreshwa sana kabisa ya Wizara ya Elimu maslahi ya walimu yameboreshwa sana, walimu wa kila fani kila mtu na kiwango chake lakini wameangaliwa vizuri sana walimu sasa kilichobaki tatizo lililobakia ni ufaulu wa wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na juhudi kubwa ya Serikali pamoja na gharama kubwa ya Serikali kwa Wizara ya Elimu lakini bado suala la ufaulu hatufikia pahala haijalipa gharama ya Serikali kwa Wizara ya Elimu haijalipa gharama hiyo, hasa ni wakati wa kujiuliza kwani kuna nini kuna maradhi gani yanayosababisha hivyo kwa sababu ikiwa mitaala ni mitaala bora ni mitaala ya kisasa, mitaala inayokwenda na wakati na ikiwa maslahi ya walimu ni maslahi bora sasa kinachobakia nini sasa hapa lazima tukae tutafakuri nini sababu inayopelekea wanafunzi wakawa hawafaulu inavyohitajika.

Mhe. Mwenyekiti, labda kwa haraka haraka nidhani kwamba moja katika linalosababisha hilo ni wingi wa *tuition*. Mhe. Mwenyekiti wazee wasema ninoyafuja katika kitu kitamu ni sukari lakini kama ukitia glasi moja ya maji ukatia sukari robo kilo huinywi pamoja na utamu wake, hasa hizi *tuition* zinafanya hawa wanafunzi wazubae zinawafanya wanafunzi wachanganyikiwe Mhe Mwenyekiti sasa hivi kwa sababu wewe utawaone huruma hasa wanafunzi hawana mapumziko huoni kupumzika saa zote ni pirika asubuhi, mchana, jioni, usiku saa zote ni kwenda huko sasa hawapati nafasi ya kupumzika, hawapati nafasi ya kuzingatia yale masomo yao hasa wanakwenda katika hali hizo hizo mpaka inakaribia mtihani hasa kwenye mtihani hachukuwi buku na hana *memory* hata wakati wa kuingiza kwanini kwa pirika huku na huku washanganyikiwa hawajui wafanye nini hili lizingatiwa bosi wangu.

Lakini zaidi ya hilo ni kwamba hizo *tuition* wanapokwenda walimu wao ni wanafunzi wenzao wale wanafunzi wa madarasa ya juu. Wanafunzi wa madarasa ya juu ndo walimu wao sasa hapa panatakiwa tatizo hili wanafunzi wale wanayasahau yale ya walimu, yale

masomo ya mule darasani wanayapuuza, wanayapuuza masomo anayofundisha mwalimu lakini wanayakumbatia yake wanayofundishwa na wale vijana wao. Wakati mwalimu anaeleweka kitaifa mwalimu kwa kuwa anaeleweka anayo leseni kila mwalimu ana leseni yule hata awe Chuo Kikuu hana leseni hiyo ya uwalimu ule hana leseni ya uwalimu kwa hiyo tofauti yule na mwalimu mwenye leseni.

Mwalimu anafuata mtaala aliopewa kwasababu mtaala una wakaguzi wanakuja kumfuata mwalimu unafundisha kufuata mtaala gani huu *reference* gani hii sasa hivyo ndio anavyokwenda mwalimu, lakini kwenye *tuition* kule hakuna hayo yeye yule aenda tuu si anataka pesa tuu yule, hazingatii mtaala wana hazingatii umri wala hazingatii hana njia za ufundishaji mpaka yule kumfahamu. Sasa matokeo yake ndiyo hayo wanafanya mtihani wanafunzi hawakulala, hawakuapumzika wala hawakufanikiwa kwa hivyo hapa pia Serikali ipaone ili mnaweza wimbi hili likachukuwa muda mrefu Serikali inapata gharama kubwa kwa elimu watoto wanahangaika asubuhi, jioni, usiku na matokeo mabaya, lazima watengewe wakati wao wale watoto na pia kuwatafutiwe walimu kuwatunza masomo ya ziada.

Mhe. Mwenyekiti, jengine linalofanana na hili ni kwamba wanafunzi baada ya kufanya mtihani wao wa mwisho hufanikiwa wanaofanikiwa na wengine hubakia pale hawafeli lakini huwa maksi zao hazikutosha tuu kuingia kule, lakini si kwamba wamefeli alosoma hajafeji maksi tuu alama tuu zile zimekuwa kidogo sasa kwa wale ambao alama zao zimekuwa kidogo kwa kipindi kile ningeiomba Serikali ikaweka ulazima wa kujiunga na mafunzo ya amali ikawa ni lazima sio hiyari Serikali ikaweka ulazima baada ya ku *drop* aingiye kule kwa lazima kwasabau gani kwasababu lengo la mwanafunzi yule ni ajira Serikali inataka kuajiri wangali na Serikali imesomesha watu wengi Zanzibar yote ina elimu sasa hivi tofauti na tunapotoka leo Wazanzibari wote ni wenye elimu na kila mwenye ataka ajira sasa ajira hiyo ataipata wapi kwa hivyo ningeiomba Serikali kwa wale *drop out* wapelekwe tena kwa ulazima hasa kwenye vyuo au kwenye mafunzo ya amali mtu akitoka pale inategemea umahiri wake ujanja wake, lakini anapondoka pale wako ambao waliotoka katika Vyuo vya Amali.

Mhe. Mwenyekiti, wakapata ajira Serikali wako ninaowaelewa huyu amemaliza Chuo cha Amali pahala fulani baadae akaajiriwa Serikalini akacha kazi yeye mwenyewe akaendelea na kazi zake...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika moja muda wako umemaliza.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante kwa hivyo ni yumkini kwamba mwanafunzi yule ambaye atapata kule mafunzo anaona bora kuyatumia mafunzo yake kwa maisha yake ya kila siku kuliko ajira.

Mhe. Mwenyekiti, basi nimalizie kwa mfuko wa bei. Mhe. Mwenyekiti hili suala la kupanda kwa bei mimi niseme kwamba liko nje ya uwezo wetu hili suala hili liko nje ya uwezo wetu sasa la kufanya nini nikuongeza juhudi ya kilimo, kuiomba Serikali ituandalie zana za kilimo kama matrekta itupelekee matrekta majimboni, itupelekee matreka hayo kwa wakati, itupelekee mbegu kwa wakati...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemaliza.

Mhe. Said Omar Said: Ahsante Mheshimiwa nimalizie la pili kuhusu wafanyabiashara hali ya uchumi hali ya mfumuko wa bei Mhe. Mwenyekiti unatoka na wafanya biashara wenyewe lazima wale wafanya biashara wawe nia zao ni safi kabisa kwa wenzao utapatikana unafuu kweli naiomba Serikali kwa kumalizia tuu iwaangalie sana hawa wafanya biashara kuwashawishi na kuwapa maneno ya kinasaha ili wende alau wende pole pole katika bei zao kwa maslahi ya Zanzibar wote.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante anaefuata ni Mhe. Saada Ramadhani Mwendwa na baadaye atafuatiwa na Mhe. Tatu Mohamed Ussi.

Mhe. Saada Ramadhani Mwendwa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii nitapata kuzungumza haya machache nilokuwa nayo.

Lakini kwanza niishukuru Kamati ya Bajeti chini ya Mhe. Dimwa kwa kazi kubwa waliokaa tumekuwa tukiwashuhudia wanavyohangaika hapa kututengezea bajeti nzuri ambayo kuwa kutuletea maendeleo kwa wananchi wetu nawambia ahsante sana. Mheshimiwa mimi sina mengi na mambo kidogo tuu niliyokuwa nayo nilitaka kuzungumzia upande wa afya.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali imekuwa inajitahidi sana kutusaidia sisi wananchi inajitahidi Serikali kujenga hospitali kila pahala ili wananchi wake walio mbali na walio vijijini wasipate tabu ya kupata huduma hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka kuzungumzia upande mmoja nilikuwa naiomba Serikali upande wa hospitali ya Chumbuni.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba Serikali hospitali ile iko katikati ya wananchi, hospitali ile tuna watoto wanaenda skuli, tuna watoto wanaenda vyuoni lakini lengo kubwa lililowekwa la kuwekwa matatizo kuwekwa kuwa ni kituo cha kipindupindu nilikuwa naiomba Serikali kupitia bajeti inayokuja basi bora itafute sehemu ijenge lakini pale ni kati kati sana wananchi wanaathirika bila ya kuwa na matatizo, ukiangalia hasa Mwenyekiti kule Chumbuni namshukuru Mwenyezi Mungu siye sasa hivi pale hakuna matatizo hayatokei pale kwetu watu wanatoka Kinuni wanatoka wapi wanaletwa pale, wanapoletwa pale juzi pia tumeshuhudia watu wanakimbia anatoroka mwanamke katoroka tukamrejesha sasa yule anapotapika, anapoharisha njiani mule ina maana wale watoto wanaende skuli na kurudi ni madhara naiomba Serikali itufikiri watu wa Chumbuni, itufikiriye watu wa Karakana ile hospitali wafanye mbinu yoyote waiweke nje ng'ambo isiwe katikati ya wananchi pale inaleta madhara mengine naiomba sana Serikali kupitia suala hili basi ituangalie sisi wanawake wa Chumbuni watafute sehemu nyengine waiweke.

Lakini jengine Mwenyekiti hospitali ile tuliwekwa kwa malengo ya kupimwa wanawake, watoto imekuwa hatupati tunashindwa kwenda hali ya watu kule masikini hali zao ngumu hawafiki popote wanategemea hospitali ile.

Wabunge wetu na wawakilishi wanakuwa wanajitahidi pakibomoka hapa wanajenga pakifanya hivi wajenga lakini sasa tokeo lake Serikali tunaomba sana Serikali tuko chini ya miguu wanawake wa Chumbuni basi itafute sehemu nyengine ya kipindupindu watuachie pale, jamani kipindupindu hakiwezi kukaa katikati ya mji kama ule tunaiomba Serikali ikapata uwezo tuu basi itafute eneo jengine ijenge pale ituachie tuhudumiwe sisi wanawake hilo la kwanza Mhe. Mwenyekiti.

Lakini jengine miye nilikuwa naenda upande wa mawasiliano miye Mwenyekiti ninapotoka Chumbuni huko kuja mjini ikifika Kariakoo tu naanza kuona mimi nishaanza kufika Mjini. Lakini namuomba Mhe. Waziri wa Mawasiliano jamani kuanzia Michezani pale kweli ile barabara vile ilivyo tuseme ndio Mhe. Waziri haioni au ndio hatuna uwezo hata wa kupiga *repair* angalau yale mashimo tukayafukia, mambo mengine Mhe. Mwenyekiti aibu. Namuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha awagaie bajeti kidogo ya pesa angalau waizibe zibe ili yale mashimo pale Michezani aibu kubwa njia sio ile. Mhe. Mwenyekiti, jana nusura ajali zitokee pale kote kule kuanzia Michenzani ukitoka Kisonge mpaka Kachorora pale pamechimbuka ajabu utafikiri mawasiliano hawapo au wao wenyewe kweli ndio hawaoni hivyo.

Kwa hiyo, nawaomba sana mheshimiwa wajitahidi kulifanya hilo ili tuepuke na ajali ndogo ndogo zitakazoweza kutokea pale. Lakini ili mji wetu uwe mzuri kwa sababu ukifika pale ukiangalia majumba ya Michezani yale Mwenyezi Mungu alivyotujaalia Mzee Karume katujengea, lakini ukiangalia chini hujui hata upite wapi. Nawaomba sana serikali ijitahidi kwa hilo ili tuwe na mji uliokuwa mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa sina mengi isipokuwa kubwa ilikuwa naipongeza serikali bajeti yake kubwa hii waliotuletea Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake lakini *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na sisi kama ni wajumbe humu tutaipitisha ili kuleta maendeleo ya wananchi wetu wa Zanzibar na kuleta maendeleo zaidi ya wananchi wenye kipato cha chini. Kwa sababu inavyotakiwa bajeti hii ndio manufaa yetu sisi tulioko chini kwa kujitayarisha na maisha yetu ambayo kuwa nina uhakika pesa hizi zitarudi bajeti kubwa itaenda hospitali kutujali sisi wanawake, na pesa hii itaenda kila sehemu kama maskuli, wanawake na watoto ili kuleta maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo, ninaipongeza sana na naishukuru na naunga mkono mia kwa mia. Lakini langu kubwa ilikuwa ni hospitali naiomba serikali ilifikirie wanawake wa Chumbuni tunateseka. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Saada ahsante sana, sasa anafuta Mhe. Tatu Mohammed Ussi na Mhe. Yussuf Hassan Iddi ajitayarishe.

Mhe. Tatu Mohammed Ussi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi kabla ya kuchangia nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama hapa ili na mimi

nizungumze machache kuhusu bajeti yetu hi ya serikali. Nianze kwa kukushukuru na wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kumpongeza Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa kwa ajili ya mpango wa uchumi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, nampongeza sana. Lakini pia niwapongeze na watendaji wote waliokaa kuipanga bajeti hii. Pia niipongeze Kamati ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Mohammed Said Mohammed.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na mchango wangu katika sekta ya fedha kwenye ukurasa wa 10, huduma za kibenki. Katika sekta hii imeeleza kuwa hali ya uchumi na mipango imeimarika kutokana na huduma za benki kutokana na ongezeko la amana kwa asilimia 33.4. Ni jambo la kupongeza sana na nimeeleza sababu ya ongezeko hili ni uhamasishaji wa benki kutokana na kushirikiana pamoja na watumiaji wa huduma ya simu za mkononi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa naomba serikali itoe muongozo kwa wananchi kuhusu miamala ya kifedha kupitia simu za mkononi. Kwani Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya wananchi wanapata matatizo yanayojitokeza kwa kutumia miamala ya fedha kupitia simu za mkononi, kwa sababu kuna watu ambao wakati mwengine wanatumiwa fedha au wanatuma fedha kimakosa na baadae wanapata usumbufu fedha zile kuzirejesha. Hivyo, tunaiomba serikali ikae na makampuni ya simu kuweka miongozo ya usalama wa miamala ya fedha kupitia simu za mkononi.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda hapo hapo kwenye huduma za fedha. Mhe. Mwenyekiti, pale Vikokotoni palikuwa na benki inayoitwa *FBME*, benki hii kwa sasa imefungwa na *BoT* kutokana na kufilisika. Sasa nilikuwa nataka kujua je, ni nini hatma ya wananchi wale ambao waliweka fedha zao katika benki ile?

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nitaenda kwenye suala zima kuhusu mapato na matumizi ya serikali. Kwa dhati kabisa ya moyo wangu niipongeze bajeti ya mwaka huu kutoka bilioni kuingia kwenye trillion. Mhe. Waziri ameonesha hali ya ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2016/2017 lakini imeongeza kwa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nashauri sana tuongeze wigo wa kukusanya fedha ya mapato yaliyokuwa ya kodi na yalikuwa si ya kodi kupitia benki, kwani mapato yanayokusanywa katika mawizara, idara za serikali yanakusanywa yawe na utaratibu rahisi wa kupitia benki badala ya kupitia mikononi mwa watu. Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali tuondokane na kulipia huduma kupitia vidirishani na badala yake uwekwe utaratibu usiokuwa na usumbufu, malipo yote ya taasisi ya serikali yanayokusanya fedha yapitie benki.

Mhe. Mwenyekiti, naomba utaratibu wa malipo kupitia benki kwani tumeona hivi karibuni Idara ya Usafiri na Leseni wamekuwa na mpango mzuri unaopunguza usumbufu, lakini bado kuna tatizo dogo ambalo limejitokeza liliopo na baadhi ya wananchi wanalipigia kelele. Usumbufu uliopo unapoteza muda mtu kwa sababu mtafutaji leseni anapohitaji leseni inabidi aache kazi zake aende benki kupanga foleni ili

kulipia shilingi elfu 3000/- za ruhusa ya barabara. Mimi nilikuwa nashauri tu kwamba watu wa benki ingekuwa vizuri wakaweka mawakala wao katika zile sehemu ambazo zinatoa leseni ili kuondoa ule usumbufu wa wananchi unaojitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, pia napendekeza taasisi nyengine za serikali zinazotoa fedha zitumie utaratibu wa mawakala wa benki kwa kukusanya malipo hayo, utaratibu huu utasaidia sana kutanua wigo wa makusanyo ya serikali ili yasipotee.

Mhe. Mwenyekiti, nije ukurasa wa 15 ambao kuna masuala ya MTAMBUKA. Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hiki kuna masuala ya MTAMBUKA ambayo ukurasa wa 15 unasema ni chati isiyorejesheka. Mhe. Mwenyekiti, nipongeze sana kuona serikali imechukua hatua madhubuti katika mpango wa kuhakikisha Zanzibar inakuwa na umeme wa uhakika wakati wote. Sasa hapa zimeelezwa fedha jumla ya Euro bilioni 3.0, hapa lakini Mhe. Mwenyekiti fedha hizi hazijaonesha mchango wa serikali ni kiasi gani. Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri akija atueleze katika fedha za mradi huu wa umeme mchango wa serikali ni upi, kwani Mhe. Mwenyekiti tusije tukategemea wafadhili hatujajua serikali yetu imejipanga vipi halafu wafadhili hawa wakatuacha mkono na mradi huu ukashindwa kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, nikija hapo hapo kwenye suala la MTAMBUKA sasa nitaingia katika suala zima ukurasa wa 22 udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, ninapokuta sehemu iliyoandikwa udhalilishaji wa wanawake na watoto kwa kweli inaniuma sana ndani ya nafsi yangu, hasa kwa vile mimi ni mwanamke na ni mzazi. Mhe. Mwenyekiti, kuna mpango wa miaka mitatu 2017/2022 umeandaliwa kwa ajili ya kupambana na ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto ambao utazinduliwa baadae. Mhe. Mwenyekiti, bado suala hili ni tatizo kubwa ingawaje juhudi za serikali zinachukuliwa. Kwa hiyo mimi naomba nieleze kuwa mimi ni mwanamke ninayewakilisha wanawake na ni mwanamke niliyezaa tumo vijijini tunaona wanawake wenzetu ambao watoto wao wamefikwa na kadhia hii. Sasa ni jambo ambalo linatusumbua sana na kweli linatudhalilisha sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika muono wangu kwa kuichangia hotuba hii kwanza naomba nitoe ushauri kufanya kuwe na adhabu kwa yule yote anayefanya makosa ya udhalilishaji yawe ni miongoni mwa makosa yasiyokuwa na dhamana. Mheshimiwa kwani tunapoitoa dhamana yule mtu anayefanya kile kitendo akitolewa basi anakuwa anapita mitaani akijisifu na vile vile ule ushahidi unakuwa unapotea.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kwamba kuwekwe adhabu kali kwa mtu yeyote ambaye atashiriki hatua za kuyamaliza mambo haya ya utaratibu wa kisheria. Kwa nini nikasema hivi Mhe. Mwenyekiti? Sisi wazee wenyewe, sisi wananchi wenyewe kunakuwa na kesi kama hizo halafu tukazipiga kifua, tukishazipiga kifua tukasema watu wapatanishwe jambo limalizike ina maana sisi baadae tunarudi tunalalamika. Sasa kwa ushauri wangu zipo kesi nyingi kama hizo ambazo nyengine zimefikishwa Mahakamani na nyengine bado hazijafikishwa Mahakamani. Sasa mimi nilikuwa naiomba tu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuleta marekebisho ya sheria ambayo yataonesha mtu yeyote atakayeshawishi kesi

imalizwe nje ya mkondo wa sheria awe ametenda kosa linalostahiki adhabu. Lazima mkakati wa kupambana na vitendo hivi vya udhalilishaji uchukuliwe na sura ya mapambano ya kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu mwengine kumekuwa na tatizo kubwa la ukosefu wa uadilifu wa vyombo vinavyosimamia kesi za udhalilishaji. Hapa nazungumza sisemi wote lakini kuna baadhi ya watendaji wa Jeshi la Polisi, Mahakama na kadhalika. Sasa tulete sheria kuweka utaratibu wa mamlaka au tuongeze pale mamlaka ya rushwa na uhujumi uchumi iwe mdau mkubwa katika kutazama hatua za upelelezi tokea kesi inapopelekwa Mahakamani mpaka inapomalizika. Mimi nilikuwa nashauri hilo Mhe. Mwenyekiti lakini maana yangu tuwe na mpango wa kuchunga uadilifu kwa vyombo vinavyosimamia kesi za udhalilishaji, kwani malalamiko ya baadhi ya wahusika kuziendeleza kesi hizi yapo. Hivyo mamlaka ya rushwa ihusishwe katika kutazama mienendo ya vyombo hivo wakati wa upelelezi wa kesi inapokuwa Mahakamani hadi mpaka mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ushauri wangu katika marekebisho ya sheria naomba kuwekwe kifungu au ikibidi tuje na sheria mpya kabisa ya kulinda mashahidi. Mhe. Mwenyekiti, tunakuwa tukizungumza hapa mashahidi na mashahidi ni sisi wananchi tunaona zile kesi, tunakuwa tukizungumza mashahidi hatwendi, hatutoi ushahidi lakini sasa mimi Mhe. Mwenyekiti nilikuwa nashauri kuwe na sheria itakayomlinda shahidi, kwani wapo watu wanataka kukaa ushahidi Mahakamani. Lakini baadae hutokea watu wakawatisha, wakawarubuni na kuwapa maneno yaliyokuwa hayana maana. Kwa hivyo, inabidi wale watu wanakuwa wanarudi nyuma kwenda kukaa ushahidi. Napendekeza tuje na sheria ya kulinda mashahidi itakayoweka utaratibu wa kudhibiti vitendo hivyo, sote tunajua hakuna hatia bila ya ushahidi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine napendekeza sana tubadilishe sera au tuweke kwenye sheria udhibiti wa maporomoko wa maadili. Jambo hili serikali imeliwacha kwa jamii sana na viongozi wa dini, sio sawa mheshimiwa lazima tushirikiane wananchi na serikali yenyewe. Lazima serikali iweke mkono wake kudhibiti mporomoko wa maadili, serikali hii idhibiti mambo yanayopelekea kuporomoka kwa maadili kwani maadili yakikosekana hata utungaji wa sheria unaongezeka mwishowe amani na utulivu hakuna katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo mimi nashauri vyombo vya habari vinavyoonesha vipindi vyenye maudhui yanayoashiria matendo machafu kama vile utumiaji wa madawa ya kulevya, zinaa, ukahaba, ugomvi, matusi na mambo mengine haya yadhibitiwe kwa kuweka kanuni kali za kukataza vyombo vya redio na TV kuweka vipindi vya michezo au burudani zenye maudhui hayo, hilo pia liko kwenye uwezo wa serikali sheria zirekebishwe.

Mhe. Mwenyekiti, jengine…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemaliza na nimekuongeza muda.

Mhe. Tatu Mohammed Ussi: Ushamalizika eeh! kidogo namalizia tu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nilokuwa nalo ni moja kuhusu udhalilishaji wa watoto tumegundua baadhi ya watu wabaya wanaharibu watoto kujipenyeza kwenye maeneo ambayo watoto wanapopatikana kwa wingi. Kwa mfano, maskuli, madarasani, kwenye timu za mpira, vituo vya kulelea watoto. Kwa hiyo, ombi langu mimi Mhe. Mwenyekiti kila taasisi inayohusika na maeneo hayo niliyoyataja waweke utaratibu wa kisheria au kanuni kuweka kumbukumbu za watu wote wanaojihusisha na watoto kwa namna moja au nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu muda wangu umemaliza na mimi nina mengi, kwa sababu suala la udhalilishaji linaniuma sana nitapeleka kwa maandishi. Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hayo naunga mkono hotuba hii ya bajeti asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante mheshimiwa, sasa namwita Mhe. Yussuf Hassan Iddi akifuatiwa na Mhe. Ame Haji Ali ajitayarishe.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza na mimi kunipa fursa hii adhimu ya kuweza kuchangia hotuba ya makadirio ya bajeti ya mapato na matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Kwanza kabisa nimshukuru Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake lakini pia tuwapongeze watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa namna wanavyochapa kazi na kutekeleza vyema ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2015/2020. Kwa hiyo, tunawaambiwa kwa ujumla hongereni sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile muda sio rafiki kwa hivyo mimi nitakwenda moja kwa moja. Mhe. Mwenyekiti, michango yangu mimi imegawika katika maeneo mawili, eneo la kwanza litakuwa la kijumla jumla na eneo jengine nitajikita zaidi katika hiki kitabu kikubwa.

Kwanza nianze na suala la pato la taifa. Tuipongeze serikali kwa pato la taifa kuongezeka kutoka shilingi 1,188 bilioni ya mwaka 2015 hadi kufikia 1,268 bilioni kwa mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 6.8. Lakini ukuaji huu bado ni mdogo kwa hivyo jitihada lazima ziongezwe ili kufikia lile lengo ambalo ni kubwa zaidi.

Vile vile pato la mwananchi ukiangalia kwa mujibu wa kitabu hiki limeongezeka kutoka shilingi 1,633,000 hadi shilingi 1,806,000 lakini nayo hii ni hesabu ya mwaka kwa hivyo, ukigawa kwa siku utaikuta kama ni shilingi elfu nne mia tisa na kidogo. Kwa hivyo, bado ukiangalia kipato cha mwananchi mmoja mmoja hakilingani na hali halisi ya maisha yetu yalivyo. Kwa sababu kama shilingi elfu tano anaipata mwananchi wa kawaida kwa maisha ya kawaida ni pesa ya chai asubuhi. Kwa hivyo, ipo haja kwa serikali yetu kuhakikisha kwamba inafikia lile lengo la dira ya maendeleo ya 2020, kwa sababu tumejiwekea malengo hayo na kwa mujibu wa vitabu hivi ambavyo tumekabidhiwa kwamba ikifika mwaka 2020 tunatakiwa *at least* mtu mmoja awe anapata dola kuanzia 1,040 hadi dola 3,000. Kwa hivyo, tuwaombe wenzetu wa tume tuliokuwanao

tunawategemea katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar wahakikishe kwamba *target* hii ambayo tunaiweka ya dira ya maendeleo ya 2020 basi inafikiwa.

Jengine nije kwenye suala la mfumko wa bei, bado tunaona kwamba hili ni tatizo sugu. Mfumko wa bei unaongezeka siku hadi siku, ukiangalia kwa mwaka 2015 tulikuwa kwenye asilimia 5.7 lakini mwaka 2016 ilikuwa ni 6.7, lakini hata juzi kipindi hiki tumeanza Mwezi wa Ramadhani vile vile kuna ongezeko kubwa la mfumko wa bei, licha ya misamaha ya kodi ambayo imetolewa. Kwa hivyo kwa kuwa ni jukumu la kusimamia huu mfumko wa bei zaidi uko katika *central bank* yaani *BoT* basi tuwashauri wenzetu wa *BoT* wazishauri vizuri serikali zetu mbili hizi za SMT na SMZ vile vile watekeleze vizuri sera za kifedha ambazo zitatetea ukuaji wa uchumi pamoja na kuongeza jitihada licha ya kwamba tunaambiwa mfumko wa bei uko katika tarakimu moja, lakini tusiridhike na tarakimu hii moja kwa hivyo lazima jitihada ziongezeke vile vyanzo *sources* ambazo zinapelekea mfumko wa bei kuwa mkubwa basi serikali ifanye kazi kubwa sana ya kuweza kudhibiti ili hali hii ipate kuondoka.

Suala jengine nije kwenye suala la deni la taifa, naipongeza serikali vile vile tunaliona deni la taifa nalo linapungua muda hadi muda. Kwa sababu tumetoka kwenye shilingi 398 bilioni hadi tukafikia kwenye shilingi 377.05 bilioni. Kwa hivyo, kuna upunguaji wa hili deni kubwa la taifa. Lakini nilikuwa nataka kujua hasa hili deni letu linafanyiwa ile *deep sustainability analysis* ili kujua vipi hili deni na tunajua kwamba deni letu ni *long term maturity*. Sasa je, ni miaka mingapi deni letu hili linaiva? Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho naomba aje anieleze na kwa mwaka *interest* yake inakuwa ni kiasi gani.

Vile vile nije kwenye suala jengine ambalo linahusiana na misamaha ya kodi. Kwenye kitabu hiki sijaona kipengele chochote ambacho kimeelezea suala la misamaha ya kodi na serikali tunajua kwamba inatoa hii misamaha. Kwa hivyo, tuiombe serikali kwa mwaka 2016/17 ni shilingi ngapi za misamaha ya kodi ambayo imetoa ikijumuisha na hizi ambazo zimetolewa juzi kwa wafanyabiashara katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile tuieleze serikali inapotoa hii misamaha ya kodi lazima iwe inafuatilia kwa makini zaidi ili kujua ile tija na lengo lililokusudiwa linaweza kufanikiwa. Kwa sababu kama tunavyoona kwamba Mhe. Waziri alikiri hapa kwamba hivi karibuni wafanyabiashara wamepatiwa misamaha ya kodi lakini bado bidhaa ziko juu. Kwa hivyo, ipo haja ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuandaa kitengo maalum cha kufuatilia hii misamaha ya kodi ili kuhakikisha kwamba lile lengo lililokusudiwa linaweza kupatikana na kama ikiona kwamba misamaha hii haileti tija basi mimi naishauri serikali isipewe kabisa. Kwa sababu lengo ni kumsaidia yule mtumiaji wa chini, lakini kama leo kuna mchangiaji mmoja Mheshimiwa alisema bei ya tende kabla ya Mwezi wa Ramadhani ilikuwa nyengine, ndani ya Ramadhani iko nyengine na wakati huku msamaha wa kodi tayari umeshatolewa. Kwa hivyo, utakuta wafanyabiashara wanafanya ujanja wanapata faida mara mbili zaidi, kwanza anapata faida ya ile biashara yake lakini ule msamaha wa kodi alioupata pia inakuwa ni faida nayo. Kwa hivyo, mimi

nafikiri ipo haja ya kuweza kuliangalia zaidi hili la misamaha ya kodi ili kuona inatumika vizuri kama lengo la serikali lilivyokusudia.

Nikitoka hapo kwa sababu muda si rafiki sana mimi nije kwenye kitabu hiki cha Makadirio ya Mapato nije kwenye suala la mapato. Kuna hiki kifungu cha mapato ya wafanyakazi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (*PAYEE*). Kwa mwaka 2016/17 ilikuwa ni shilingi 38 bilioni lakini safari hii iko shilingi 46 bilioni. Kwa hivyo, mimi hapa nilikuwa nataka nimuulize Mhe. Waziri katika haya mapato yaliyowekwa 46.7 je, yamezingatia ile *nine percentage* ya *income tax* au makadirio haya yalikuwa katika ile asilimia ya zamani ya 13%? Kwa hivyo, nilikuwa naomba atakapokuja atueleze kwa sababu tumeona hii ya mwanzo imepanda kuliko ile ya mwaka jana, lakini huku tunajua kwamba asilimia imeshuka ya *income tax* kutoka asilimia 13 hadi asilimia 9 kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kwa hivyo, Mheshimiwa atapokuja naomba maelekezo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ukija chini kuna kodi hii mahsusi ya tija (*TRA)*, kwa mwaka huu wa 2017/2018 pana *zero* kwenye ukurasa wa pili, lakini ukija kwenye ukurasa wa tatu kodi hii hii inajitokeza tena na kwenye mwaka 2017/18 kuna 8.7 bilioni. Sasa je, kodi hizi ziko tofauti au ni moja, kama moja kwa nini kuna *repetition* ya hivi vifungu. Kwa sababu huku ukurasa wa pili kodi hii ipo Kodi Makhsusi ya Tija, lakini kwa mwaka huu haikupangiwa pesa yoyote na unapokuja huku ukurasa wa tatu kodi ile ile au chanzo kile kile cha mapato, lakini utakuta kwamba kimepangiwa pesa. Sasa hatuelewi hapa, kwa hivyo atakapokuja naomba atueleze.

Mhe. Menyekiti, nikija chini kuna kodi ya fedha za miundombinu kifungu cha 11,41,108, ambapo kwa mwaka huu tunakadiria kukusanya hiyo kodi ya miundombinu ya shilingi 34.8. Lakini ukija kwenye kitabu huku kuna 34.9 kwa mujibu wa kitabu hiki cha bajeti. Kwa hivyo, ipi tuifuate, 34.8 au 34.9?

Halafu ukija ukurasa wa tatu chini huku kwenye kifungu cha 14, 15, 004; 14, 15,007 Kodi ya Nyumba za Serikali. Mhe. Mwenyekiti, naona katika mwaka huu kuna 00. Je, kumetolewa msamaha nyumba zile za serikali zisilipiwe, kwa sababu hakuna fedha yoyote ambayo itakusanywa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na nyengineyo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja tunaomba atupatie maelezo.

Nimalizie kwenye vyanzo viwili vya mapato katika ukurasa wa sita, cha kwanza ni 1422. 082, vile vile pako sufuri ambapo chanzo hiki ni kuchelewesha kusajili cheti cha kuzaliwa na tunaona wanaochelewesha vyeti vya kuzaliwa wanakwenda na wanalipa, lakini hapa hapana kitu.

Vile vile kwenye mitihani ya madereva nadharia 14,22,087 na hapo naona hapana kitu. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, atakapokuja waziri atueleze kwa nini vifungu hivyo viko sufuri. Lakini ukifungua ukurasa huo huo wa 21 kwenye Muhtasari wa Matumizi kwa mafungu ambapo hapa tunapata picha ya serikali nzima na namna ambavyo imetengewa fedha. Sasa ukiitizama kwa kweli mimi nina maeneo mawili hapa nataka nipatiwe ufafanuzi.

Jambo la kwanza utakuta kwamba kumbe bajeti ya Wizara ya Afya ni ndogo sana, kwa sababu mwaka jana walikadiriwa kupatiwa shilingi 67 lakini mwaka huu wamepatiwa shilingi 83. Lakini ukilinganisha na bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iko karibu shilingi 167 bilioni, hawa wana 83 tu, sawa na ongezeko la 15.5 bilioni. Kwa hivyo, utakuta kwamba bajeti ya Wizara ya Afya ni ndogo sana na wananchi wetu wengi sana wanahitaji hii huduma ya afya. Kwa hivyo, niiombe serikali katika bajeti inayokuja ya 2018/19 basi hili fungu la Wizara ya Afya liweze kuongezwa angalau likaribiane na hao wenzao wa elimu, kwa sbabu vituo vya afya vimeenea zanzibar nzima kwenye wilaya zote, mikoa yote.

Mwisho kabisa kwenye Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko katika ukurasa wa 21 Wizara ya Biashara nayo ndio wizara pekee sana ambayo ina fungu katika hii keki ya taifa. Kwa sababu keki ya taifa hii inagawanywa kwa wizara, ukiangalia Wizara ya Biashara wamepata *only* 7.2 *billion* na kazi hiyo kwa kweli ni kubwa sana huku ndiko kwenye viwanda, masuala ya biashara. Hata ukiangalia kwenye kitabu urari wa biashara, biashara zilizosafirishwa nje na bidhaa ambazo zimeingizwa ndani basi utakuta sisi ule urari wa biashara wa bidhaa na huduma si mzuri katika nchi yetu. Sasa ili kuuboresha basi ni vyema nao Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko waongezewe fungu, 7.2 milioni haiwezi kufanya kitu, kuna wajasiriamali hapa na hii ndio kaulimbiu tunaipigia kelele kila siku. Kwa pesa hizi naona ni kidogo serikali lazima katika bajeti ijayo iweze kutenga fedha.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nimalizie ukurasa wa 23 kwenye muhtasari wa Makadirio ya Matumizi ya Shughuli Kuu za Serikali, hapa shughuli kuu za serikali zimepangwa katika mafungu 10, sasa fungu Nam. 5 inasema kuhusu uhifadhi wa mazingira. Uhifadhi wa mazingira umetengewa shilingi 6.9 bilioni ambapo mwaka jana zilikuwa shilingi 13.7. Sasa nimuulize Mhe. Waziri kwa nini fungu la mazingira limeshuka kibajeti na ukiangalia kwamba maeneo mengi ya nchi yetu yameathirika na yanatakiwa yarejeshwe katika hali yake ile ya mwanzo. Kwa hivyo, ipo haja katika bajeti inayokuja suala la uhifadhi wa mazingira likapewa kipaumbele zaidi ili tuanze kudhibiti ile hali ya kuimarisha madhara ya tabianchi. Kwa hiyo, naomba na fungu hili lije liongezwe.

Jengine katika suala la michezo fungu 0.8 Michezo, Utamaduni na Dini. Mwaka jana walikuwa na 7.7 bilioni lakini mwaka huu kuna 2.7. Kwa hivyo, *five million* imeondoka hapa katika masuala yanayohudumia michezo, utamaduni na dini na ukizingatia kwamba sisi sasa tumejiunga katika shirikizo lile la *CAF;* kuna ada kule zinatakiwa zilipwe lakini kuna maandalizi yetu sisi wenyewe ili tusiwe kila siku tukiingia katika zile mechi tukawa tunapigwa bao. Kwa hivyo, ni vizuri fungu hili nalo katika bajeti inayokuja kwa sababu hii tayari tunaipitisha hapa na ni ngumu kuweza kuifanyia mabadiliko yoyote, lakini katika bajeti inayokuja tuwaombe wenzetu kwamba fungu hili nalo waliboreshe zaidi ili tupate na sisi kujipanga zaidi katika michezo ya kitaifa na kuna mpango wa kujiunga na shirikisho la dunia *FIFA.* Kwa hivyo, kwa *amount* hii kwa kweli kwa masuala ya michezo naona itakuwa ni ndogo haitoshelezi.

Baada ya maelezo hayo machache mimi binafsi na wananchi wangu wa Jimbo la Fuoni tunaunga mkono bajeti hii ya serikali kwa asilimia mia moja ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Yussuf Hassan. Sasa ninamuita Mhe. Ame Haji Ali na Mhe. Suleiman Makame Ali ajitayarishe.

Mhe. Ame Haji Ali: Mhe. Mwenyekiti ahsante, kwa ruhusa yako nami naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunipa uzima nikaweza kusimama mchana huu nami kuchangia machache sana katika hotuba hii ya Wizara ya Fedha kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwanza nianze kwa kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa umahiri na umakini mkubwa sana wa ukusanyaji wa mapato ambao unatupelekea leo hii tusimame hapa tukizungumzia bajeti ya trilioni 1.08 kutoka shilingi 848 bilioni. Hii ni hatua kubwa na ni ya kupigiwa mfano katika ukanda wetu huu wa Afrika Mashariki, niwaombe tu wale wasimamizi wote wajitahidi kuendelea kusimamia fedha hizi ili ziongezeke.

Sambamba na hilo niishukuru pia serikali kwamba bajeti hii imeonesha kwamba imemjali Mzanzibari kwa kila hali, kwa hiyo ni bajeti yao ambayo tunapaswa tuiunge mkono ili tuipitishe hapa ikafanyiwe kazi iwanufaishe Wazanzibari wote.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hayo kwa ruhusa yako niingie ndani kidogo katika hiki kitabu ili niweze kuona nami natoa mchango wangu, nianze na ukurasa wa 7 pale pana Sura ya Kumi na Tano kuna viashirio hivi vya ongezeko la mapato wamevitaja hapa wenyewe kwenye kitabu ni kilimo cha mazao, hoteli na mikahawa, ujenzi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Sasa mimi niishauri serikali kwamba kwa kuwa tumeviona hivi ndio vipaumbele vyetu vya ongezeko la mapato basi tuzisaidie hizi sekta ili ziweze basi hili ongezeko liweze kukua vizuri zaidi. Kwa sababu ukisema kilimo cha mazao maana yake wakulima hawa tuwawezeshe ili waweze kulima vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo hapa pana hoteli na mikahawa, ni vizuri kwamba wananchi wetu wengi huko vijijini wamehamasika katika eneo hili na wanaekeza katika eneo lile la hoteli na mikahawa. Lakini kwa bahati nzuri sana eneo hili linahitaji gharama kubwa sana za uendeshaji wake. Ni vizuri sasa na niombe serikali yetu kwamba iwe karibu na watu hawa ambao wana nia ya kuekeza ili wawapatie nyenzo kuona kwamba hii adhma yao inafikiwa na waengeze kipato.

Lakini chengine niende haraka haraka katika kitabu hichi niende katika ukurasa wa nane sura ya 17 pale wamezungumzia tena suala zima la hizi taasisi ambazo zinakusanya mapato tuanze na *ZRB, TRA* na taasisi nyengine. Kwanza mimi niwashukuru sana kwa ujasiri wao hawa na niwapongeze kwa jitihada kubwa ambazo zimetupelekea leo kukusanya mapato makubwa kiasi hichi ambacho tunayazungumzia hapa. Lakini ni muhimu sana katika taasisi hizi wakatanguliza uzalendo kwa sababu bado wapo baadhi ya maafisa ambao sio waaminifu na hawa wanashirikiana na watu ambao wanapenda kukwepa kulipa kodi na wanasababisha kupunguza mapato katika nchi yetu.

Niwaombe sana waendelee kushirikiana na wateja wao ili mapato haya yakusanywe ipasavyo na wao na wateja wao isiwe kuna uadui kati yao. Maana sasa inaonekana kwamba kuna maafisa wengine wanajenga dhana ya kwamba mpaka wale wateja wao wanakuwa na uadui kiasi ambacho kazi zao hazifanyiki vizuri. Nawaomba sana waendelee kushirikiana na hawa wateja wao ili kazi zao zaiendelee kufanyika vizuri.

Nikitoka hapo Mhe. Mwenyekiti, ninde moja kwa moja mpaka ukurasa wa 15 wa kitabu chake Mhe. Waziri wa Fedha hapa alizungumzia jambo zima linalohusiana na pencheni ya wazee wetu. Kwanza niipongeze serikali kuliendeleza jambo hili na kwa kweli ni jambo la kupigiwa mfano. Sasa niwaombe tu wahusika katika eneo hili bado kuna kasoro ndogo ndogo za wazee wetu hawa wengine wanakuwa hawatambuliki vizuri wengine hanastahiki hawapati hizi haki na wengine hawastahiki wanapata. Naiomba sana taasisi hizi ziendelee kuboresha kuhakikisha majina haya ili wale wanaostahiki kupata pencheni hii waendelee kupata na wale ambao hawastahiki basi wasubiri umri wao utakapofika nao waweze kuja kupatiwa.

Lakini sambamba na hilo naiomba tena serikali iangalie katika eneo hili kwa sababu ni eneo ambalo wazee wetu hawa kwa kiasi kikubwa wanalitegemea. Kwa hiyo, ni busara sasa kama basi mfuko utaendelea kutuna kidogo basi waongezewe wazee hawa kwa sababu sasa hichi ndicho kitegemeo chao ambacho kinawafanya waendeleze maisha yao ya kila siku. Sambamba na hayo Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naenda kwa haraka haraka kwa sababu ya muda wako Mhe. Mwenyekiti, sitaki uje unambie kwamba nimebakiwa na dakika moja. Sambamba na hapo mimi niende katika ukurasa wa 28 sura ile pale ya 58 hapa tumezungumzia suala zima la wazee.

Kwanza niwapongeze sana *ZECO* kwa jitihada zao wanazozifanya kutungarisha, lakini niwapongeze kwa mpango mzima huu ambao wameuanzisha hapa kwamba sasa wameazimia kwa makusudi kupunguza deni hili tunalodaiwa na *TANESCO*. Niiombe serikali iwape nguvu katika jambo hili deni hili limekuwa la muda mrefu na kwa kweli linaitia aibu nchi yetu. Kwa hiyo, tushirikiane kwa pamoja na watu wetu hawa wa *ZECO* ili tuhakikishe kwamba deni hili kama walivyoandika katika hichi kitabu kwamba hata ifikapo Julai mwaka huu wategemee kwamba tayari bilioni 44 hizi ziwe zimelipwa kweli ili tuondokane na adha na aibu hii ambayo ipo katika jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo sasa niende katika ukurasa wa 28 pale chini sura ya 61, hapa serikali imeweka vipaumbele ambavyo inataka kuvisimamia katika bajeti hii. Naomba tu niseme tu kwamba kuna vipaumbele vilivyotajwa hapa vikiwemo Elimu, Afya, Makaazi pamoja na maji safi na salama.

Sasa mimi nianze tu kwa kuishukuru serikali kwamba hili ni eneo ambalo linawagusa maisha ya watu wetu wote. Kwa hiyo, sasa wenye sekta hizi kwa mfano elimu niwashukuru wamefanya vizuri katika miaka iliyopita, lakini niwaombe tu bado katika jimbo langu kuna maeneo mengine majengo mengine yanahitaji kumaliziwa waje pale waje wanimalizie. Lakini kwa upande wa afya pia nilipokuwa nikichangia Bajeti ya Wizara ya Afya niliwaambia kwamba kuna baadhi ya vituo katika jimbo letu ni vibovu

mno vinahatarisha uhai wa hata hiyo afya yenyewe. Sasa nawaomba tu basi tushirikiane kwa pamoja tukafanye hayo marekebisho katika baadhi ya hivyo vituo.

Lakini pia katika upande wa upatikanaji wa maji safi na salama nawashukuru ZAWA. Jitihada kubwa wanafanya wenzetu hawa lakini nawaombe tu waendelee jitihada hizo kwa sababu bado tuna maeneo mengi sana ambayo tuna upungufu na ukosefu mkubwa wa maji safi na salama.

Mwisho, Mhe. Mwenyekiti, sasa katika mchango wangu niende katika azma hii ya serikali ya kujenga viwanja katika mawilaya yetu. Hii ni azma nzuri kwa kukuza michezo yetu huku tukitilia maani kwamba sasa sisi ni wanachama wa mashirikisho ya Dunia ya mpira na michezo mengine. Kwa hivyo, viwanja hivi ambavyo tumeazimia kujenga vitatukomboa sana katika kutufikisha mahali ambapo inaweza tukapiga hatua katika michezo. Lakini Waheshimiwa wengi hapa walipokuwa wakichangia jambo hili wameishauri na mimi naishauri serikali kwamba jambo hili basi ni vyema tukaliendeleza hatua kwa hatua. Viwanja hivi ni vingi wilaya zetu ni nyingi na uwezo wetu ni mdogo basi tuanze hatua kwa hatua wilaya kwa wilaya ili tuanze kujenga katika mfumo huu.

Ushauri wangu mimi binafsi naomba sana tuanze na Wilaya ya Kaskazini "A". Naomba tuanze huko kwa sababu tunao wanamichezo wengi lakini ukweli usiofichika ni kwamba hatuna kiwanja hata kimoja ambacho kinakidhi na kina hadhi ya kuendeleza michezo. Sasa tukianza pale nafikiri tutawasaidia sana wale wanamichezo wetu na naamini tutaibua vipaji vingi kutoka pale. Kwa hiyo, nashauri sana serikali itakapoanza zoezi hili la uanzaji wa ujenzi wa viwanja hivi basi tuanze ili tuweze kuona hali hiyo inatekelezeka hasa.

Sasa mimi nilikuwa nataka niseme haya tu kwa sababu mambo mengi haya tumeyachangia katika bajeti za wizara na nilikuwa nitilie mkazo baadhi ya maeneo hayo ambayo nimetaja kwa haraka haraka kwa kulingana na muda.

Sasa niseme tu kwa niaba yangu mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nungwi walionileta katika chombo hichi basi niseme naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe.Ame Haji Ali kwa mchangio wako na sasa nimwite Mhe. Suleimana Makame Ali na Mhe...

MUONGOZO

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kuniona nataka nisome Katiba ya Zanzibar kifungu cha 43(5). Mhe. Mwenyekiti inasema:-

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndiyo itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya Sera za Serikali ya ujumla na mawaziri chini ya Makamu wa Pili wa Rais itawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za kila siku za Baraza".

Mhe. Mwenyekiti, ghofu yangu na muongozo ambao naomba kwako nikiangalia leo tunatizama Bajeti kubwa ya Serikali wala sio Bajeti ya Wizara na mawaziri wengi hawapo katika viti vyao kusikiliza hoja za Wajumbe. Muungozo ninaoomba kwako je, tutaweza kupitisha na kuchukuwa hoja kikamilifu za serikali ili kuweza kuwajibu Wajumbe wakati viti viko vitupu. Naomba muongozo tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe ni kweli baadhi ya mawaziri hapa katika ukumbi walikuwa hawapo lakini sasa wamerejea ila niwaombe na mimi nawaangalia kwamba waweze kuchukuwa zile hoja za Wajumbe baada ya kumwachia waziri peke yake. Mwanasheria yupo na Makamu wa Rais yupo hapa. Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Mawaziri wanaohusika nao wachukuwe wajibu wao kama inavyotakiwa ili hoja za Wajumbe ziweze kuchukuliwa katika michango hii ya bajeti baada ya kumwachia Mhe. Waziri wa Fedha peke yake. Ahsante naomba tuendelee.

Mhe. Ahmad Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwepo hapa tukawa tunajadili Bajeti kubwa sana ya serikali.

Kwanza, awali ya yote nampongeza Mhe. Dr. Ali Mohamed Shein kwa usimamizi wa karibu sana wa wazira hii ambayo wizara inagusa misingi ya nchi yetu.

Baada ya hapo mimi mchango wangu zaidi utakwenda katika ukurasa wa 27 unaohusu deni la Shirila la Umeme. Mhe. Mwenyekiti, tukiri kwamba deni hili lilishitua nchi yetu na hasa lilipokuja, lakini si nchi tu lilibaraganya hasa na kujiuliza wawekezaji ambao ni msingi mkubwa unaosaida katika kutupatia mapato katika nchi yetu. Lakini kwa umahiri wa nchi yetu lilikubali kwa kiungwana deni hili na kwa mkokoto wa haraka haraka na kama jaduweli ya kitabu tutalipa karibu *40 billion point 6* na kuna salio kama la *20 billion*. Mambo ya kudaiwa ni mambo ya kisheria na ni mambo ya kawaida katika biashara wao *TANESCO* wanafanya *business* na sisi hapa tunafanya *business*.

Lakini ghofu yangu Mhe. Waziri kwamba hili ni deni la mlundikano kwa kipindi kirefu na pengine *unit* tunazozinunua kutoka *TANESCO* bei ni tafauti na tunavyouza na hii pengine inasababisha kwa huruma na mapenzi ya nchi yetu kwamba wananchi wasibebeshwe mzigo mkubwa Mhe. Mwenyekiti. Ikiwa juhudi serikali inafanya kwa umakini kabisa kuliondoa deni hili wasi wasi wangu uko hapa kadiri siku zinavyoendelea matumizi yangalipo na ukiangalia urari wa matumizi baina ya tunavyouza na tunavyotumia lazima kuna *gape* hapa. Hofu yangu hili deni lisije likarejea tena pamoja na juhudi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, lazima wachumi wa wizara waandae mpango makhususi ambao utakaotusaidia deni hili liwe linapungua kwa kiasi kikubwa na lisije likajitokeza kama lilivyojitokeza hivi sasa. Tunao rafiki zetu wawekezaji lilipotokezea wakaanza kutuuliza *what next* kwa kuwa wanajua hii ni nishati muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Kwa hiyo, mimi namshauri Waziri aunde mpango makhususi na wa muda mrefu utakaowezesha deni hili lisitune tena mpaka likawa *disaster* katika nchi yetu. Mpango ambao ukiwa utafuzu na utatekelezwa naamini kwamba hakutatokea tena kudaiwa na kuingia aibu kama ile ambayo imeingia, si aibu deni si aibu ulimwengu mzima hesabu ina-c*redit* na *debt*. Lakini linapokuwa kubwa tayari yule anaekudai anaanza kukushitua anakwamba hili bwana deni tutakuzuilia huduma hii na hii. Kwa hiyo, hili kwa upande wetu sisi lingetuharibia sana na Mhe. Waziri namuomba tu aandae mpango makhususi wa muda mrefu ili tuweze kulitatua deni hili.

Mhe. Mwenyekiti, katika mkokoto wa hesabu kuna 19 ambazo hizi zililikuwa zipo katika upande wa *payee (Pay as one)* hapa kitabu ni jambo rahisi kuondoa mkokoto kwamba sasa hivi tutalipa *40.6 billion* hadi Julai au hadi Juni. Mkazo Mhe. Mwenyekiti, uwekwe kwa makusudi timu yetu isimamie kikamilifu hii *18* bilioni iwe *contact* ihesabu *contact* kwamba mfumo huu unakosa unapata huu ili kusudi wananchi wetu waelewe hasa hii 18 bilioni imeshalipwa. Pamoja na deni la 2.5 la Taasisi za *Union* kusudi ziweze kulipwa au vyenginevyo inawezekana kufanya hesabu za vitabuni kwamba nakudai 55 nimekulipa *40 balance 20* kwa hiyo matokeo baada ya *reconsolidated* ya mwaka mmoja inakutwa 18 bado haijalipwa. Kwa hiyo, timu hii mimi naiamini na inafanya kazi vizuri ina wachumi mahiri lisimamiwe hili, kwa sababu limo kwenye mpango kwamba *18 billion* hii inaweza ikapatikana.

Kwa hayo, machache Mhe. Mwenyekiti, mimi bajeti naipongeza haina mashaka na mimi naita bajeti ya mkombozi kwa wanyonge. Kwa hayo, machache Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono asilimia mia chini ya mia bajeti hii haina matatizo na sina matatizo nayo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante naomba nifanye marekebisho kidogo nilikuwa nishamwita Mhe. Suleiman Makame kwa bahati nilimruka na nimkawamta Mhe. Nassor Salim Ali. Kwa hivyo, Mhe. Suleiman Makame Ali endelea na baadae atafuatia Mhe. Nassor Salim Ali

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa sina wasi wasi wowote kwa sababu najua muda upo wa kutosha wa kuweza kuchangia hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa sababu yeye ndie roho ya serikali kwa hotuba yake nzuri ya bajeti hii kuu ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo niende katika bajeti iliyopita. Mhe. Mwenyekiti, katika bajeti iliyopita niliwasikia wapinga maendeleo waliwahi kusema kwamba bajeti ile ilikuwa ni ndogo nakubali hilo ni kweli.

Lakini sasa wakadiriki kusema kwamba hata *Panadol* hatutaweza kununua katika kwenye bajeti ile iliyopita. Lakini Mhe. Mwenyekiti, walisau kwamba ule msemo wa kwamba "mbuzi anakula majani kwa urefu wa kamba yake". Mhe. Mwenyekiti, na ukizingatia kwamba bajeti ile iliyopita ambayo tunaendelea nayo hadi hivi sasa na udogo

wake iliyokuwa nao iliwalipa wafanyakazi mishahara yao hakuna aliekopwa na nyongeza imekuja na kila mtu ameshuhudia.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ukiangalia hapo hapo mpaka zile sekta za kimaendeleo ambazo kwamba zilikusudiwa kutekelezwa pia yametekelezeka huduma za jamii zimepatikana kwa bajeti ile ile na bajeti hii tunaendelea nayo ndio hiyo hiyo. Sasa Mhe. Mwenyekiti, sijui mara hii wapinga maendeleo hawa watasema nini kwenye *trillion* 1.4.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niende kwenye ukurasa wa 28 vipaumbele vya kitaifa. Mhe. Mwenyekiti, lengo la serikali ni kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma bora lakini niombe kitu kimoja hapa kwenye vipaumbele hivi wameorodheshwa mambo mengi mabarabara, maji, kila kitu. Kwa hiyo, niziombe zile wizara ambazo kwamba watapatiwa fedha hizo kwa wakati basi nao watekeleze yale mahitaji yanayohitajika yaliokusudiwa kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano tukitengeneza barabara zenye viwango na za uhakika kwa kipindi cha muda wa miaka kadhaa kwa mfano 10 na 15 na kuendelea mbele itakuwa sisi Zanzibar suala la barabara itakuwa tunalisikia kama ni ndoto. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tukitengeneza kwa kuripua ripua itabidi kwamba kila Rais atakae kuja tuwe tunatengeneza barabara.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kama tutadhamiria hasa ni ukweli kililahi taala kuhakikisha kwamba kama ni pesa ya mkopo ni pesa yetu sisi wenyewe ni pesa yoyote ile ya ufadhili basi ni kwamba kila kitakachofanyikana kama ni majengo ya serikali hizo barabara na mambo mengine basi yafanywe kiuhakika zaidi ili kuhakikisha kwamba tunakuwa kwenye ubora na ili kupeleka serikali yetu mbele kimaendeleo kwa sababu kuna mambo mengine tukiyafanya yanadumu kwa muda mrefu. Kwa vile tutafikia hatua ya kwamba nchi yetu iwe ni bora zaidi kwenye masuala ya kimaendeleo. Lakini tukifanya kuripua ripua kwamba kila tunachojenga tunajenga kwa kuripua ripua kuondosha njiani itakuwa hatofikia lile lengo tunalolikusudia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niseme mengi nayasema hayo machache, kwa sababu mengi nimeshayasema kwenye wizara zote nilizowahi kuchangia. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante kwa kujali muda wako. Anayefuata ni Mhe. Nassor Salum Ali.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini la pili nikupongeze wewe na kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo hotuba hii ya Waziri wa Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukuwe fursa hii kwanza kumpongeza sana Rais wetu mpendwa Dk. Ali Mohammed Shein. Vile vile na msaidizi wake mzee wetu baba yetu Balozi Seif Ali Iddi kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutuletea maendeleo kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze pia Mhe. Waziri kwa kazi nzuri anazozifanya pamoja na Katibu wake Mkuu na watendaji wote na kuweza kutuandalia ripoti hii ya fedha kwa mwaka 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa mchango wangu mdogo kwa kuanzia katika mazingatio maalum ya serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba serikali yetu imeanza kuzingatia na kuona umuhimu mkubwa wa mazingatio ya kuondoa tatizo la maji kwa wananchi wetu kwa Unguja na Pemba. Katika mazingatio ambayo ameweka ni kumalizia visima vilivyojengwa kwa msaada wa Ras Al Kheima kwa Unguja na Pemba. Nichukuwe fursa hii kuipongeza sana serikali kwa kuliona hilo kwa kufikiria kuliondoa tatizo la maji kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimefanyakazi kwa kupitia kamati yangu, lakini vile vile nikiwa kama mjumbe wa bodi ya ZAWA nalijua tatizo kubwa la maji kwa sehemu mbali mbali kwa Unguja na Pemba. Ndio nikasema kwamba nichukuwe fursa hii kuipongeza sana serikali kwa kutenga fedha hizi takriban 1.5 bilioni, ili kumalizia visima hivi vya maji. Kuna siku Mhe. Mwenyekiti, kama unakumbuka niliwahi kusema kwamba kuna msemo unaosema "maji yatekwayo ndio hayo", na leo serikali imesikia kilio hiki na imetenga fedha hizi ili kuweza kumalizia visima vile ili wananchi wetu waondokane na tatizo hili la maji. Kwa hivyo, hongera sana serikali yetu, hongera Dk. Shein hongera serikali ya CCM, haya yote ni katika kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, katika kuangalia katika maeneo ya vipaumbele ambavyo vimewekwa na serikali yetu kwenye bajeti hii ya mwaka 2017/2018 ni kuendeleza utalii. Mhe. Mwenyekiti, utalii ndio tegemeo kubwa la kuweza kuingiza fedha na kuenea shughuli zetu zote za serikali na kuweza kupata mapato.

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ya Utalii tunaitegemea sana katika kuendeleza na kuutangaza utalii wa Zanzibar. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nitowe pole kwa familia ya Katibu Mtendaji aliyepita ndugu yetu kaka yetu Mzee Ferouz Mwenyezi Mungu amjaalie alale mahali pema huko aliko peponi, amjaalie maisha mema huko aliko.

Mhe. Mwenyekiti, toka kufariki kaka yetu Ferouz ambaye ndiye alikuwa Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii, Kamisheni ya Utalii imeyumba na kwa kweli serikali lazima iangalie utendaji mzima wa Kamisheni ya Utalii. Nimuombe sana Mhe. Rais na wasaidizi wake kuhakikisha kwamba tunaboresha na kumuweka mtendaji ambaye ataendesha Kamisheni ya Utalii vizuri na vile serikali ambavyo imejiwekea malengo ya kuendeleza utalii, kwa faida ya taifa letu na kwa faida ya kuleta maendeleo kwa nchi yetu.

Nikitoka hapo Mhe. Mwenyekiti, nije katika kuimarisha miundombinu na uingiaji nchini kwenye barabara na nishati. Niipongeze serikali katika kuangalia na kuweka kipaumbele zaidi katika suala hili la kuimarisha miundombinu hii.

Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hiki imeeleza hapa ununuzi wa meli ya mafuta na meli nyengine ndogo, haya ndio maendeleo ambayo tunayataka. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Rais wetu, Rais wetu anajali wananchi wake, anaijali nchi yake na ana mapenzi na nchi yake na hawa ndio viongozi tunaowataka, viongozi hawa ndio ambao wanatuletea maendeleo kwa nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Rais wetu Dk. Ali Mohammed Shein chini ya kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi amekuwa akifanyakazi kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nassor Salim Ali naomba usubiri kidogo. Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwatangazie kama kuna Waheshimiwa Wajumbe walioko nje ya ukumbi huko ambao wako walioleta orodha yao ya kuchangia hapa, nawaomba wafike kwa sababu muda ungalipo waweze kutumia muda huu ili baadae tuweze kuendelea na hatua nyengine. Kwa hivyo, kama wako nje ya ukumbi basi wafike hapa kabla hajamaliza Mhe. Nassor Salim tuweze kuendelea. Ahsante Mhe. Mjumbe, endelea.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, niendelee hapo hapo nilipomalizia kwa kuweza kumpongeza Rais wetu pamoja na msaidizi wake mzee wetu mzee Balozi Seif Ali Iddi.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ni ambayo ina visiwa viwili vya Unguja na Pemba na Zanzibar ni nchi ambayo tofauti na wenzetu Tanzania Bara. Bara wenzetu wana maeneo makubwa, lakini vile vile ni nchi ambayo Bara ina milima na mabonde. Lakini Zanzibar visiwa hivi vimezungukwa na bahari. Katika kipaumbele ambacho tumepewa ni katika kuzingatia pia mazingira. Mhe. Mwenyekiti, hali ya mazingira kwa visiwa vyetu kwa kweli sio vizuri. Kwa hivyo, nichukuwe fursa hii kuipongeza sana serikali yetu kwa kuliona hili ili kuweka katika hali ya mazingira mazuri ya visiwa vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala la utawala bora, uimarishaji wa taasisi na kukabiliana na maafa ambayo imezungumzia suala hili la mazingira. Mabadiliko pia ya tabia ya nchi, uwekaji wa mji katika hali ya usalama. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hivi punde tukio ambalo lilitokea katika kukabiliana na suala la kiusalama kwa watalii ambao wanakuja Zanzibar, ambapo utalii ndio tegemeao la Zanzibar. Tukio lile limeleta taswira mbaya, lakini kwa hali halisi na kuuona umuhimu wa suala hili la utawala bora na usalama wa nchi serikali imeliona hili.

Kwa hivyo, mimi niiombe sana serikali ili kuhakikisha kwamba inaimarisha vikosi vyetu na hapa inaonesha kwamba serikali imedhamiria vizuri kabisa kwa nia njema, ili kujenga vikosi vyetu hasa ulipoona kwamba inaimarisha kuweza kuzijengea nyumba za kisasa vikosi vyetu vya KMKM, Mafunzo na JKU. Suala hili kwa kweli ni wajibu wetu sisi kama viongozi kuiunga mkono serikali yetu kwa kuweza kufanya mambo mazuri ambayo yanaleta tija kwa wananchi wetu kwa kujenga usalama wa nchi yetu. Hongera sana Dk. Shein, hongera sana Mhe. Balozi Seif. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa suala zima kama wenzangu walivyolizungumza. Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni kaka yangu Mhe. Yussuf Hassan alilizungumza hili, Mhe. mzee wangu mwana Simba nambari 2 mzee Ali Suleiman Shihata Mjumbe wa Kamati

maalum wa Timu ya Simba, akiongozwa na Abdalla Maulid Diwani kwa uchungu na mapenzi ya nchi yao na furaha waliyonayo kwa kuungana na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kulipokea kwa mikono miwili kwa furaha kubwa uanachama wa chama au Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (*CAF). CAF* wananchi wanaijua maana yake, lakini sio ile nyengine ambayo mnaijua nyinyi, hilo watalijua wao. Sisi tunajua *CAF* ni Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika.

Mhe. Mwenyekiti, fedha ambazo zimetengwa na huko tunakotoka kwenye bajeti ya mwaka 2016/2017, lakini bajeti iliyotengwa kwa mwaka 2017/2018 na mwaka 2018/2019 kila mmoja amepata *shock* ya utengwaji wa bajeti hii, hasa ukizingatia Zanzibar tumepata uanachama wa Shirikisho hili la Soka la Afrika. Lakini vile vile tukitegemea na tukiwa na matumaini ya kuwa wanachama wa *FIFA*. Kwa hivyo, kama walivyotangulia wenzangu na mimi natilia mkazo kwamba huko tunakokwenda tuboreshe bajeti yetu hii, ili yale malengo au matumaini tuliyonayo tutakapopata uanachama wa *FIFA*, au tukianza kuwa katika maandalizi ya mashindano haya ya Shirikisho la Mpira wa Afrika, basi tuwe tunafanya maandalizi mazuri na tunaandaa timu zetu ili kuleta ushindi na kuleta sifa kwa nchi yetu. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri alizingatie hili na alifikirie ili tutakapokuja kwenye bajeti ya mwaka 2018/2019 basi tuwe tumeboresha bajeti yetu hii.

Mhe. Mwenyekiti, michezo ni afya na michenzo ndio iko katika utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nimalizie kwa kusema kwamba haya yote mafanikio tunayoyapata ni katika utekelezaji vyema wa ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kufanikiwa kuwa wanachama wa FIFA, kufanikiwa kuwa wanachama wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika yamo katika ilani ya Chama cha Mapinduzi. Wale ambao wanasema waseme, wanaonuna wanune lakini Chama cha Mapinduzi kinafanya vizuri kwa kupitia viongozi wetu chini ya Jemedari Dk. Ali Mohammed Shein na msaidizi wake mzee Balozi.

Lakini la mwisho Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo ambalo limekuwa likijitokeza mara kwa mara, ndani ya wizara zetu na ndani ya taasisi zetu. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri hili alichukuwe na alifanyie kazi na bahati nzuri Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imeshatoa ushauri huu na mimi nikiwa kama mwakilishi na mimi nimeliona hili, basi Mhe. Waziri alichukuwe kwamba wahasibu wetu na washika fedha wetu wa mawizara na taasisi mbali mbali wawe wanafanya mabadiliko kila kipindi kikifika. Isiwe mtu anakaa miaka 10, 15 au 20 yuko pale pale, wewe kila mwaka ukienda yuko mhasibu huyo huyo, mshika fedha huyo huyo. Pale ndio kunajenga taswira mbaya. Kwa hivyo, kuwe na mabadiliko leo baada ya miaka mitatu, minne, au mitano anaondoshwa anakwenda wizara fulani, au anaondoka huku anakwenda wizara fulani. Isiwe tu mtu huyo huyo anakaa miaka 10 au 15 yuko hapo hapo, tunajenga mizizi ambayo inaleta athari katika utumiaji wa fedha za serikali na katika taasisi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii, na niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wenzangu, kwa sababu haya yote ni katika kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi na serikali yetu chini ya viongozi wetu kwa maendeleo ya wananchi wetu,

basi tuiunge mkono bila ya kupiga buti hata moja. Baada ya kusema hayo nakushukuru sana, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, muda upo wachangiaji wanaruhusiwa kuchangia, majadiliano yanaendelea. Kwa hivyo, kama kuna mjumbe mwengine ambaye kuwa hajaleta jina lake, anaweza kuleta akaweza kuendelea kuchangia. Majadiliano yanaendele.

Kwa hivyo, naomba nimwite Mhe. Ali Khamis Bakar Mwakilishi wa Jimbo la Tumbe, mheshimiwa endelea.

Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi mchana huu kuweza kuchangia Wizara ya Fedha ambayo iko mbele yetu na tunaijadili kuhusiana na bajeti hii nzima ya serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha siku ya leo tukakutana hapa, tukiwa wazima na afya njema. Vile vile namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tumalize Baraza letu hili tukufu kwa awamu hii, tukiwa wazima na afya njema na vile vile tumalize swaumu zetu ambazo tunaendelea nazo za mwezi Mtukufu wa Ramadhani akiwa Mwenyezi Mungu amezipokea vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nianze kwa kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo imefanya mengi ndani ya kipindi chake hiki cha miaka mitano ambayo tunakwenda nayo katika muda mfupi sana. Mhe. Mwenyekiti, tumejionea wenyewe serikali yetu jinsi ambavyo imewajali wananchi wake kwa kuboresha mambo ambayo yamo ndani ya jamii kwa hatua kubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze hapa Wizara ya Fedha kwa kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kazi kubwa ambayo wameifanya na moyo mkubwa ambao wanao wa ujasiri kuweza kusimamia mapato yetu yaliomo ndani ya serikali na kufikia hatua hii ambayo sasa hivi tunatarajia kufika na *In Shaa Allah* Mwenyezi Mungu atujaalie tufikie lengo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nikiendelea nimpongeze tena Mhe. Waziri kwa kutuona na sisi kilio chetu watu wa Micheweni. Nilipokuwa nikichangia kwenye Wizara ya Fedha kabla ya bajeti hii kuu nililisema hili. Lakini vile vile nilikuwa sijaangalia vizuri Mhe. Mwenyekiti, lakini baada ya muda tu Mhe. Waziri yale malalamiko yangu ama maombi yangu nimshukuru kwamba aliyasikia na akayafanyia kazi, hatimaye nimeona mpango mahususi ambao umeshaandaliwa kuweza kupata watu wa Micheweni *ATM* ili kupunguza mirundikano ya kule Wete na Chake Chake. Lakini vile vile kupunguza ule mwendo ambao watu walikuwa wanaupata. Pia kwa kwa kutuona sisi ndugu zake tuna kilio kikubwa hiki cha muda mrefu ambacho hata wazazi wetu walikuwa wakipata shida sana, ambapo ilikuwa ikiwafanya wanapopata ile pesa basi hawajui namna gani ya kufanya, lakini almuradi tu Mwenyezi Mungu kajaalia na sisi watu wa Micheweni tumeonekana sasa hivi kuna mpango mzuri na mahususi ambao umeshaandaliwa na Mhe. Waziri kuweza kutuwekea *ATM* hii.

Mhe. Waziri hongera sana na nikuambie tu kasi hiyo hiyo na wenzetu ambao watakuwa wanahitaji hili jambo basi uwaone kwa mara mbili zaidi, kwa sababu tumeona tunapokwenda mabenki yote yamejaa watu wanakosa. Mtu anakwenda pale kwa muda ambao pengine ni mfupi sana kuweza kufanikisha jambo lake na akarudi nyumbani anapata kuchelewa kwa msongomano wa watu, lakini zitakapoendelezwa kuwekwa hizi *ATM* katika mazingira tofauti au mikoa tofauti na wilaya, basi itapunguza idadi kubwa ya watu ambao wanakwenda kukaa sehemu moja na badala yake iwe wanaweza kupata katika sehemu zao za mawilaya.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kuhusu habari ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji. Mhe. Mwenyekiti, mimi hawa niwapongeze kuanzia Mhe. Waziri, Naibu Waziri na wajumbe wake wote ambao wanaisimamia wizara hii kwa juhudi kubwa ambazo wanazifanya kuona na wao yale ambayo wananchi wanayahitaji, basi kwa kasi kubwa na wao wanaweza kufanikisha hatua wa hatua.

Lakini tu niwaambie kwamba Mhe. Waziri hapa ambapo kama tunawapata hawa wakandarasi kuweza kutujenga barabara zetu basi nimuombe sana wasimamie kuweza kuona barabara zetu ziwe zina kiwango, wasikae tu kapigwa dana dana wakifika wakakabidhiwa na wao wakaridhika kwamba barabara ile ishaisha, mimi niwaambie Mhe. Magufuli yuko karibu yeye mwenyewe ana zana zake ambazo anakagulia barabara basi Mhe. Waziri na Naibu nafikiri atakuwa yupo ananisikia hapa hebu nendeni kwa Mhe. Magufuli mkifika mmwambie tupe hizi zana ambazo unakagulia barabara na sisi tunataka kuangalia barabara zetu zilizoko Pemba na Unguja, alimradi na sisi tuone zinafikia hatua nzuri. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, tumeona sote katika mvua ambayo imepita barabara nyingi zimenyofuka, nyengine zimechimbika na nyengine zimekatika kiasi ambacho barabara zile ukiziangalia hata miezi mitatu nyengine hazijapata.

Lakini kuna nyengine zimekaa mwaka tu zimeshaanza kukatika kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba hapa wakati wa kukabidhiana hii mikataba basi waangalie kwanza wale watu wanaokuja kutujengea hizi barabara kwanza wawe na *Guarantee* yaani muda gani ambao labda pengine likitokezea tatizo wao ndio watawajibika badala ya kuwajibika Serikali. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri na hili nalo aliangalie wakati wa kujengesha hizi barabara na wakati wa makabidhiano waone kwamba kunakuwa na vitu maalum ambavyo wanakabidhiana kwa maandishi kwamba hii barabara ikifikia muda huu basi kama kutatokezea lolote wao ndio wawe watengenezaji.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye Wizara ya Afya kwanza nimshukuru Rais wa Zanzibar nimpongeze kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kuijali nchi yake, lakini vile vile kuwajali wananchi wake kwa kuweza kutujengea hospitali kubwa nyengine za ghorofa, nyengine za chini. Lakini vile vile kwa kutufanyia katika matibabu ambayo wananchi tunayapata sasa hivi kwa kasi kubwa na yenye unafuu, hapo nyuma sote tumejionea kadhia iliyokuwepo kubwa juu ya wananchi wakati wanapokwenda mahospitali katika kujitibu, kwa mfano wazee wetu akina mama walikuwa wanapata usumbufu mkubwa sehemu za kulazia wagonjwa kwa upande wao akina mama za

kujifungua zilikuwa finyu, lakini vile vile wakifika katika maeneo yale walikuwa wana ada maalum waliyokuwa wanatozwa.

Lakini tumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwajali wananchi na kuwajali wazazi wetu basi hili limeweza kuondoka na badala yake sasa hivi tunatumia matunda yetu tukiwa na hali nzuri, lakini vile vile wazazi wetu wakijisikia vizuri wakati wa kujifungua.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hapa hapa mimi niseme kidogo kusema na Wizara ya Afya na wafanyakazi wote kwa ujumla, Mheshimiwa Mjumbe aliyepita kama mtu wa tatu nyuma nilimsikia akilisema hili kwa msisitizo lakini na mimi naomba nitilie nyama kwamba baadhi ya Wafanyakazi ambao wanakwenda katika Wizara zao ama katika sehemu zao husika ambazo wanafanyakazi basi wanachelewa, mimi juzi tu nimekwenda Hospitali lakini tumefika pale daktari wa lilie tatizo ulilonalo wewe unafika mwanzo kuliko yeye ambae anapokea mshahara. Ingawa wewe tayari lazima ujihimu kwa sababu unaumwa lakini na yeye ikifika ile angalau saa moja au saa moja na nusu basi anafika kwa wakati kuweza kufanikisha. Lakini mnaweza kufika pale Mhe. Mwenyekiti siku nyengine masaa matatu mazima kutoka asubuhi saa moja mpaka saa tatu basi mfanyakazi hajafika unabakia na ukija sasa foleni ni kubwa.

Mhe. Mwenyekiti mimi nimejionea huku Unguja kuna king'ora juzi mimi nilikuwa sikijui maana yake nikauliza nikaambiwa kwamba kile king'ora asubuhi kinapigwa saa moja na nusu wanahimizwa watu waende kazini, ikifika muda huo na kuna saa tisa nikaambiwa ni sehemu ya watu kutoka kazini, kuna na chengine saa kumi na mbili kuonesha kwamba cha kunywea uji. Niipongeze sana Serikali kwa kutumia njia ile waliyoifanya kwa kule Pemba hichi King'ora hakipo lakini king'ora cha mtu ni yeye mwenyewe juhudi yake, lakini vile vile niseme kwamba wale wakuu wa hizi taasisi basi kuwe na taimu maalum kwamba mtu anapofikia muda huu hajafika kazini pasipokuwa na sababu maalum labda pengine amefiwa au kuna dharura ambayo ni kubwa iliyomfanya muda ule amechelewa basi kuwe na uwajibikaji.

Kwa sababu kuna wengine hupata nafasi ya kusema mimi pengine nakaa mbali lakini ile mbali isiwe sababu kwa sababu ukisema unakaa mbali wewe unatakikana ujihimu kuanzia asubuhi utoke mapema ili mradi ule muda ambao unatakikana ufike kazini basi ufike kwa wakati, lakini wengine Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyoona unafika pale unamsubiri mhudumu unaendelea kubaki masaa yaliyopo mhudumu yule hajafika na matatizo yanabakia. Kwa hivyo Mhe. Waziri nikuombe sana na hili nalo liangaliwe.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwa Wizara ya Nisharti, Maji, Ardhi na Mazingira nimpongeze sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi kubwa ambazo wanazifanya juu ya kuondolea wananchi wake shida nyingi ambazo walikuwa wanazipata, kwamba sasa hivi Alhamdulillahi lile tatizo kubwa lililokuwepo ndani ya visiwa vyetu viwili Unguja na Pemba kwa kiasi kikubwa limepungua, najua kama kuna baadhi ya sehemu nyengine haya mambo hayajakaa vizuri lakini ndio safari na mambo yote hayakamiliki kwa siku moja, lazima kuwe na taratibu maalum leo panafanywa hapa kesho pengine na keshokutwa kwengine. Kwa sababu

Mhe. Mwenyekiti hivi mimi ninavyokwambia kwamba katika kilio kikubwa ilikuwa mimi ndani ya Jimbo langu la Tumbe nashukuru nilichimbiwa vizima viwili ambavyo vilikuwa vikitoa maji katika shehia mbili Tumbe ya Mashariki na Magharibi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha kwanza tulikaa kwa muda miaka miwili mpaka mitatu maji yale yalikuwa yanatumika lakini yalikuwa ni mabaya kwa sababu maji yaliyopatikana katika kipindi kile yalikuwa ni maji ya fuwe, ilikuwa ukiyachota ukiyaweka kwenye ndoo basi masaa matano tu kuna kama vilui lui vinaita. Nashukuru Wizara imeliona hili na kilio chetu tukakipeleka kwa Wizara basi kisima kile kimefungiwa na kuchimbwa chengine pale Saninga sasa hivi Alhamdulillahi katika Jimbo langu la Tumbe nashukuru sana suala la maji kwa kweli limekamilika asilimia sabini na tano zimebakia karibuni ishirini na tano, na hizo ishirini na tano zilizobakia kwenye mia nina imani kwamba kwa bajeti hii tunayokwenda nayo Mhe. Waziri akiwaingizia pesa tu kila Wizara yake basi ishaallah tutafanikisha na tutafikia hatua ambayo ni nzuri.

Lakini Mhe. Mwenyekiti katika Wizara hii hii nigusie kidogo kwenye suala la umeme, juzi hapa tulipokuwa tukichangia baadhi yetu tumegusa baadhi ya sehemu kidogo lakini na leo na mimi naomba nigusie kidogo nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba awaongezee watu wetu wa umeme hii pesa, kuona kwamba kuna baadhi ya mambo sasa hivi wananchi wanapata shida mtu akitaka kuunga umeme kama yuko nyumba ya tatu labda au kuna nyumba nne tuseme katika kijiji ambacho kimeanzishwa, kwa sababu tunaona Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wetu wengi masikini tunakimbilia maeneo ambayo ni ya sehemu za shamba shamba. Sasa shamba unaanza wewe anakuja ndugu yako anakuja baba yako yaani mnakaa watu kama watano au sita tuombe kwamba Mhe. Waziri kwamba wawaone wale watu na wao wanahitaji huduma wawapelekee nguzo za umeme wasiwaachie kwamba mtu yule aweze kuunga umeme mwenyewe na kuunga umeme mwenyewe ni vipi Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba ajigharamie nguzo tatu nne kupeleka katika lile eneo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri na Naibu wake wananisikia kwamba watusaidie wale wananchi wetu wawapelekee zile nguzo badala yake wao waachiwe kazi moja tu ya kuunga ule umeme kwa zile gharama za *Loop hole* lakini wakiwaambia kwamba mpaka nguzo wagharamie wao kwa kweli inakuwa shida, watu wanapata tabu kusema kweli hawawezi ni wanyonge, mtu kahangaika labda kenda mwani mabavua matatu siku nyengine mwani ndio kama hivyo tunavyoona siku nyengine unakuwa haufikii lengo, pengine unapigwa na mvua au siku nyengine hajauza lakini anataka atie umeme anafika pale anaambiwa laa hapa bwana wewe mpaka upate milioni tatu au mbili. Kwa kweli umeme anautaka lakini akitizama na gharama zinakuwa kubwa anashindwa kufanikisha suala lile. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri waone watu hawa tulio kwenye vijiji tuwapelekee hizi nguzo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hili sijalifanyia uchunguzi lakini nasikia tu kule Bara wenzetu wakiiona tu nyumba imeshajengwa basi hapo hapo wanakupelekea laini unabakia wewe mwenyewe kuweza kuunga, sasa kama hili kule lipo na sisi nchi yetu ndogo hii kwa hivyo niwaombe tu watu wahusika zaidi. Mhe. Waziri na Naibu Waziri mnanisikia

kwamba hapa na wao watu walio katika vijiji tuwaone kwa mfano kama mimi ndani ya jimbo langu kuna sehemu moja inaitwa Uwaani hichi ni kijiji kipo muda mrefu. Lakini vile vile kuna sehemu nyengine ndani ya jimbo langu la Tumbe tunaita Mamoja hii Mamoja ishapata umeme, lakini kuna nusu kwa nusu wengine hawajapata imetoka tu Shumbaviamboni ikafika pale sasa pale kama napo tutaanza kutandaza zile nguzo kwa kupitia lile eneo la Uwaani nao watashawishika kuunga haraka kuona na wao wanapata lakini vile vile mapato ya nchi yetu yanaongezeka. Kwa sababu yule akienda kununua umeme elfu ishirini tayari kodi imeshapatikana mambo yameshaingia kwa hivyo tunaendelea kuongeza kile kipato.

Lakini vile vile wananchi wanapungua zile shida kwa sababu wakati mwengine mtu huu umeme unamdhalishia anapata kuuza *juice*, wengine wanapata kufanya masuala mengine tofauti wengine wanaweza wakaweka kiwanda pale cha kuchoma vyuma akaweza kupata angalau kuganga njaa. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba haya masuala hebu tuwafanyieni wananchi wetu wajisikie *Comfortable* wajione kwamba nchi yao wanaipenda lakini na vile vile na wao wanapendwa kuweza kupelekewa hizi huduma ambazo tunazo, najua kama mnayafanya haya lakini mimi ni msisitizo kuwakumbusha zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi isipokuwa na mimi nataka nichangie hii Wizara kuona kwamba nisikae kimya na ni jambo ambalo tunalo hapa wajumbe wote tunatakiwa tuijadili na baadae tuipitishe, niwaombe wenzangu tuendelee kuichangia hotuba hii na mimi naunga mkono asilimia mia moja. Ahsante (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Doholo kwa mchango wako na sasa ninamuita Mhe. Shaib Said Ali, akifuatiwa na Mhe. Mwanaasha Khamis Juma.

Mhe. Shaibu Said Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuniona kunipa fursa hii kuichangia hotuba hii hotuba ambayo kwetu sisi ni dira na ndio hotuba ambayo italeta ufanisi katika masuala yetu yote ya utendaji wetu w kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kusema kwamba wazee walisema kwamba peupe hapaoshwi nasema hivyo kusema kwamba hotuba hii ni hotuba safi, na hotuba yenye mwelekeo kwa hivyo haina haja ya kwamba ina nongo kwamba tuioshe ni hotuba iliyo nyeupe na nilisema kwamba peupe hapaoshwi. Baada ya shukurani hizo kwa Mhe. Waziri nianze hotuba yangu kwa kusema kuwa nije katika suala la mapato.

Mhe. Waziri mimi mchango wangu sana utakuwa ni ushauri kwako kwa sababu mengi yameshazungumzwa mengi yameshasemwa naamini iliyobakia sasa ni utekelezaji tu, kwa hivyo nije katika suala la mapato, mimi ushauri wangu Mhe. Mwenyekiti nimuombe Waziri kwamba suala la mapato aangalie sana sehemu ambazo mapato yanavuja, kwa sababu bado mapato yetu kuna nyanja nyingi ambazo zinavujisha mapato hususan kuna sehemu za bandari bubu hizi bandari zinavujisha mapato kwa asilimia kubwa sana kwa kuongeza mapato uchumi wetu. Mhe. Waziri kuna watu ambao hawapendi maendeleo huzitumia bandari bubu katika kupitisha bidhaa zao kwa kukwepa ushuru, kwa hivyo mimi nimuombe Mhe. Waziri kwamba bandari hizi aziangalie ili mapato yetu yazidi

kukua. Mhe. Waziri sehemu hizi kwa kule kwetu Kisiwani Pemba ndio sehemu ambazo mpaka uchumi wetu mkuu huwa unapitishwa katika sehemu hizo, kwa hivyo mimi nimuombe kwamba sehemu hizi aziangalie kwa jicho kubwa sana ili kama inawezekana basi sehemu hizi zijulikane na zifungwe kabisa.

Mhe. Mwenyekiti sasa nije kwenye mfumko wa bei mimi kama ninavyozungumza kwamba kubwa kwangu mimi itakuwa ni ushauri nimuombe Mhe. Waziri kwamba suala hili alichunguzwe sana kwa sababu bado wananchi wetu wa vijijini suala la mfumko wa bei hawajui maana yake nini, kwa hivyo mimi ningeomba kwamba suala hili wananchi wetu wa vijijini waelezwe na wajue mfumko huu wa bei unatokezea wapi na kwa nini nchi yetu inakuwa na mfumko wa bei kila baada ya uchao.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwenye viashiria vya umasikini hotuba hii imeeleza kwamba viashiria vya umasikini baada ya uchunguzi vikawa vimepungua sana vijijini, lakini nimuombe Mhe. Waziri kwamba suala hili alifanyie utafiti kwa sababu bado wananchi wetu wa vijijini ni masikini sana, kwa hivyo inavyoambiwa viashiria vya umasikini vimepungua mimi bado nasema suala hili lifanyiwe utafiti kwa sababu bado umasikini vijijini wazee, vijana, umasikini umezidi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niende kwenye suala la mtambuka au ugatuzi mimi namuomba Mhe. Waziri kwamba suala hili liangaliwe na mimi ninaloomba kwamba suala hili liwe kama ni majaribio kwa muda huu ili liangaliwe, hawa waliopelekewa mtambuka kwa baadhi ya Wizara Je, watatekeleza vipi suala hili litakuwa na ufanisi, litakuwa zuri, litajenga jamii au litafanya nini kama halikuwa na ufanisi basi naomba zile Wizara ambazo zimepitia katika mtambuka basi naomba zirudishwe katika Wizara zake ili wananchi wapate ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije masuala ya bandari uchumi wetu mkubwa sana unategemea bandari, mimi ninaloliomba kwamba zile bandari za Pemba Waziri muhusika azifanyie ukarabati hususan Bandari ya Mkoani, Wete, Wesha ili bandari hizi ziweze kuleta uchumi, kwa sababu bandari hizi vile zinavyokaa ni kwamba wananchi hawazitumii ipasavyo kwa sababu wakati mwengine kule haziji hata meli kubwa hutaka abiria wawe wengi lakini huwa ni kidogo kutokana na hali, kwa hivyo uchumi wetu wa ndani saa nyengine nao pia hukosesha mapato.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama nilivyosema kwangu mimi ni ushauri badala ya hapo nije katika suala la uzalilishaji wanawake na watoto, suali hili limezungumzwa sana sana na suala hili mimi nasema kwamba wakati mwengine hata uchumi wetu unapungua kwa suala hili, kwa sababu saa nyengine mama anafikiria au wazazi wanafikiria baada ya kufanya masuala ya kiuchumi huwafikiria watoto wake walio skuli, huwafikiria watoto wake walio chuoni, huwafikiria watoto wake walio matembezeni watafikwa na hatua gani kwa suala hili. Kwa hivyo mimi ninalomuomba kwamba suala hili bado lipewe kipaumbele ili wananchi wapate kufanya kazi zao waongeze masuala ya kiuchumi.

Halafu pia kuna suala la kwamba takwimu zilizoletwa katika masuala haya ya udhalilishaji mimi naona bado Wizara ifanye tena utafiti kwa sababu mimi naziona ni

ndogo sana sana ukilinganisha, masuala ya udhalilishaji watoto maskulini, vijijini, katika vyuo ni madogo sana. Kwa hivyo mimi naomba suala hili lifanyiwe tena utafiti ili ijulikane hasa ni watoto wangapi wanadhalilishwa na wanawake wangapi wanadhalilishwa wanaonyang'anywa haki zao, walionyang'anywa waume zao na kadhalika, kwa hivyo mimi naomba suala hili lifanyiwe utafiti zaidi ili wananchi waweze kulijua.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nije katika masuala ya kijamii yaani masuala ya afya nafikiri Wizara ya Afya imeshapitisha bajeti yake kwa maana hiyo naiomba tu mimi kwamba Mhe. Waziri atakapopata fedha basi ili kuondoa mambo ambayo yako katika Wizara ya Afya basi naomba zile changamoto aweze kuziondoa, kwa sababu katika Wizara ya Afya kuna changamoto nyingi sana majengo mabovu, wafanyakazi ni kidogo, madawa hospitali hakuna, vifaa hakuna kwa hivyo mimi naomba tu kwamba Mhe. Waziri wa Fedha atakapofika Wizara ya Afya hili suala alione zuri ili aondoshe.

Halikadhalika na Elimu ni hivyo hivyo kwa maana hiyo elimu si sawa sawa na Wizara ya Afya kwamba maskulini nako vile vile kuna changamoto nyingi kwa hivyo naomba tu Wizara zitakapopata fedha hizi ziweze kutumia kwa yale mahitajio ambayo wamepewa Mheshimiwa mimi kwa hayo machache yangu machache na mimi nisema tu nitoe mchango wangu nanilitaka kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake na naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia juu ya Hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango ambaye yeye ndio jicho letu, Serikali nzima pamoja na Wizara zote husika yeye ndio baba.

Mhe. Mwenyekiti na mimi nimeona nichangie katika maeneo tofauti tofauti ambayo Mhe. Waziri ametusomea hotuba zake, lakini kabla ya kuchangia naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wakuu wote kwa kutuwasilishia Mpango huu au bajeti hii iliyokuja kusomwa juzi hapa.

Mhe. Mwenyekiti kwanza mimi nakuja katika kitabu cha Hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango, katika Hali ya Uchumi katika mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo kwa 2016/2017 katika ukurasa wa 6 *paragraph* 13 kitabu hichi kimesema ili kipate maendeleo endelevu ya jamii yetu tunahitaji uchumi wetu ukuwe vyema kila mwaka na kuwanufaisha wananchi walio wengi, niwashukuru sana kwa kuliona hilo na kwa kujua hilo. Lakini pia amesema kuwa mwaka 2011/2015 uchumi wetu ulikuwa kwa kiwango cha kuridhisha kwa wastani asilimia 7. Ukuwaji huu ulitokana na kuimarisha kwa sekta za viwanda, huduma, kilimo, uvuvi na misitu pamoja na sekta ndogo za ujenzi fedha na bima na usafiri habari na mawasiliano.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika kuliona hili nadhani mipango yote katika bajeti yake inatekelezeka au imetekelezwa kwa mujibu wa fedha walizojipangia, lakini nilitaka kujua Mhe. Waziri atakapokuja mfumo huu wa bajeti ambao tunaoutumia ni wenye kuzingatia matokeo, kama ni wenye kuzingatia matokeo na hapa wametwambia kuwa katika maendeleo endelevu, tayari imeonekana kuwa kuna ongezeko la ukuwaji wa

uchumi katika sekta ya kilimo, uvuvi na misitu, lakini nataka nijue imezingatia vipi kuhusiana na suala zima hli la kilimo hasa ukizingatia wanaohusika katika kilimo na uvuvi wengi ni wanawake. Kama wanawake umewazingatia vipi au ule ukuwaji na wao ni moja ni kali ya kuukuza uchumi, sasa hawa wanawake wao wamefaidika na nini. Je, wao wanawake katika sekta hii tayari na wao wamenufaika kwa sababu tayari uchumi umekuwa na tunategemea na hawa wazalishaji kwa kilimo au uvuvi na wao kwa vyovyote kipato chao kitakuwa kimeongezea, kwa hiyo tunataka tujuwe Mhe. Waziri atakapokuja katika majumuisho yake atueleze ni kwa kiasi gani hususan wanawake ambao wamo katika kilimo na uvuvi wamenyanyukaje. Hilo nilitaka nijue Mhe. Waziri atakapokuja atwambie.

Lakini pia niendelee katika kwa ujumla kuhusiana na sekta ya afya. Mhe. Waziri tumepitisha bajeti ya wizara husika lakini na leo tunapitisha bajeti kama nilivyosema mwanzo kuwa yeye ndio baba wa Mawizara yote haya kwa mujibu wa fedha. Mara nyingi tukipita katika hizi wizara wana malalamiko kwa kutokuingiziwa fedha kwa wakati na hii inapelekea kuwa hata ule utendaji wao wa kazi zao unakuwa mgumu kwa hivyo nilikuwa namuomba Mhe. Waziri alibebe hili katika Sekta hizi za Afya na Elimu na mambo mengine. Lakini nazungumzia Sekta ya Afya na Elimu kwa sababu afya inawagusa wananchi moja kwa moja. Kwa hiyo hayo maendeleo hayawezi kupatikana kama tutakua hatuna afya au kitengo au sekta ya afya bila ya kuimarishwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika hii Sekta ya Afya katika bajeti ya Wizara ya Afya tuliambiwa hapa na Mhe. Waziri kimeanzishwa kitengo cha Saratani lakini, sijaona katika maelezo yake kuwa hichi kimepewa kipaumbele. Namuomba sana Mhe. Waziri na hili alipe kipa umbele kuhusiana na Sekta hii ya Afya kwa upande wa Kitengo cha Saratani. Mhe. Waziri kuna jengo au kituo jengo pale hospitali ya Mnazi Mmoja limetengwa kwa ajili matibabu ya saratani kwa hatua zile za awali, na Mhe. Waziri wa Afya alizungumza kwa mapana yake hapa na akasema kuna madaktari bingwa wawili wakuhusiana na haja masuala ya saratani lakini, lakini tumegundua kuwa ni watu wengi wanaathirika na haya mambo ya saratani na matibabu yake makubwa lazima tusafiri twende Tanzania Bara.

Mhe. katika maelezo ya Mhe. Waziri wa Afya alizungumzia sana kuhusiana na kichi kitengo kuwa kitatoa huduma za awali lile jengo mpaka leo lipo limeshatengwa, jengo hilo lilikuwa ni hospitali ya watoto na wao wamehamishiwa katika jengo jipya lakini jengo lile mpaka hivi sasa bado halijafanya kazi na lipo tu limekaa halina kitu chochote ambacho kinafanyika na badala yake linaanza kutaka kuvunja au limeshaanza kuvunja na kutaka kuharibika, kwa hiyo namuomba Mhe. Waziri wa Fedha alione hili katika Sekta ya Afya ili wananchi wetu waondokane na ule usumbufu wa kwenda kupata zile huduma ya awali kule ocean road ibakie kama kama alivyosema Mhe. Waziri kule waendele kwa ajili ya miyonzi. Lakini inawezeka na hao madaktari bingwa tunao wa kutoa zile huduma za awali katika Kitengo kile, kwa hiyo namuomba sana Waziri katika Mpango wake kazi huu na suala hili walizingitie kwa imani yao. Kwa sababu wananchi wetu wanapata tabu na mara nyingi ndio wanaoathirika na hili na uwezo wao ni mdogo na niduni.

Lakini pia nataka niende katika Sekta hii ya Elimu. Mhe. Waziri Sekta ya Elimu kama nilivyosema ni Sekta mama pamoja na Wizara ya Afya ili tupate madaktari wazuri,

lazima wapate elimu iliyokuwa bora, lakini pia tumeona kwamba Serikali haina ajira lakini katika sekta ya elimu kuna vyuo vya elimu vya mafunzo ya amali, mara nyingi vituo hivi vidogo vimesahaulika. Na vimesahaulika na vinatoa huduma nzuri na kinaweza kikatoa vijana sekta ile wakatoka vizuri katika sekta ile na wanapata mafunzo. Mhe. Mwenyekiti katika hivi vyuo vya elimu vya mafunzo ya amali kuna kituo cha elimu Mkokotoni, kuna kituo Mwanakwerekwe kuna kituo pia hata kule Forodhani vile vyote vijana wengi wanakwenda pale kupata mafunzo. Lakini chakusikitisha bado Serikali haijaipa kipaumbele au umuhimu wa kuona kitengo kile kukiingizia fedha za kutosha kwa ajili ya vifaa vya ufundishaji wa wale vijana wetu wanaokwenda pale. *(Makofi)*

Kwa hio nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri katika mipango yake na kipa umbele vyake ili vijana waondokane na ile kuwa lazima wapate ajira Serikalini, lakini vitengo vile kama tutaviimarisha na kuviwekea miundo mbinu iliyobora basi nna imani tatizo hili linaweza likaondoka kwa namna moja au nyengine lakini Serikali au Wizara ijidhatiti kuona hili suala wana lipa kipaumbele kwa ajili ya manufaa ya vijana wetu, pamoja na wananchi kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti mimi nikuwa nataka nichangie hayo machache ambayo nimeyaona na Mhe. Waziri ili nayeye alifanyie kazi suala hili niseme kuwa kwa niaba ya mwananchi wa Jimbo la Chukwani tunaunga mkono hii bajeti kwa sababu ni Waziri msikifu na Waziri mahiri atafanya yale ambayo kama alivyoyaeleza katika hizi hotuba zake na mipango kazi na kila kitu ambacho kimetolewa humu, pamoja na mapendekezo ya Kamati pamoja na michango mbali mbali ya Waheshimiwa Wawakilishi wa humu ndani nna imani atayachukua na kuyafanyia kazi kwa maslahi ya Zanzibar na kwa maslahi ya wananchi wetu. Naunga mkono hoja asilimia 100 ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sasa ninamwita Mhe. Rashid Makame Shamsi na kama muda utatosha nitamwita Mhe. Hamadi Abdalla Rashid umaarufu Gei umalizie. Ahsante Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuichangia hotuba hii muhimu ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Lakini vile vile, nianze kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Khalid Salum na watendaji wake wote kwa uwasilishaji wa bajeti hii ambayo ni bajeti kwa ufupi inatowa matumaini makubwa sana kwa mwananchi wa kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze vile vile, Kamati ya Bajeti ikisimawiwa na Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) kwa yale majumuisho waliyoyafanya na hatimae kuwasilisha hapa katika Baraza letu Tukufu, nimpongeze sana Mhe. Dimwa kwa uwasilishaji wake.

Mhe. Mwenyekiti kwa nilivyoipitia bajeti hii, ni bajeti ambayo imewagusa wananchi wa kawaida na imewafikiria sana na kuwajali wananchi wetu, bajeti hii inavyoonekana hakuna ongezeko la kodi ambalo hili ni jambo moja muhimu sana kwa wananchi wa

kawaida. Kwa sababu kadri utakavyoengeza kodi maana yake unamuumiza mtu wa chini lakini vile vile, inaonesha kwamba tuna mipango na mikakati ya kuweza kudhibiti mianya ya mapato, kutokana na taratibu za ki-eletroniki ambazo zitatumika katika kudhibiti suala hili. Lakini vile vile, imeangalia suala zima la kuongeza pencheni kwa waastafu wetu ambao wanalalamika kwa kipindi kirefu lakini imezingatia vile vile, huduma mbali mbali za kijamii kama afya, maji, elimu na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti niipongeze sana kutokana na bajeti hii na ukuwaji wa kiuchumi wa nchi yetu pamoja na kwamba kipato chetu kinaongeza lakini wakati mwengine mwananchi wa kawaida yeye anaona kila siku anadidimia, lakini tuipongeze sana Serikali kwa kuweza kuhakikisha kwamba uchumi wa nchi yetu unakuwa siku hadi siku. Lakini hapa nichukue fursa hii ya kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania John Pombe Magufuli, kwa kile kitendo alichokifanya cha kuhakikisha kwamba uchumi wa Tanzania unanyanyuka kwa kuweza kuangalia vyanzo vyote vile vinapoteza mapato ya nchi hii tumpongeze sana Mhe. John Pombe Magufuli kwa maamuzi yake magumu. Mimi nna imani kwamba maamuzi kama haya ya Rais wetu wa Tanzania kama na sisi tutayachukua katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar basi bajeti yetu au zetu kwa miaka inayokuja haitakuwa tegemezi, nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha aweze kulisimamia hili na nina imani kwamba analiweza na linawezekana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti nielekee katika kitabu chetu kwenye mazingatio ya Serikali, katika mazingatio ya Serikali kuna suala la fedha ambazo zimetengwa bilioni 18 kwa ajili ya ununuzi wa meli mpya ya mafuta, lakini bado inaelezwa kwamba inafanyiwa kazi ile dhamira ya ununuzi wa meli nyengine ya abiria, niipongeze sana Serikali lakini nitowe indhari katika hili juu ya maamuzi sahihi na mikataba imara ambayo itatufanya sisi tuweze kupata meli ambazo ndizo ambazo zinaendana na viwango tulivyovitaka.

Mhe. Mwenyekiti utakapopata meli ya mafuta na meli ya kawaida hii ya abiria, mimi nina imani kwamba kwa suala zima la uchumi katika suala la usafiri basi tutapiga hatua. Lakini vile vile, katika mazingatio mengine kuna shilingi bilioni 2 ambazo zimetengwa kwa ajili ya uwazishaji wa Bima ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti hili ni jambo zuri sana katika kukuza Sekta ya Afya na wananchi wa Zanzibar wanalisubiri kwa hamu sana, wasi wasi wangu ni kwamba fedha hii imetengwa lakini hadi leo Baraza hili halijapokea Sheria inayohusiana na Bima ya Afya sidhani vile vile, kama kuna Sera ambayo tayari imeandaliwa kwa ajili ya Bima hii ya Afya kwa hiyo niombe sana Serikali, fedha zimetengwa lakini kunahitaji maandalizi, kwanza ipatikane sera madhubuti ambayo itasimamia huduma hii ya Bima ya Afya lakini vile vile, Sheria ya kuweza kusimamia Bima ya Afya Zanzibar kwa upande wa hospitali zetu, Mhe. mwenyekiti kunahitaji maandalizi makubwa ili wananchi ambao watakuja kuchukua Bima ya Afya waweze kuona kwamba fedha zao zinawanufaisha pale wanapoenda katika hospitali zetu na kuweza kupata huduma kwa mujibu wa Bima zao. Hivi sasa inajionesha kwamba bado kuna hospitali zinachukuliwa Bima ya Afya, lakini wananchi wanapokwenda wanakuta huduma zile ziko duni haziendani na kila ambacho wamekilipa.

Mhe. Mwenyekiti nije sana katika mazingatio kwenye fedha za mtaji ambazo zinatarajiwa kuwekezwa kwa wakala wa uchapaji shilingi bilioni 1.5. Mhe. Mwenyekiti tuna Wakala wa Uchapaji na tuna mategemeo sana wa kiwanda hichi au Wakala huyu kuweza kuzalisha kutokana na huduma za uchapaji wa kazi za Serikali lakini hata kazi za wananchi na wateja wengine wa ndani na nje ya nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti kuwekeza fedha ni kitu kimoja lakini jinsi ya gani yakuweza kuuendeleza ule mtaji ambao tumewapa ni kitu chengine, tunahitaji mazingatio sana kwamba wenzetu hawa Wakala wa Uchapaji kabla hatujawapa hizi fedha za kuwekeza lazima tuhakikishe kwamba wana mpango kazi, na mikakati mizuri ya kibiashara ambayo inaweza kuleta tija kwa taifa letu. Lazima wazingatie masoko na lazima waweze kujitangaza ndani na nje ya nchi ili fedha hii ya wananchi ambayo itawekezwa pale iweze kuleta tija. Lakini vile vile kunajionyesha kwamba taasisi hii kabla ya kuwa wakala ilikuwa ina madeni mengi. Kunaulazima kwanza kuwa na mikakati ya kuweza kurejesha madeni ili kuweza kuona kwamba wakala huyu anafanya kazi ile ambayo itaweza kuiletea serikali mapato.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika suala la ajira na uchumi, kadri uchumi unavyoongezeka matarajiyo yanaonyesha lazima kuwe na ongezeko vile vile la ajira. Inapotokezea uchumi umepanda lakini hakuna ongezeko la ajira hivi vitu kidogo vitakuwa vinakwenda tofauti. Kwa sababu hata mwananchi wakawaida tu uchumi wake unapopanda maana yake ana uwezo wa kuwatuma watu wengine. Katika suala hili serikali ina haja ya kuweza kushajihisha na kuweza kuwekeza katika suala zima la kuhakikisha vijana wanapata kujiajiri au kuajiriwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo, kuna vijana wengi wanaomaliza sekondari, wanaomaliza vyuo vya ufundi, wanaomaliza vyuo Vikuu, lakini tatizo lipo katika *mindsets* zao, wengi wao *mindsets* zao ziko katika ajira kutoka serikalini. Hii ni hatari kwa sababu ndani ya serikali ajira zilizopo ni chache mno. Inashangaza sana hata wale vijana ambao wamepata elimu ya mafunzo ya amali basi vile vile utashi wao ni kuajiriwa na serikali. Sasa nafikiri kuna kazi ya kuweza kubadilisha *mindsets* za vijana wetu katika mitaala ambayo tunaitumia ili kuweza wenyewe kujiona kwamba elimu na ujuzi wanaoupata basi unawawezesha kujiajiri.

Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu chetu nimeona kuna programu hii ya kuendeleza na kukuza ajira kwa vijana ambapo kituo cha kulelea wajasiri amali ambacho kipo Mbweni imeweza kuwapatia mafunzo vijana 53 mafunzo yanayohusiana na usarifu wa mazao na matunda ya mboga mboga ni jambo zuri sana. Lakini vile vile kuna vijana 124 walipata mafunzo ya ujasiri amali ya nadharia na vitendo.

Mhe. Mwenyekiti, hapa ningetaka kujua tu kwamba vijana hawa ambao tayari wamekwisha andaliwa ili waweze kufungua viwanda vidogo vidogo vya kuweza kusarifu mazao haya, sijui serikali tumewasaidia vipi. Kwa sababu tunaweza tukawa na vijana ambao tumewapa mafunzo lakini tukiwafuatilia basi pengine mafunzo yale wameyawacha pale pale katika kituo.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na tunakoendelea katika uchumi wa viwanda vijana hawa ambao wamepatiwa mafunzo haya ya usarifu wa mazao na matunda wangeweza kukusanywa na hatimaye kuwezeshwa kufungua viwanda vidogo vidogo vya kuweza kusarif hayo mazao, hapo nina imani itakuwa tumewatendea haki na wanaweza kujiajiri. Lakini kwa kuweka figa tu kwamba tumetoa wangapi bila ya kufanya *follow up* nafikiri haitatusaidia. Kama halijafanyika hili ningependa sana niiyombe taasisi inayohusika kuweza kuona kwamba mafunzo tuliyowapa vijana hawa yanaleta tija kwa taifa letu na hatimaye kuweza kukuza uchumi na vipato vyao wenyewe lakini vile vile kukuza uchumi wa serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika gawiwo la fedha la Mashirika ya Serikali katika ukuwaji wa uchumi serikali yetu inaasilimia fulani ya kipato ambacho kinatokana na gawiwo la fedha kutoka kwenye Mashirika ya Serikali, imeelezwa hapa mchango wake ni shilingi bilioni 4. Wenzangu wamezungumza juu ya hili hata na mimi sijaridhika sana na kiwango hichi cha pato linalotokana na gawiyo kutoka Mashirika ya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo ambalo hivi sasa linajitokeza kwa mashirika yetu haya kutoa uwakala. Suala la mashirika yetu ya serikali kutoa uwakala wakati mwengine unapoteza fedha nyingi kutokana na baadhi ya mawakala wetu wanakuwa siyo waaminifu. Kwa mfano ukielekea Shirika la Bima. Shirika la Bima imewapa uwakala watu mbali mbali, lakini kinachojitokeza ni kuongezeka kwa bima ambazo ni feki. Hapa maana yake anafaidika wakala, wakati serikali haiwezi kupata kipato na inawezekana vile vile kuna wakala wa mashirika mengine.

Ningeishauri serikali kuweza kuangalia kama kuna ulazima wa kuweza kutoa uwakala katika mashirika yetu basi tuangalie uwadilifu na uwajibikaji mzuri wa wakala hawa. Vyenginevyo itakuwa ni njia moja wapo ya kuweza kusababisha mianya ya kuvuja kwa mapato yetu kutokana na mawakala ambao siyo waaminifu na sio waadilifu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kukua kwa uchumi wa nchi yetu kunategemea sana uzalendo wa watendaji wetu. Kunategemea sana uwadilifu wa watendaji wetu, lakini inategemea sana uwajibikaji wa kila mmoja. Mimi nafarajika sana kwa kuiona Bajeti hii inaangalia suala zima la kuweza kuangalia vyanzo vipya vya mapato. Niishauri sana serikali katika miradi ya kimaendeleo ambayo imetajwa katika hotuba hii lazima iweze kuangalia kwamba mikataba yetu ina ubora, ina uwazi, lakini vile vile mikataba hii inafungwa na wanasheria ambao ni waadilifu.

Mhe. Mwenyekiti, uchumi wa nchi yetu kwa kweli umeathirika sana kutokana na mikataba mibovu. Tukiangalia majengo yanayojengwa barabara zinazojengwa na humu tunaona kwamba kuna maskuli yatajengwa kuna barabara zitajengwa, ningependa sana tusirudie kuliko toka, lazima tuweze kutandika misingi mizuri sana ya kuweza kuona kwamba mikataba yetu inakuwa ina uwadilifu ili kuweza kuona nchi yetu inaweza kupiga hatua kubwa za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya haya nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nikupongeze na mimi niseme tu naiyunga mkono hotuba hii ya bajet kwa asilimia 100 na niwaombe wenzangu vile vile waichaingiye na baadaye tuipitishe ili serikali ianze kufanya matumizi yake. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa dakika zetu zilizobakia ni kumi sasa nampa Mhe. Hamad Abdalla Rashid kwa dakika 9 amalizie katika siku yetu ya leo hii.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mimi kwa kupata nafasi hii ndogo ya kuchangia. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na serikali maana najikita sehemu moja tu hii hali ya ukuwaji wa uchumi nchi kwetu.

Inaonyesha dhahiri kwamba juhudi za Mhe. Waziri na serikali yetu inaonyesha kwamba kuna ukuwaji wa uchumi, kutoka asilimia 6.5 mpaka asilimia 6.8. Niipongeze serikali kwa ukuwaji huu ambao kwa kweli bado haujawa mkubwa wa kutosha nataka na mimi nisaidie namna gani ili uchumi huu utakuwa vya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianzie na sehemu ya ukusanyaji wa kodi. Inaonyesha dhahiri ukusanyaji wa kodi nchini kwetu mimi niseme haujakuwa katika mfumo mmoja kitu ambacho kinaonyesha dhahiri labda sekta binafsi au za serikali kuna udanganyifu ambao unapoteza kodi ile na kudumisha huu ukuwaji wa uchumi wetu. Mfano hai ule pale ambapo wafanyakazi hawa wa sekta binafsi au mashirika ya serikali wameachiwa kukusanya kodi ambayo sisi kama serikali tunasubiri mwisho wa mwezi kujua ni kiasi gani wanapata na nitoe mfano hai. Tuangalie kwenye Shirika la Meli au Shirika la Bakharesa au meli binafsi. Wana Mashine zao zinapokusanya kodi haziingii moja kwa moja kwenye mtandao wa serikali kuonyesha kwamba hapa sasa pameingia abiria wangapi. Tunasubiri mwisho wa mwezi kwenda kuuliza hivi mwezi huu umeingiza abiria wangapi au yeye anakuja kutoa tarifa ni abiria wangapi aliopata. Hapa serikali kama ingeweka mtambo wake wa kuonyesha kwamba akidota tu kule abiria 300 wameingia serikali imeshaelewa mpango wa ukusanyaji wa kodi ungekuwa mzuri na kodi hapa isingepotea.

Mhe. Mwenyekiti, nije tena katika sekta binafsi zaidi, serikali haiwezi kujua ni makusanyo gani yaliyopatikana pale kwa sababu wafanyabiashara wetu wengine siyo waaminifu wengine. Hata maduka zile risiti hawatoi pale anaweza akauza vitu chungumzima akashindwa kutoa risiti ambayo risiti ile ndiyo ingeweza kuingiza kodi serikalini. Mimi ningemuomba Mhe. Waziri angeweka mtango maalum au serikali kwa jumla tukajua kila sekta inayokusanya kodi ya serikali basi kodi ile akigusa inaingia kwenye mfuko wa serikali bila ya kwenda kuuliza, moja kwa moja iingie pale. Hapa kodi zitakwenda vizuri na tutakuwa hatuna wasi wasi wa kupotea.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Sekta ya Utalii, hivi sasa tunapata shida kujua watalii wangapi wanaingia nchi kwetu wamelala wapi, wanaondoka baada ya siku ngapi. Hii yote inachangia upotevu wa mapato kama laiti serikali ingeweka mdandao maalum wa kujua kuna watalii wangapi wameingia, wanabakia siku ngapi, wanalala hoteli ipi, basi tusingepata tabu kujua serikali inapata kiasi gani cha watalii wale walioingia nchini

kwetu. Matoke yake tunapitisha watu wetu ambao wafanyabiashara kama tunavyosema siyo waaminifu wanaweza kuwadanganya hawawapi ripoti kamili ya kuweza kujua kwamba ni kweli au sikweli na wengine hata kuwaficha kwenye mahoteli wanawaficha. Hapo pato la serikali linapotea tena.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kipaumbele cha kitabu cha Mhe. Waziri ambapo kipaumbele hiki kipo kwenye sekta ya viwanda. Mimi nimpongeze Mhe. Waziri na serikali kwa sekta hii ya viwanda kupewa kipaumbele. Sekta ya viwanda ndiyo sekta pekee ambayo ingeweza kutuondolea mfumuko wa bei. Kwa sababu tungeweza kujenga viwanda vyetu vya kutosha nchini kwetu, tukaweza kuzalisha kama Wizara ya Kilimo ikaweza kuzalisha mpunga wa kutosha yaani tukaiwezesha ikaweza kuzalisha mpunga wa kutosha kupitia sekta hii ya umwagiliaji, tukaweza kuwa na mchele wa hapa hapa nchini ungekuwa mchele mpya ambao wananchi wetu wangeupenda, lakini na bei tungekuwa tunapanga sisi wenyewe kwa sababu hichi kitu tunakizalisha wenyewe hapa hapa nchini.

Nije upande wa uvuvi wa samaki, kama tungewawezesha wavuvi wa samaki sekta hii ingepatiwa fedha za kutosha tukaweza kuwawezesha wavuvi wa samaki wa bahari kuu wakaweza kuvua na maboti ya kutosha. Tungeweza kuuza samaki hapa nchini ikawa tunauwezo kwanza wa ajira kwa vijana wetu lakini pato la serikali lingeweza kukua kwa kuuza samaki nchini na wengine kuwauza nchi za nje tukapata kodi kubwa ya kutosha kwenye nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kwenye mfumko wa bei Mhe. Waziri kasema hapa kasamehe kodi lakini wenzangu wamechangia na wakasema kwamba bado pamoja na kusamehewa kodi wafanyabiashara lakini bado bei zimefumko. Lakini ingelikuwa uzalishaji ule upo kwetu hapa, mchele wangezalisha kwetu, tukaweza kuzalisha mambo haya yangeondoka na serikali ingeweza kupata pato la kutosha kuweza kuwahudumia wananchi wetu.

Mhe. Spika, niende kwenye sekta ya makaazi holela, hapa mimi ningeshauri na mara nyingi serikali yetu inapofanya plani ya miji basi inafanye pengine mji wa Mjimkongwe au mji wa Mjini Magharib lakini Makunduchi hakuna plan kiasi kwamba wananchi wetu wanajenga nyumba ambazo hazipo katika *standard*, hetu tuone mfano wa Mhe. Marehemu Karume tungeweza kujenga majumba kama yale ya Michenzani tukayafikisha ng'ambu tu basi tungepata eneo dogo la makaazi ya watu lakini tukapata eneo kubwa la kuweza kujenga viwanda na sehemu kubwa ya kilimo. Pale uzalishaji ungekuja wa kutosha tukaweza kujua tunafanya nini na tuko wapi. Lakini leo huu ujenzi wa nyumba ndogo ndogo unachukuwa nafasi kubwa tunaimaliza nchi yetu kwa ujenzi holela. Tungeweka sehemu maalum ya kutenga kabisa kwamba maeneo haya ni maeneo ya kilimo, maeneo haya ni maeneo ya makaazi, maeneo haya ni maeneo ya makaazi ya viwanda. Tungeweza kufanya hivyo tungekuwa mbali na tungejipanga vizuri na tukaweza kudhibiti mapato yetu yakaenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, naona dakika zinamaliza nimalizie la mwisho nije katika vipaumbele vyengine ambavyo Mhe. Waziri ameviweka katika kitabu chake vya hii plan ambayo nimeshaisemeya lakini nirudie nyuma kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nchini kwetu tuna maeneo makubwa kwa mfano Pemba. Kuna maeneo makubwa ambayo sasa hivi yamekaa hayatumiki, lakini maeneo yale yanapotokezea muwekezaji au serikali inapotaka kufanya kitu basi wananchi wetu tayari pale wanavamia na wanasema ni maeneo yao, maeneo ambayo hayana chochote. Lakili serikali yetu kwa upendo wa wananchi wale wanalipwa. Tunalipa mijiti ambayo haina maana na wala hawakuilima, lakini serikali kwa upendo wa wananchi wake inawalipa. Nimpongeze Mhe. Rais hili liko wazi kabisa akija muwekezaji wananchi wa pale wananufaika na pato la muwekezaji ili waachie nafasi ile.

Mhe. Mwenyekiti, nafasi ile kama serikali ingelikuwa na plan ikajulikana kabisa kwamba nafasi ile imeshatengwa kwa plani ya makaazi ya viwanda, makaazi ya miji, serikali ingekuwa haipati hasara ya kuwalipa wananchi wake fidia ingejulikana kabisa.

Mwisho labda nimalizie kwa kumpongeza tena Mhe. Waziri na kuipongeza serikali katika kuhakikisha inakuza mapato ya nchi yetu ili wananchi wetu wapate huduma zinazotakikana.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia na moja juu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe nashukuru kwa utulivu wenu muda wote huo na michango mbali mbali ambayo kuwa imeweza kuchangiwa hotuba hii na hadi hapa itakuwa ni mwisho kwa muhula huu wa leo. Naomba niliakhirishe Baraza hili hadi kesho saa 3:00 za asubuhi. Chamsingi muwahi mapema kuwa katika nafasi zetu kabla ya muda haujapotea.

(Saa 9:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 16/6/2017 saa 3:00 za asubuhi)